

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 27 Juni, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill, 2022*).

MHE. TARIMBA G. ABBAS K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022 (*The Finance Bill, 2022*).

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 455

Ujenzi wa Barabara ya Utugi hadi Kirongwe

MHE. ESTHER N. MATIKO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Utugi hadi Kirongwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Utugi – Kirongwe yenye urefu wa kilometra 48 inaendelea kufanyiwa upembuzi yakini na usanifu wa kina. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2022. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Majibu ya Serikali kwa kweli yanaskitisha. Barabara hii ni ya ahadi tangu Awamu ya Tatu ya Hayati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Rais Mkapa. Sasa maswali yangu yangu mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, tuna barabara ya kiusalama ambayo iko Jimbo la Tarime Vijijini inayoanzia Jimbo la Rorya, inapita Susuni - Mwema - Sirari - Mbogi - Gwitio mpaka Nyanungu. Barabara hii imekuwa ikiahidiwa itajengwa kiwango cha lami mpaka leo. Ni lini sasa barabara hii itaenda kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuimarisha usalama pale mpakani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna barabara ya kuanzia Ut.cgi inapita Kowaki kwenda Kinesi. Ni barabara pia ambayo imeahidiwa toka Awamu ya Nne lakini mpaka leo haijajengwa. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi ukizingatia kule tuna ziwa, tunavua samaki na mazao mengine: Ni lini barabara hii itaenda kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuinua uchumi katika Jimbo la Rorya kwa ujumla?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG.GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja ya ulinzi ambayo inaanzia Kirongwe kupita Mribha hadi Kegongo ni barabara ya Ulinzi kati ya Tanzania na mpaka wa Kenya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa Serikali inahakikisha kwamba barabara hii inapitika muda wote wa mwaka. Kwa hiyo, imetengewa fedha kuhakikisha kwamba inatengenezwa kwa kiwango cha changarawe ili iweze kuitikika kuimarisha ulinzi.

Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja ya Kowaki kwenda Kinesi tunajua inaunganisha Kowaki na Hadari, na ni kweli ni barabara ya uchumi sana kwa Mkoa wa Mara na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hasa kwa Jimbo la Rarya. Tunachofanya sasa hivi pia ni kuhakikisha kwamba tunatenga fedha; na ukiangalia kwenye bajeti ya mwaka huu, tumetenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba tunaitengeneza iweze kuitikika wakati huo Serikali inatafuta fedha ili ianze kufanya kufanya usanifu wa kina. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa barabara ya Kahama - Bulige Mwakitalio mpaka Solwa ni barabara ya kimkakati na iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi; je, ni lini ujenzi wa kiwango cha lami utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG.GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Kahama kwenda Solwa imeshafanyiwa usanifu wa kina na sasa Serikali inatafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Agnesta Lambert, swali la nyongeza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Barabara ya Morogoro - Dodoma ni barabara ambayo inatumiwa na wananchi wengi na hususan viongozi wa kiserikali na wanadiplomasia wa kigeni wanapokuwa wanatembelea Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imekuwa chakavu maeneo mengi na hususani kutoka Dumila – Gairo: Swali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

langu, Serikali inampango gani wa kujenga barabara hii ili kuondoa vifo vya ajali vinavyotokea na kunusuru Maisha ya wananchi? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG.GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii imechakaa na *traffic* imeongezeka sana. Tayari tumeshafanya usanifu wa kina ikiwa ni pamoja na kuipanua hii barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti tunayolendea sasa hivi, maeneo mengi ambayo ni korofi yatakarabatiwa ikiwa ni pamoja na mpango wa kuifumua barabara nzima ili kuipanua na kupunguza hizo ajali na mashimo ambayo yapo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

MHE. IDDI K. IDDI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara inayotoka Bulyanhulu kwenda Kahama ni barabara ya kimkakati na inachangia pato kubwa katika nchi hii. Sasa swali langu lilikuwa: Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii ambayo kimsingi ni barabara ya muda mrefu na ni muhimu sana katika Jimbo la Msalala? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG.GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja kutoka Bulyanhulu kwenda Kahama ipo kwenye mpango wa bajeti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tuliyoiopanga na pia ni barabara ambayo wenzetu wa Mgodi wa Tembo Barrick wamekubali kuisaidia Serikali kuijenga hiyo barabara. Kwa hiyo, tayari Serikali inaendelea na mazungumzo na wenzetu, lakini pia Serikali imepanga bajeti kuanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza Naibu Waziri wa Ujenzi: Ni lini Serikali itatafuta fedha ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Amkeni – Kitangali hadi Mtama kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG.GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna Mtanda, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoanisha Serikali inaitambua. Tutakamilisha kwanza kufanya usanifu wa kina halafu baada ya hapo, Serikali itatafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, swali la nyongeza.

MHE. MWITA B. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali la nyongeza. Barabara ya Nyamswa – Bunda – Bulamba na barabara ya Sanzate – Mgeta – Nata, wanachi wamebomolewa nyumba zao. Ni lini wananchi hao watapewa fidia ya nyumba zao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Getere Mbunge wa Mbunda Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara mbili alizozitaja ya Nyamuswa – Bunda kwenye Bulamba na Nyamuswa kwenda upande wa Nata ni barabara ambazo zinajengwa kwa kiwango cha lami. Tayari tulishafanya tathimini na sasa hivi Wizara ya Fedha inafanya uhakiki wa mwisho ili kuandaa malipo kwa wananchi ambaa wamepisha ujenzi wa hizo barabara mbili. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swalii la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini barabara ya kutoka Lyazumbi hadi Kabwe itajengwa kwa kiwango cha lami? Kwa sababu kule kuna bandari kwa uchumi wa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Lyazumbi – Kabwe ni barabara ambayo ilikuwa finyu. Cha kwanza ambacho Serikali imefanya baada ya kujenga bandari ilikuwa ni kuipanua ile barabara ili iweze kupitisha magari makubwa na pia kujenga madaraja ambayo sasa yanaweza yakahimili magari yenye uzito mkubwa na hatua ya sasa ni kukamilisha usanifu ili kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 456

Kuanza Ujenzi wa Treni ya Mwendokasi kutoka Kaliua - Mpanda hadi Karema

MHE. FATMA H. TOUFIQ K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa treni ya mwendokasi kutoka Kaliua-Mpanda hadi Karema?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia *TRC* imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia ya reli ya Kaliua – Mpanda – Karema kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa reli hii. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Fatma Taufiq, swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TAUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa reli hii ni muhimu sana kwa uchumi wa ukanda wa Kusini Magharibi na pia ni muhimu sana kwa usafirishaji mizigo kwa nchi jirani za Kongo, Burundi na Rwanda: Je, Serikali haionti sasa imefikia wakati kuharakisha kujenga reli hii ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata tija? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii moja la nyongeza la Mheshimiwa Taufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali inatambua umuhimu wa reli hii na inatambua kwamba nchi jirani kama Kongo, Zambia ni wadau wetu na ndiyo tunaofanya nao kazi na mizigo mingi inatoka katika hizo nchi. Kwa maana hiyo, Serikali kuitia bajeti yake ya mwaka wa fedha ujao wa 2022/2023 imetenga kiasi cha shilingi 199.4 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hii.

SPIKA: Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swalii la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kukamilika kwa barabara ya kutoka Tabora kwenda Mpanda na kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Karema ni kishawishi kikubwa sana cha nchi jirani ya DRC Congo kutumia huduma ya bandari ile, na wameshaanza kuleta hiyo huduma:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa haraka zaidi kukamilisha kile kipande cha ujenzi wa kutoka Mpanda kwenda Karema ili kiweze kuwa kiunganishi na nchi jirani?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Kakoso hicho kipande ni cha barabara au ni cha treni.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, ni cha reli, cha kutoka Mpanda kwenda Karema.

SPIKA: Maana ulianza kwa maelezo ya barabara, sasa nikataku kujiridhisha, wa barabara ameshatoka hapa mbele. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba kwanza tumejenga hiyo bandari ya Karema na upande wa pili ni Karemii kwa wenzetu Congo na Wizara kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kukamilisha kipande hiki cha Mpanda – Karema. Ndiyo maana tumetenga kiasi hiki cha fedha kiasi cha Shilingi 199.4 ili iwe na tija hiyo barabara na bandari yetu ambayo tumejenga ya Karema. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ujenzi wa Treni hauwezi ukaacha mbali ujenzi wa vituo vya reli, kituo cha reli cha Mpanda ni chakavu, Waziri anasema nini katika kuhakikisha kituo kile kinajengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Kapufi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua kipande hiki cha kutoka Kaliua – Mpanda kina changamoto ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

miundombinu pamoja na *station*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika bajeti ambayo Bunge imetu idhinishia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuititia *TRC*, Shirika letu la Reli Nchini, tumetenga kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa *station* iliyopo pale Mpanda Mjini pamoja na kuboresha miundombinu mingine katika Reli hii ya Mpanda – Karema. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Japhet Hasunga, swalii la nyongeza.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Ahsante sana. Kuna treni ya *TAZARA* ambayo inatoka Dar es Salaam mpaka Tunduma. Je, upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inaipanua treni hiyo ili iwe ya mwendokasi na iweze kukidhi mahitaji ya nchi yetu kwa Nyanda za Juu Kusini? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii moja la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba reli yetu ya *TAZARA* inaongozwa na nchi mbili kati ya Tanzania na Zambia. Kumekuwepo na changamoto nyingi katika uendeshaji wa reli hii, lakini habari njema ni kwamba ndani ya mwezi huu ifikapo tarehe 30 ya mwezi huu Mawaziri wa pande zote mbili kutoka Tanzania na Zambia watakutana. Lakini pili, tunataka tubadilishe Sheria. Hivi sasa Sheria inayotumika ni Sheria ya tangu ilivyoanzishwa *TAZARA*. Sasa sisi upande wa Tanzania tukitaka tuwekeze tunashindwa kwa sababu ile Sheria imetubana. Tayari maandiko au maandalizi ya Sheria hii imeshapitishwa. Kwa hiyo tunasubiri sasa kikao hicho cha Mawaziri watakapokaa halafu hizo Sheria zije ndani ya Bunge la Tanzania za upenda wa Zambia ili tuweze kuhuisha hii reli. Ahsante. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo, swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kujua Serikali imefikia hatua gani katika ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara mpaka Bambabeyi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli reli yetu ya kutoka Mtwara kuja Bamba Bay pamoja na matawi mawili ya Liganda na Mchuchuma imetengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 100, lakini pia tumepeata ufadhlili wa *SADC* kiasi cha dola za Kimarekani milioni sita. Na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tayari umekwishafanyika katika reli hii. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha treni inayotoka stesheni kwenda Pugu inayojulikana kwa jina la treni ya Mwakyembe kwa kuweka miundombinu ya vituo ili kuepusha ajali zinazojitokeza baina ya treni na magari?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, ni kweli treni hizi ambazo zinatusaidia sana Mji wa Dar es Salaam, hususan kipindi cha asubuhi na jioni ambacho kunakuwa na foleni kubwa kuna changamoto baadhi ya maeneo. Sisi upande wa Shirika, kuititia Shirika letu la reli nchini tumejipanga kuboresha maeneo yote hususan maeneo yale ya makutano kati ya barabara na treni ili kuweka alama. Na alama hizi zitaenda na elimu pia kwa jamii katika mazingira hayo kwa sababu wakati mwagine treni inapopita kunakuwa na changamoto pia ya watu kupita na huwa zinatokea hizo ajali. Kwa hiyo tumejipanga kutoa hiyo elimu, lakini tutaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Dola hususan Polisi kwa ajili ya kuelimisha jamii katika maeneo hayo ambapo kuna makutano kati ya barabara na reli. Ahsante. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Daktari Christine Ishengoma, swalii nyongeza.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naishukuru Serikali na baada ya kuishukuru Serikali, nauliza kuwa ni lini reli ya Mwendokasi kuanzia Dar es Salaam mpaka Morogoro itaanza kazi, tegemeo la Serikali? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kutoa fedha takribani zaidi ya trioni 6.5 kwa Wakandarasi wote katika *Standard Gauge*. Lakini pia tumeingia Mikataba zaidi ya dola la Kimarekani bilioni 7.2, takribani trioni 15 pamoa na VAT. Sasa reli hii ya kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro yenye urefu wa kilomita 300

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunategemea itaanza rasmi mwezi wa tisa, *operation* zake zote zitaana mwezi wa tisa. Na mwezi wa Nane yataingia yale mabehewa pamoja na vichwa; kwa sababu sasa hivi tunachokifanya ni kufanya *testing* kwa maana ya vituo, stesheni kwa stesheni, umeme, *signals* na kila kitu ndicho kinachofanyika kwa wakati huu. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Ninajua kabisa uchumi wa Nyanda za Juu Kusini unategemea pia reli ya *TAZARA*. Tunajua kwamba kama ulivyo sema mnataka kubadilisha Sheria lakini bado mabehewa ni chakavu na wateja ni wengi. Tunajua tukitumia treni hiyo tutasaidia kurahisisha barabara kupona wakapeleka kwenye treni. Ni lini Serikali sasa itawekeza zaidi kwenye kuleta mabehewa mapya na kutengeneza miundombinu vizuri?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo jibu swali la nyongeza kupitia Mheshimiwa Japhet Hasunga, kwamba kilichokuwa kimetubana sana kama nchi ilikuwa ni Mkataba tulioingia.

Kwa hiyo ulikuwa huwezi kufanya namna yoyote ile hata kama nchi inatoa trioni moja hivi sasa, lakini upande wa pili wasiwekeze chochote *automatically* hiyo fedha baadaye mtagawana *equally*. Kwa hiyo mwarobaini wa *TAZARA* ni hii Sheria ambayo nimesema tarehe 30 Juni, 2022 Mawaziri wetu watakutana na Sheria ile itakuja ili na sisi tuwekeze upande wa Tanzania na wao wawekeze upande mwengine.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge pia kwamba Sheria iliyopo kwa sasa inaruhusu pia wawekezaji binafsi. Kwa hiyo kupitia *PPP* tunawakaribisha wawekezaji ili tuweze kununua hayo mabehewa. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Daktari Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 457

Mabadiliko na Sheria ya hakimiliki Sura Na. 218

MHE. DKT. RITTA E. KABATI aliluliza: -

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki ili iwezeshe Mkataba wa Marakesh kutekelezeka kwa mujibu wa Sheria?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Pauline Gekul, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Daktari Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria tajwa yalishashaletwa Bungeni na kupitishwa tarehe 7 Februarri, 2022. Kwa sasa Serikali ipo katika utaratibu wa kuandaa Kanuni za kusimamia Mamlaka ya usimamizi na kuiwezesha kibajeti kwa lengo la kuhakikisha wanufaika wa Mkataba huu wa Marsakesh wanapata machapisho mbalimbali watakayohitaji katika upataji wa Elimu na Habari ikiwa ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pamoja na kudhibiti machapisho ambayo yatakua kinyume na utaratibu na sheria za nchi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Kwanza nianze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ajili ya majibu haya ya Sheria hii ya Marakesh.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria hii inaruhusu *Authorized Entity* inaweza kuzalisha kazi ya msanii bila idhini yake kwa matumizi ya *beneficially person*. Je, Serikali imewajulisha wadau juu ya hili?

Swali langu la pili, je, mchakato wa Kanuni unategemea kukamilika lini ili wanufalka hasa watu hawa wenye ulemavu waweze kunufaika na sheria hii? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta, kwamba wadau wameshirikishwa wakati wa kuandaa Sheria hii. Lakini kama kutakuwa na uhitaji wa kuendelea kuwashirikisha Wizara yetu iko tayari kuendelea kuwashirikisha.

Mheshimiwa Spika, lakini swali lake la pili, alipenda kufahamu ni lini Kanuni hizi zitakamilika. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba tarehe 07 Februari, 2022 tulipitisha Sheria hii. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta kwamba Kanuni zipo katika hatua za mwisho zikikamilika wadau pia tutawashirikisha waweze kuzifahamu. Ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Aaah, kuna swali lingine, Mheshimiwa Hamisi Mohamed Mwinjima, Mbunge wa Muheza.

Na. 458

Taasisi binafsi kukusanya mirabaha kwa niaba ya Wasanii

MHE. HAMISI M. MWINJUMA aliuliza:

Je, kuna mpango gani kuruhusu watu/taasisi binafsi hasa za wasanii kukusanya mirahaba maeneo ya wazi yanayotumia kazi za sanaa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuruhusu watu binafsi na Taasisi kuanza kukusanya mirabaha na tayari mapendelekezo yameshaletwa kwenye *Financial Bill* ya mwaka 2022. Aidha, inapendekezwa *COSOTA* kubaki na jukumu la kusimamia Hakimiliki na jukumu la ukusanyaji na ugawaji wa Mirabaha kwenda kwa Taasisi au Wadau binafsi yanii *Collective Management Organizations (CMOs)*. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Hamisi Mohamed Mwinjuma, swali la nyongeza.

MHE. HAMISI M. MWINJUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu ya kutia moyo ya Serikali. Na nina swali moja tu la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa vile suala hili linakuja na maslahi makubwa ya kiuchumi na kuna Ushahidi wa migongano katika maeneo kadhaa ambayo *CMOs* zimewahi kuruhusiwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha migogoro miongoni mwa *CMOs* hizi binafsi haitakuwepo? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, nikushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza moja la Mheshimiwa Hamisi Mwinjuma, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Sheria hii illipoanza kutekelezwa kwenye nchi zingine kuna migogoro ilijitokeza baina ya wadau. Sisi tumejipanga baada ya hili kupitishwa na Bunge hili tutakaa na wadau wote wa tasnia mbalimbali katika sanaa, kama ni wanamuziki wa Injili, kama ni wanamuziki wa Kizazi Kipyta tutakaa nao. Tutahakikisha Uongozi wao tunauimarisha, lakini pia wanafahamu kwa nini *CMOs* zikakusanye na *COSOTA* itasimamia suala zima, kuhakikisha kwamba hawa watu hawaingii kwenye mgogoro.

SPIKA: Tunakushukuru sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 459

Hitaji la jengo la Mahakama ya Wilaya – Hai

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga majengo mapya ya kisasa ya Mahakama ya Wilaya Hai kwa kuwa jengo la sasa ni chakavu?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipeleka wataalam na kubaini kuwa ni kweli Mahakama ya Hai ni chakavu na hivyo ilihitaji ukarabati. Ukarabati katika Mahakama hii ulishafanyika toka Februari, 2021.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli Mahakama hii imefanyiwa ukarabati lakini swali langu la msingi ilikuwa ni ujenzi wa majengo mapya ya kisasa ya Mahakama ya Wilaya ya Hai. Maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Wilaya ya Hai, Mahakama zake za Mwanzo takriban zote ni chakavu, Mahakama ya Hai Kati, Masama na Boma ya Ng'ombe. Lakini Mahakama ya Mwanzo Machame tumefanya ukarabati, tena kwa kutumia vyanzo vyta Mbunge mwenyewe, mimi mwenyewe na Mfuko wa Jimbo.

Swali langu, je, ni lini Mahakama hii kwa kuwa imeshakarabatiwa itafunguliwa na kuanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa Kata ya Rungugai, hususan Kijiji Kikafu Chini wanatoka mbali sana kufuata huduma za Mahakama huku Boma ya Ng'ombe.

Swali langu, je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya pale Rungugai ili iweze kuhudumia pamoja na Kata ya Mnadani?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nipende kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mafuwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudzi zake za kutusaidia kufanya ukarabati katika Mahakama ile ya Machame, na kwamba kwa sasa imeshakamilika na inangoja tu kufunguliwa. Niombe Mhimili wa Mahakama uweke ratiba ya haraka ili waweze kwenda kuifungua ile Mahakama na ianze kufanya kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali dogo la pili, Kata Rungugal lini tunakwenda kujenga Mahakama pale. Ni kwamba katika utaratibu wa kawaida nadhani Waheshimiwa Wabunge wote mnao, nimewatumia kwenye mfumo, mmeona jinsi mikakati ya ujenzi tuliyonayo. Kimsingi tunakwenda kuanza ujenzi wa kila Makao Makuu ya Tarafa kupata Mahakama ya Mwanzo. Kwa hiyo kutokana na Mheshimiwa Mbunge na juhudzi anazozionyesha tutampa ushirikiano wa kutosha, tutatemebelea lile eneo kuona namna kama ni Makao Makuu ya Tarafa *obvious* ipo kwenye mpango lakini kama ni kwenye Kata tu tulishaeleza mwanzo kwamba Kata itakayopata upendeleo ni ile iliyombali na huduma inayotolewa kwa sasa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mafuwe tutakuwa bega kwa bega. Kwanza kwa juhudzi zako ambazo umetuonyesha hatuhitaji kukuangusha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo katika Jimbo la Tabora Mjini karibu zote ni chakavu ikiwemo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mahakama ya Kata ya Isevya ambayo Mahakama ile ya Mwanzo mvua ikinyesha pale Isevya hata Mahakimu wanashindwa kuingia mle ndani kwa sababu maji yanajaa kwenye ile Mahakama.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati hizi Mahakama za Mwanzo katika Jimbo la Tabora Mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka Mbunge wa Tabora, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunakiri kwamba Mahakama nyingi zimechakaa sana hasa hizi za Mwanzo; na kama nilivyooleza wakati najibu hili swali la nyongeza la Mheshimiwa Mafue; ni kwamba tunakwenda kuanza ujenzi wa Mahakama zile zilizopo kwenye maeneo ya Makao Makuu ya Tarafa. Lakini mpango wa ukarabati unaendelea wa nchi zima unaendelea katika yale majengo ambayo tunaona yanafaa kufanyiwa ukarabati. Lakini Mahakama nyingi sana za Mwanzo ni zile ambazo hazina vigezo, nyingi zilijengwa katika nyakati hizo, nyingi zinahitaji kufanyiwa maboresho makubwa na hasa ujenzi mpya kabisa.

SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nanafasi nami ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nitoe shukrani zangu za dhati baada ya kupata fedha kwa ajili ya jengo la Mahakama ya Wilaya, lakini ziko Tarafa za Makata, Tarafa za Kibutuka, Tarafa hizi ziko mbali sana na hazina majengo ya Mahakama.

Je, Serikali ni lini itaona umuhimu wa kujenga majengo ya Mahakama kwenye Tarafa hizi mbili?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nipende kujibu swalii moja la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza tunapokea shukrani zako, na huu ndio mpango kazi wa Wizara kuhakikisha tunaboresha majengo yote ya Mahakama nchini. Kuhusu Tarafa hizi mbili, tukuahidi tu kwamba katika mpango unaokuja ambao ni kuanzia bajeti hii na kuendelea tunakwenda kuanza ujenzi wa Mahakama za Makao Makuu nchi nzima. Ifikapo 2025 kila Makao Makuu ya Tarafa itakuwa na majengo mapya ya Mahakama.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, swalii la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Na mimi nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kutujengea Mahakama ya Wilaya ya Bunda; imekamilika na inafanya kazi. Iakini katika Wilaya ya Bunda Mahakama za Mwanzo zina hali mbaya Nansimo, Jimbo la Mwibara wanatumia Ofisi ya Kata, haifanyi kazi, Mgeta, Jimbo la Bunda Vijijini, Kabasa Jimbo la Bunda Mjini, zote zina hali mbaya.

Je, ni lini mtatujengea Mahakama ya Mwanzo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nipende kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza tupokee shukrani zako kwa kukiri kwamba Serikali inafanya kazi. Suala la uchakavu wa Mahakama za Mwanzo kama nilivyojobu muda mfupi uliyopita, ni kwamba tunaendelea na mkakati wa ukarabati

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwenye majengo yale yanayowezekana kukarabatiwa. Lakini tunakwenda kuanza ujenzi wa Mahakama katika kila Makao Makuu ya Tarafa hapa nchini na ifikapo 2025 kama nilivyooleza hapo nyuma nchi nzima tutakuwa na Mahakama katika kila Makao Makuu ya Tarafa. Lakini mbali zaidi ni kwamba maeneo yote ambayo tutayabaini yako mbali na Makao Makuu ya Tarafa, vilevile yanaenda kupata upendeleo.

SPIKA: Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, swali la nyongeza.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Tarafa ya Kipatimu Jimboni Kilwa Kaskazini, shughuli za Mahakama ya Mwanzo zimekuwa zikiendeshwa katika Ofisi ya Afisa Tarafa.

Je, ni lini Serikali itawekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo maalum kwa ajili ya shughuli za Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Kipatimu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis, Mbunge wa Kilwa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyooleza huko mwanzo, najua wazi kabisa kwamba tuna mahitaji makubwa ya majengo ya Mahakama katika maeneo mbalimbali na kwamba mpango unaokwenda kuanza sasa ni kuhakikisha kwamba tunajenga Mahakama zetu katika Makao Makuu zote za Tarafa nchini. Lakini hapa Kipatimu ambapo unapozungumzia tutaangalia kama ni Makao Makuu ya Tarafa na kwa sababu kuna ushahidi wa kutumika jengo la Katibu Tarafa, basi ni sahihi kabisa kwamba mpango huu ambaeo tunaanza kuutekeleza kwenye mwaka huu wa bajeti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo mmeipitisha tunakwenda kuanza ujenzi katika maeneo hayo ambayo yamekosa Mahakama. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Henry Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Wilaya ya Mbogwe inazo Tarafa Tatu, Tarafa ya Rulembela na Masumbwe hazina Mahakama za kuridhisha.

Je, Serikali ni lini itaanza kujenga Mahakama katika hizo Tarafa ili wananchi waweze kupata huduma ya Mahakama?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maganga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli naendelea kurudia neno langu kwamba ni kweli nakiri kwamba kuna uchakavu mkubwa wa majengo katika maeneo mbalimbali ya Mahakama hapa nchini. Naomba nikiri kwamba vilevile Wizara yangu inafanya kila aina ya maboresho kwenye Mahakama na Waheshimiwa Wabunge wengi ni mashahidi tumeweza sasa hivi, tunayo miradi kama 22 kwa kipindi hiki tu cha mwaka kwa ajili ya kujenga Mahakama za Wilaya ambazo nchi nzima kila mahali pameguswa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la eneo hili la Mbogo Mheshimiwa Mbunge, nikuhakikishie Makao Makuu zote za Tarafa kwenye eneo hili zinakwenda kupata majengo mapya ambayo yatasaidia maboresho mazuri kabisa ya utoaji wa huduma za Mahakama. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mahakama yetu iliyopo Mlandizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, majengo yako yako katika hali chakavu sana, hayafai hata kukarabatiwa kwa kuwa yamejengwa kwa matope, miti na kusakafiwa simenti kwa juu.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha inatujengea majengo mapya? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mchafu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba maeneo mengi kama nilivyojieleza mwanzo majengo yake yamechakaa na mengi yalijengwa kwa kujitolea kupitia nguvu za wananchi huko nyuma na kama ilivyo Mlandizi walijenga jengo la tope.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kuanza ujenzi wa haraka katika maeneo yote niliyoyataja ambayo ni Makao Makuu ya Tarafa zote nchini, muda wowote kuanzia sasa baada ya bajeti hii kupita miradi mingi sana inakwenda kuanza. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Hawa utuvumilie kidogo katika safari hii ya ujenzi wa Mahakama na muda mfupi ujao utaona mabadiliko Mlandizi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Twaha Mpembewi swali la nyongeza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wilaya ya Kibiti ni moja katika Wilaya zilizopo ndani ya Mkoa wa Pwani lakini wakazi wa maeneo yale pamoja na Rufiji tunapata shida kubwa sana katika Mahakama ya Rufaa ambayo lazima waende Kibaha.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka pale Kibiti kuweza kuweza kuweka Mahakama ya Rufaa ya Kanda?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpembewi, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye maswali ya msingi ni kwamba tunakwenda kuanza ujenzi katika maeneo yote, ngazi ya Wilaya tunaendelea na miradi na tunayo miradi mpaka 2025 na Waheshimiwa Wabunge wote nimeshawatumia kwenye mitandao yenu, lakini kwenye Mahakama hizi za mwanzo tunakwenda kuhakikisha kwamba kwenye Makao Makuu yote ya Tarafa nchini tunapata majengo mapya ya Mahakama kwa maeneo yale ambayo hayakuwa na majengo kabisa.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tunaendelea na ukarabati kwenye majengo yote yanayorekebishika ambayo yanakarabatika.

Kwa hiyo, tuvute subira Waheshimiwa Wabunge ni mchakato ambao kufikia 2025 maeneo yote nadhani kutakuwa hakuna maswali Bungeni kuhusu Mahakama. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini sasa aulize swalii lake.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Na. 460

Serikali Kujenga Chuo cha VETA Wilayani Muleba

MHE. DKT.OSCAR I. KIKOYO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Muleba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Dkt. Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujenga Vyuo vya *VETA* katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi ambacho Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Muleba na maeneo mengine, wananchi wa Muleba wanashauriwa kuendelea kutumia Kituo cha Ufundidi Stadi katika Wilaya ya Muleba kinachoitwa Ndolage *VTC* pamoja na vyuo vya *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo ya ufundi. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma Kikoyo swali la nyongeza.

MHE. DKT.OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na ninaishukuru Serikali kutupa Kituo cha Ndolage.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wilaya ya Muleba ni mionganini mwa Wilaya kubwa hapa nchini yenye Majimbo mawili ya uchaguzi na ina shule nyingi za sekondari zaidi ya 67. Kila mwaka zaidi ya watoto 3,000 hawaendelei na Kidato cha Tano baada ya Kidato cha Nne. Ninaomba kupata *commitment* ya Serikali ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* chenye hadhi ya Wilaya kama ziliyvo Wilaya nyingine? (*Makof*)

Swali la pili, Serikali ina mkakati gani wa kutupatia Vyuo vya *VETA* ambavyo vinamilikiwa na Taasisi za Dini na watu binafsi kuvipatia ruzuku ya kujidoresha ili viendelee kuwasaidia na kuwaelimisha watoto wetu katika Wilaya zetu? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOGIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya msingi kwamba Serikali inafanya ujenzi wa Vyuo hivi kwa awamu. Ni muondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Muleba Kusini kwamba katika bajeti ya Serikali imetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo 36 vya *VETA* katika Wilaya mbalimbali nchini. Kwa vile tunakwenda kuweka vigezo vya namna gani tunaweza kwenda kugawa vyuo vile 36, ninampa tu taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Wilaya hii ya Muleba ina Majimbo karibu matatu na idadi ya wananchi ni kubwa na hivyo ni mionganini mwa vigezo ambavyo tutaviweka kulingana na ule uhitaji. Kwa hiyo nikuondoe wasiwasi katika mwaka ujao wa fedha kati ya vyuo vile 36 na Muleba itakuwa ni mionganini mwa hizo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo lake la pili kuhusu vyuo vya binafsi kuvipa uwezo au ruzuku ya kujidoresha, utaratibu huu haukuwepo lakini Mheshimiwa Mbunge kwa vile ametoa hapa mapendekezo, naomba tuchukue mapendekezo haya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tuende tukayafanyie tathmini ili tuweze kuangalia namna gani Serikali inaweza *cheap in* kwa sababu wanaosoma humu ni watoto wa Kitanzania. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Phillipo Mulugo swali la nyongeza.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Songwe ni mionganini mwa Wilaya zenyenye stadi za kilimo, madini, uvuvi na ufugaji na inakidhi vigezo vyote vya kupata Chuo cha VETA kwa sababu tunalo eneo kubwa na tayari eneo hilo lina Hati Miliki ya chuo cha VETA toka mwaka 2011.

Je, katika bejeti hii iliyo tengwa mwaka kesho Serikali itanipa chuo cha VETA Wilaya ya Songwe?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpungeza sana Mheshimiwa Mulugo kwa vile tayari wananchi wameshajitolea au Halmashauri au Wilaya eneo na mionganini mwa vigezo au vielelezo ambavyo tutavizingatia kwenye yale maeneo ambayo tayari walishatenga maeneo, yameshapimwa na yana hati. Kwa vile, Mheshimiwa Mulugo wewe kwako tayari kuna eneo limeshapimwa na lina Hati, basi katika ugawaji wa vile vyuo 36 nadhani hiki kitakuwa ni kigezo muhimu kuhakikisha kwamba wananchi wa Songwe wanaweza kupata chuo hiki.

Nikuondoe wasiwasi vilevile katika bajeti yetu mionganini mwa Mikoa ambayo haina vyuo vya VETA ni pamoja na Mkoa wa Songwe. Kwa hiyo, tunakwenda

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kujenga vilevile chuo cha kikubwa sana pale Songwe ambacho kitawea sasa kuchukua wanafunzi wote kutoka wilaya zile za Mkoa wa Songwe. Ninakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itafanya maboresho ya chuo cha *VETA* Gela kilichopo Wilaya ya Misenyi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Oliver, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu wa Serikali kufanya ukarabati pamoja na upanuzi kwenye vyuo vile vya zamani, kazi hii tulianza na vyuo vyetu vya *FDC*. Tulikuwa na vyuo vya *FDC* 54 tumefanya upanuzi pamoja na ukarabati na ununuzi wa vifaa. Hivi sasa tunakwenda kwenye vyuo hivi vya *VETA* vya zamani, ukienda pale Karagwe tayari kazi hii tulishaianza Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, sasa kwenye vyuo vingine na tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati pamoja na upanuzi kwenye vyuo mbalimbali vya *VETA* vile vya zamani. Ninakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niulize swali la nyongeza.

Kwanza naishukuru Serikali kwa kutujengea chuo cha *VETA* Wilaya ya Namtumbo, pia mmetuletea vifaa vya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufundishia umeme, kompyuta, vifaa vya kushonea na mitambo lakini hatukupata vifaa vya kufundishia ufundu selemala.

Je, Serikali inaweza kutuletea pia vifaa vya kufundishia ufundu selemala? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari iko kwenye mkakati na kwenye bajeti yetu inayokuja mwaka wa fedha 2022/2023, tumetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Tumesafanya hivyo, tulitenga mwaka huu zaidi ya bilioni 6.8 kwa ajili ya vyuo vya *FDC*, vilevile tumetenga kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwenye vyuo 25 hivi ambavyo tunakwenda kuvimalizia vilivyokuwa vinaendelea na ujenzi, vilevile kwenye vyuo vile vya zamani ambavyo vilikuwa bado havijapata vifaa tutapeleka vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo na hivi vifaa kwa ajili ya uselemala. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalo swali la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali kwa ujenzi wa chuo cha *VETA* Wilaya ya Rufiji na Wilaya ya Mafia. Kwa kuwa Serikali imetenga Bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya *VETA* kwa Wilaya 36; na kwa kuwa ndani ya Mkoa wetu wa Pwani Wilaya ya Bagamoyo na Wilaya ya Mkuranga hakuna chuo cha *VETA*.

Je, Serikali inatuambiaje kama kuna uwezekano wa kupata chuo kutoka na vyuo 36 vitakavyojengwa? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Subira Mgali, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Pwani, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mgao uliopita mionganii mwa wilaya za Mkoa wa Pwani, Wilaya ya Mafia pamoja na Rufiji vilipata vyuo hivi lakini wilaya nyingine kama Mkuranga, Kisarawe pamoja na Bagamoyo bado havijapata vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kama Wilaya hizi zitakuwa tayari zimetenga maeneo yaliyopimwa tayari yana Hati kama nilivyozungumza wakati najibu swalii la Mheshimiwa Mulugo vitapata kipaumbele. Kwa hiyo, jukumu kubwa hapa ambalo ninakupa Mheshimiwa Mbunge ni kuhakikisha mnawenza kutenga maeneo kwa haraka ili kwamba wakati tunajaribu kutenga zile fedha maeneo haya yaweze kufikiwa kirahisi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareoso swalii la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Kwa jinsi ambavyo mtiririko wa bajeti unaendelea kila mwaka na kwa kuwa kuna mahitaji makubwa ya ujenzi wa VETA, na kwa kuwa kuna baadhi ya Wilaya hapa nchini, kuna taasisi za dini zina vyuo vya ufundi. Je, Serikali sasa hamuoni upo umuhimu wa kuingia kwenye mfumo wa PPP na hizo taasisi ili wananchi wetu ambaa wanahitaji ujuzi huo waweze kwenda VETA? (Makof)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa mapendekezo au mawazo haya muhimu. Kimsingi utaratibu huu kwa hivi sasa Serikalini haupo au hatuna, kwa vile ni mapendekezo tunaomba tuchukue mawazo haya, tuende tukayafanyie kazi, tufanye tathmini ya kina, tuweze vilevile kukaa na wakuu hawa wa taasisi hizi, tuweze kuangalia namna gani tunaweza tukaendelesha vyuo hivi labda kwa mwendo ule wa *PPP*. Nakushuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana; naomba kuuliza swali. Kwa kuwa chuo cha *VETA* kilichopo Temeke ni chuo cha Kimko kwa Mkoa mzima wa Dar es Salaam na sasa vijana ni wengi sana katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam.

Je, mna mkakati gani wa kujenga vyuo vya *VETA* katika Wilaya zetu zote hasa katika Wilaya ya Temeke?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dorothy Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba Serikali inajenga vyuo hivi kwa awamu. Katika awamu zilizopita tumeshawenza kujenga katika Wilaya 77 nchini na Wilaya zilizobaki ni Wilaya 62.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka ujao tunakwenda kujenga katika Wilaya 36. Tafsiri yake ni Wilaya zitakazobaki ni *around*kama Wilaya 25 au 26 hivi. Tunaamini katika mwaka wa fedha 2023/2024 tunakwenda kumaliza katika Wilaya zote. Kwa hiyo, nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge hata kama hutakuwepo katika mgao huu wa hizi Wilaya 36 lakini tunaamini katika mwaka ujao 2023/2024 kwa vyovyyote vile Wilaya zote tutakuwa tumekamilisha ikiwemo na Wilaya ya Temeke. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itajenga chuo cha *VETA* kwa ajili ya Wilaya ya Mtwara kwa sababu kile kilichopo kilijengwa kwa ajili ya Mkoa wa Mtwara na Wilaya ya Mtwara ina Halmashauri Tatu na Majimbo Matatu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge, pale Mtwara kuna chuo cha Mkoa wa Mtwara ambacho kipo kwenye Wilaya ya Mtwara, katika chuo kile tafsiri yake ni kwamba kinahudumia Wilaya nzima ikiwemo Jimbo la Mtwara kwa maana ya Mtwara yenyewe, Manispaa pamoja na Jimbo la Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa hivi mkakati wetu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga kwanza kwenye kila Wilaya nchini, baada ya kukamilisha mchakato huu wa kujenga katika kila Wilaya sasa tunaweza

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kufikiria yale Majimbo au zile Wilaya ambazo zinakuwa na Majimbo mengi kuweza kufikia sasa yale Majimbo mengine ambayo yapo mbali na Makao Makuu ya Mkoa. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Chikota nakuomba tu nikuhakikishie kwamba tukamilishe kwanza ujenzi wa kila Wilaya ipate halafu baada ya hapo tutakwenda kwenye hizi Halmashauri au Wilaya ambazo zina Majimbo mengi. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Stella Manyanya swali la nyongeza.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, changamoto moja wapo ambayo inakabili hivi vyuo vya VETA ni upungufu mkubwa wa Walimu, kwa sababu tunategemea na vyuo vingi zaidi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa walimu kwa ajili ya vyuo hivyo na vyuo vya ufundi kwa ujumla?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Manyanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna changamoto kubwa sana ya Walimu, lakini sisi kama Serikali kama Wizara nimwondoe hofu Mheshimiwa Manyanya tayari tumeshaifanyia kazi.

Kwanza, kwenye ajira hizi ambazo zimetangazwa/ alizozitoa Mheshimiwa Rais hivi karibuni sisi Wizara ya Elimu tumepata ajira 2,035 na kati ya ajira hizi 2,035 ajira 1,000 tumesema ziwe za Walimu wa vyuo hivi vya ufundi. Kwa hiyo, tunakwenda kupunguza changamoto kwenye maeneo haya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo tunapeleka hivi vyuo vipyta kwa kuhakikisha tunaajiri hawa Walimu wapya 1,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimwondoe wasiwasi vilevile Chuo chetu cha Walimu wa Ufundu pale Morogoro tumekikarabati na tumekiongeza miundombinu kwa kuhakikisha kwamba kinaongeza udahili wa Walimu hawa, ili kuhakikisha kwamba upungufu wa Walimu kwenye vyuo hivi unapungua.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mapitio ya mitaala tunayofanya sasa hivi tunakwenda kuongeza *component* kwenye hivi vyuo vya kawaida vyta ualimu kuhakikisha kwamba tunakuwa na *component* vilevile ya ufundi, ili Walimu wale wasiwe tu wanakwenda kufundisha kwenye shule zetu, lakini vilevile waweze kwenda kufundisha kwenye vyuo vyetu hivi vya ufundi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Jimbo la Kilwa Kusini halina Chuo cha *VETA* na hakuna mpango wa Serikali kujenga Chuo cha *VETA* badala yake tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, lakini miundombinu yake ni chakavu na haitoshelezi. Tuna upungufu wa bwalo, viwanja vya michezo pamoja na maabara ya kompyuta. Nini mpango wa Serikali wa kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba pale katika Jimbo la Kilwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kusini tuna Chuo chetu cha *FDC*, tulifanya ukarabati kidogo, lakini bado kuna upungufu wa majengo haya aliyoyataja ikiwemo pamoja na bwalo. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Kassinge, katika mwaka ujao wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kuongeza miundombinu au upanuzi wa vyuo hivi kikiwemo hiki chuo chako, lakini vilevile na chuo cha pale Kisarawe ambacho sasa hivi kinaendelea na ujenzi, pamoja na kule Kigamboni kwa Mheshimiwa Dkt. wa Kigamboni kule tunakwenda kuviongezea miundombinu hii ya majengo ili kuweza kudahili wanafunzi wengi, lakini kutengeneza mazingira mazuri na salama ya watoto wetu kuweza kusoma. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 461

Ukarabati wa Vyuo Vikuu Nchini

MHE. DKT. THEA M. NTARA aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukarabati Chuo Kikuu cha Dodoma na Vyuo vingine ambavyo vilijengwa na kuonekana vina dosari?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
aliuju:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu nchini huanzishwa kwa kuzingatia taratibu na miongozo maalum inayotambulika na Sheria ya Vyuo Vikuu nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa Mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)*, Serikali itaboresha miundombinu kwa kujenga na kukarabati Taasisi 23 za Elimu ya Juu ikiwemo Vyuo Vikuu vya Umma ambapo Chuo Kikuu cha Dodoma ni miongoni mwa vyuo hivyo. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, swali la nyongeza.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri yanayoonesha angalau matumaini, nina swali moja la nyongeza.

Je, atatuhakikishia kwamba ukarabati utaendana sambamba na kuweka vifaa vya ufundishaji katika vyuo vyote ikiwemo vyuo vya kati? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza kwenye jibu la msingi kwamba, tumeposta mkopo wa zaidi ya *dollar* milioni 425, matumizi makubwa ya mkopo huu ni kuhakikisha tunakwenda kuviongezea miundombinu vyuo vyetu hivi vikuu, lakini vilevile tunakwenda kuboresha mitaala na kuanzisha mitaala mipyaa na vilevile tunakwenda kusomesha Walimu/Wahadhiri kwa ajili ya vyuo hivi.

Sambamba na hivyo tunakwenda kununua vifaa kwa ajili ya vyuo vikuu vyote vya umma nchini. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi hili eneo la vifaa nalo vilevile limezingatiwa. Kwa vile amezungumzia vilevile vyuo vya kati, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge vyuo vya kati navyo tumevitengeneza mkakati wake maalum kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwanza tuna mradi wetu wa *EASTRIP* ambao zaidi ya *Dollar* za Kimarekani milioni 75 tumeweza kusaini kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo lakini vilevile kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Kwa hiyo, sambamba na huu mradi wetu wa *HEET* ambao utashughulikia vyuo vikuu, lakini tuna miradi mingine midogo midogo ambayo itashughulikia vyuo hivi vya kati kwa kuhakikisha kunakuwa na wahadhiri wa kutosha na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwenye vyuo vyetu. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

MHE. MARYAM AZAN MWINYI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa vile Serikali ina mpango wa ukarabati wa vyuo vikuu hapa nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati vyuo vikuu vilivypo kule Zanzibar? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Maryam Mwinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivoyeleza kwenye majibu yangu ya msingi kwamba, mkopo huu wetu wa *HEET* (*Higher Education for Economic Transformation*) unakwenda kuboresha maeneo yote ya vyuo vikuu vya umma vikiwemo na vile vya Zanzibar.

Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi chuo chetu kile cha *SUZA* Zanzibar kimepata gawio katika gawio hili la mradi wetu wa *HEET* lakini taasisi yetu ile ya *Marine Science* ya Zanzibar ambayo inasimamiwa na Chuo chetu cha Dar es Salaam nayo vilevile sio tu inakwenda kuboreshwa bali inakwenda kujengwa upya. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi Zanzibar nayo tumeizingatia kwenye mgao huu na tutahakikisha kwamba kazi hii inakwenda kufanyika kwa haraka.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Chuo Kikuu cha Muhimbili majengo yake ni chakavu eneo ni dogo wanafunzi ni wengi kila mwaka. Je, Serikali inatoa kauli gani kuitanua Chuo Kikuu cha Madaktari Muhimbili ili kiweze kukidhi haja ya kututolea madaktari wengi nchini? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Nahato, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwanza tukiri kwamba Chuo chetu cha Muhimbili eneo lake limebana sana, lakini sisi Serikali tayari tumeshalionna hilo na kwa kutambua hilo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika mradi wetu huu wa *HEET* tunakwenda kufanya mageuzi makubwa sana katika Chuo chetu hiki cha Muhimbili kwa kujenga *campus* au chuo kingine kipyaa kabisa katika eneo letu la Mloganzila ambalo litakuwa na fani au ndaki tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo haikutosha, tunakwenda tena kufungua *campus* nyingine mpya katika Mkoa wa Kigoma ambayo itasimamiwa na Muhimbili. Hiyo vilevile haitoshi, tena tunakwenda kufanya hivyo katika Mkoa wa Mbeya kwa kujenga *campus* nyngine hii ya Muhimbili. Kwa hiyo, mchakato huu umeshaanza, nimwondoe wasiwasi tutadahili pale wanafunzi wa kutosha kuhakikisha kwamba tunapata wataalam wa tiba hapa hapa nchini. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Bakar Bakar, swali la nyongeza.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, elimu ya juu ni sekta ya Muungano na kwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Mwinyi ameitangaza Pemba kwamba ni eneo maalum la uwekezaji. Je, ni upi mpango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuititia Wizara hii wa kuwekeza kwenye sekta hii ya elimu kwa kujenga Chuo Kikuu Pemba? Ahsante. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Bakar Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara hii ni Wizara ya Muungano hasa hasa kwenye masuala ya elimu ya juu, lakini kama nilivyokwishaeleza katika maswali yaliyopita, katika mradi wetu wa *HEET* tunakwenda kufanya ujenzi mkubwa katika eneo lile la Zanzibar kwa upande wa Chuo chetu kile cha *Marine Institute* ambapo nacho vilevile kitatengeneza *branch* baadaye katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwondoe wasiwasi kwa kadri muda utakavyokwenda, tutaifiki Pemba. Hivi sasa mkakati uliopo vilevile chuo chetu cha masafa marefu, hiki Chuo Kikuu Huria tayari kina *branch* pale Pemba na katika mgao huu kimenufaika na maeneo ambayo yanakwenda kuboreshwa ni pamoja na tawi letu lile la Chuo Kikuu Huria pale katika Kisiwa cha Pemba ambacho nacho vilevile ni chuo kikuu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 462

Sekta ya Kilimo kuwa na Mchango Mkubwa kwenye Uchumi wa Taifa

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sekta ya Kilimo inakuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu Swalii la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kujenga msingi imara wa muda mrefu wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Mpango huo, utaweka msingi wa kukabiliana na athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo m dororo wa uchumi ili kulinda sekta hiyo na pia kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Ili kufikia dhamira hiyo, Serikali imelenga kujitosheleza katika chakula, kuongeza thamani ya mauzo ya mazao, kuongeza idadi ya mashamba makubwa, kuongeza eneo la umwagiliaji, kujihakikishia upatikanaji wa malighafi, kuimarisha utafiti, kuongeza uzalishaji wa mbegu bora, kuongeza mitaji, kuongeza mauzo ya mazao ya bustani na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka Shilingi Bilioni 298 ya mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi Bilioni 954 kwa mwaka 2022/2023 kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ajili ya kuanza utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya kufikia lengo kuu la ukuaji wa sekta wa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tutakubaliana kwamba ili kilimo kivutie ni pale ambapo kinakuwa na tija kwa maana ya *productivity*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba uzalishaji kwa kila hekari inaongezeka ili tulingane na nchi zingine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa kilimo kinahitaji mtaji na ni ukweli usiopingika kwamba benki yetu ya kilimo haina uwezo kimtaji na kimuundo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba benki hii inawezeshwa ili iweze kuwafikia wananchi wengi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kati ya changamoto kubwa ambayo inawakabili wakulima wa Tanzania ni kulima kwa tija. Serikali katika kutatua changamoto hii hivi sasa inaendelea kuwawezesha Maafisa Ugani kuhakikisha wanawafikia wakulima na kuwapa elimu bora na kanuni bora za kilimo ili wakulima wetu waweze kulima kwa tija sambamba na upatikanaji wa mbegu bora na pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili pia *TARI* wameendelea kufanya tafiti mbalimbali kuhakikisha wakulima wetu wanapata elimu bora ili waweze kulima kwa

tija na tunayo mifano ambayo imetokea katika Mkoa wa Mwanza, Simiyu na Geita kwenye kilimo cha pamba ambapo kanuni ile ya 9060 imesaidia sana kuongeza tija katika uzalishaji wa pamba.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la kuhusiana na mitaji, ni dhahiri kwamba kilimo hakiwezi kuendelea pasipo kuwepo na mitaji katika kusaidia kuchochaea sekta hii. Yalitoka maelekezo kupitia benki yetu kuu ya kuhakikisha taasisi zote za kifedha ambazo zinatoa mikopo zififikhe riba ya *digit* moja kwa maana ya tarakimu moja ili wakulima wetu waweze kukopesheka kirahisi. Zoezi hilo limefanyika katika baadhi ya mabenki na mkakati unaendelea kuhakikisha kwamba na benki nyingine zote zinafikia katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuiwezesha *TADB* ni dhahiri kwamba Wabunge wote wameshuhudia kazi ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba benki hii inapata mtaji wa kutosha na benki hii ilisaini makubaliano na benki kutoka Ufaransa kwa ajili ya kuongeza mtaji. Vilevile, tunaweka nguvu kubwa kuhakikisha kwamba *TADB* inasimama kwa dhati ili iweze kuwasimamia wakulima wengi ambao wanashindwa kukidhi masharti katika taasisi za kifedha za kibiasahara ili wao wabaki kama *guarantor* na wakulima waweze kukopesheka. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naipongeza Serikali kuiongezea Wizara ya Kilimo bajeti yake kwa asilimia 300. Kwa kuwa vijana wa Tanzania sasa wako wengi wenye nguvu lakini hawana namna ya kuwekeza kwenye taasisi kama hiyo sekta ya kilimo; na kwa kuwa kwenye jibu la msingi, Waziri ametueleza kwamba wako tayari sasa kuona kwamba tunajitosheleza kwa chakula. Je, Serikali inawatumiaje vijana hao wengi kwa kuwawezesha katika sekta hii ya kilimo kwa kuwapa mashamba kulima kwenye hizo *block farming* na kuwawezesha miundombinu yote ili tuzuie fujo zilizo mitaani? (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *Intergated Labour Force Survey* inasema nchi yetu ina takribani ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi milioni 22.3 ambaao asilimia kubwa ni vijana. Sisi kama Wizara ya Kilimo tumeona kundi hili kubwa tukilitumia vizuri lina uwezo wa kukuza uchumi wa nchi yetu na kuikuza sekta ya kilimo. Kufuatia hayo Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa bajeti yake kuanzia mwezi Julai tunakuja na utekelezaji wa *program* maalum ambayo itawahusisha vijana nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, *program* hii itakuwa ni kuwapatia vijana maeneo kwa maana ya mashamba makubwa ya kilimo kuwasaidia kupata mitaji, kuwasaidia pembejeo na kuwatafutia pia masoko na kwa kuanzia tumepata eneo la hekari 20,000 katika Wilaya za Chamwino na Bahi na mradi huu utaanza mwezi Julai, kama sehemu ya majoribio na baadaye utakwenda nchi nzima ili kuwafikia vijana wengi zaidi. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Venant Daud Protas, swalii la nyongeza.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilitekeleza agizo la Serikali la kuengeneza *block farming*, ikaandaa hekari 15,000 katika kijiji cha Kalangazi na aliyekuwa Naibu Waziri na sasa ni Waziri wa Kilimo alituahidi ataleta shilingi bilioni tano na trekta.

Je, ni lini Serikali itatekeleza *block farming* ya Kalangazi ili ianze kuleta tija kwa uchumi wa nchi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant Protas, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu wakati tumeisoma hapa Bungeni tulisema, moja kati ya malengo yetu makubwa ni kufikisha mashamba makubwa 10,000 ifikapo mwaka 2030. Kwa hiyo, popote panapotokea fursa ya uanzishwaji wa mashamba makubwa sisi tupo tayari kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya namna hiyo. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge jambo hili alishalisema baada ya Bunge la Bajeti, mimi na yeye tutaongozana kwenda Uyui kuangalia eneo hilo na baadaye tutashirikiana na wataalam kwa ajili ya utekelezaji.

SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niwashukuru Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanazofanya. Wakulima wa pamba maeneo wanakolima pamba hasa katika Jimbo la Ushetu wamekuwa na changamoto kubwa sana ya maghala ya kuhifadhiya pamba na madhara yake pamba hii inachafuka sana na kuhatarisha soko letu la ndani na la nje. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea maghala ya kudumu wakulima wa pamba hapa nchini, hasa katika Jimbo la Ushetu ili waweze kuhifadhi pamba yao ili kulinda soko letu la ndani? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mikakati tuliyonayo ni kuhakikisha tunapunguza *post harvest loss* kutoka asilimia 35 ilivyo hivi sasa kurudi tarakimu moja. Mkakati uliopo ni ujenzi wa maghala ya kutosha, ndio maana kwenye bajeti yetu tulioisoma hapa Bungeni, bajeti ya ujenzi wa maghala

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

imetoka Shilingi Bilioni mbili mpaka Shilingi Bilioni 25 lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na ujenzi wa maghala mengi zaidi. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tunaangalia maeneo hayo yote hasa ya uzalishaji ili tuweze kuwa na maghala ya kutosha na tuweze kuhifadhi mazao yetu ya kilimo katika mfumo mzuri.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 463

Faida na Hasara za Nchi Kuwa Uchumi wa Katil

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU aliuliza:-

Je, hasara na faida gani Taifa linapata kuwa uchumi wa katil na asilimia ngapi ya wananchi wanafahamu na kuishi uchumi wa katil?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania kuingia kwenye kundi la nchi za uchumi wa pato la katil la chini kunaambatana na fursa pamoja na changamoto mbalimbali. Fursa hizo ni pamoja na kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa fedha za mikopo ya kibiashara kwa ajili ya miradi ya maendeleo, uhuru wa kupanga matumizi ya fedha za mikopo ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kibiashara, kuchochea uwekezaji kutokana na ukuaji wa wastani wa pato la mtu na mtu, na kuzidi kuaminika katika taasisi za kifedha za Kimataifa kutokana na kutengamaa kwa viashiria vya uchumi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni pamoja na kupungua kwa upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu, kuongezeka kwa kiwango cha michango kwa taasisi na mashirika mbalimbali ya Kimataifa. Ni matumaini ya Serikali kupitia juhudii ya vyombo vya habari kuwa wananchi walio wengi wanafahamu kuhusu nchi kuingia katika uchumi wa kati wa chini. Hali hiyo imejidhihirisha kwa kuona mabadiliko chanya kwa mwananchi mmoja mmoja na ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE SJ. KANYASU: Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Tanzania ilipoingia kwenye uchumi wa kati wa chini, baadaye liliuja tatizo la *Corona* na sasa hivi tuna-experience mgogoro wa kivita wa Ukraine; dunia inatabiriwa kuwa na mgogoro mwingine wa kiuchumi; Tanzania itaathirika vipi iwapo mgogoro huo utatokea? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, katika jibu lake la swali langu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema moja ya sifa ya nchi inapoingia kwenye uchumi wa kati ni kuwa na sifa ya kukopeshwa mikopo ya kibiashara. Hata hivyo zimekuwepo lawama baada ya Tanzania kukopa kibiashara.

Ni nini mtazamo wa Wizara iwapo tutaendelea kukopa kibiashara wakati wengine wanaona pamoja na sifa hiyo tunayo, tusikope kibiashara? (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie Mbunge kwamba, nchi yetu bado hajashuka katika uchumi wa kati chini, bado tuko pale pale. Pamoja na changamoto zote hizo, kilichotokea ni kushuka kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja tukatoka 7% kuja 4.8%.

Mheshimiwa Spika, lakini swalii lake la pili, kauli ya Serikali ni kwamba wananchi waache kuwa na lawama kwa sababu Serikali yao iko makini sana katika kufanya tathmini aina gani ya mkopo nchi yetu iingie, na una tija gani kwa maslahi ya Taifa letu? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na sahihi. Napenda niongezee tu kipengele kimoja; ameshaongelea upande wa Serikali, lakini faida nyingine ambayo inapatikana kutokana na nchi yetu kuwa katika ngazi hiyo, ni pamoja na kwamba taasisi nyingine za sekta binafsi zilizoko kwenye nchi yetu na zenyewe zinanufaika kwa sababu mnajua miradi mikubwa ama kampuni kubwa zinaendesha biashara zao kwa mikopo. Kwa hiyo, nchi inapofika hatua hiyo, tunafanya *credit rating*. Ile *credit rating* haiisaidii Serikali peke yake kukopa, bali inasaidia pia kampuni zilizoko kwenye nchi husika kuweza kuaminika na kuweza kupata hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nchi inapopata hiyo *credit rating*, haiisaidii tu Serikali kukopa, bali inasaidia

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pia wakandarasi wa nchi husika ama kampuni ya nchi husika kuweza kuaminika kupata mikopo katika soko lile la mitaji ambapo na Serikali pia inaweza ikanufaika na mitaji hiyo ambayo iko kwenye soko la mitaji duniani. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo ya wageni tulionao Bungeni siku ya leo. Kabla sijasema kuhusu wageni, upande wa Serikali, kwa sababu majibu ni mawasiliano rasmi, nawaomba sana kwa sababu sisi ndio wazazi wa Kiswahili, basi tutumie Kiswahili fasaha na pia tusichanganye na Kiingereza pale ambapo hakuna sababu. Yaani tumia Kiswahili kwa sababu wale wanaotumia Kiingereza huko kwenye nchi zao hatuoni wakichanganya na Kiswahili. (*Makof!*)

Kwa hiyo, kwa sababu haya ni mawasiliano rasmi, tutumie Kiswahili. Kama hakuna neno, litafute, lakini tusihalalishe, yaani kama vile lugha ya mazungumzo ambavyo huwa tunachanganya lugha halafu tunavumiliana humu ndani, sasa naona na majibu yameanza kuja kwa kuchanganya lugha, yaani kama ni sehemu ya sentensi kuweka neno la Kiingereza. Siyo sawa sawa. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo humu ndani siku ya leo, tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Spika. Kwanza ni wageni tisa ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar; yupo Mheshimiwa Abdallah Kombo ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, karibu sana. (*Makof!*)

Yupo pia Mheshimiwa Fatma Mohammed ambaye ni Mjumbe, karibu sana; Yupo Mheshimiwa Issa Gava ambaye ni Mjumbe, karibu sana. Jamani, huyu sio Issa Gava, naona hawa waandishi; ni Issa Gavu, tafadhalii usimame tena, ahsante sana. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Haya, Mheshimiwa Miraji Mussa, Mjumbe, karibu sana; yupo pia Mheshimiwa Prof. Omar Hamad, Mjumbe, Karibu sana; yupo pia, ndugu Abas Mohammed ambaye, ni Katibu, Ndugu Asha Mohamed, Katibu. Ndugu Husna Othman, Katibu na Ndugu Shaib Fadhili Shaib, Katibu. Karibuni sana Bungeni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kutoka Baraza la Wawakilishi. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni watano wa Bunge ambaao ni viongozi wa Wizara ya Maji Bara, na Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar. Tutaanza na Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara ambaye ni Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, karibu sana Mheshimiwa Waziri; tunaye pia Dkt. Mngereza Mzee Miraji ambaye, ni Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Dkt. Salha Mohamed Kassim ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar, karibu sana; tunaye pia Prosper Buchafwe ambaye, ni Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Mipango Wizara ya Maji, huyu ni wa Bara sasa, lakini pia yupo Maryam Issa Juma ambaye ni Mkurugenzi wa Mipango Sera, Utafiti Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Zanzibar, karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wa Bunge ambaao ni mtoto Baraka Self Mpanda mwenye umri wa miaka nane ambaye ni Mтанzania pekee aliyeanza kucheza mpira wa miguu akiwa na umri wa miaka minne. Sijui yuko wapi huyu? Sasa simama kwanza. Haya, mtoto huyu amecheza mpira katika vilabu vikibwa duniani ambavyo ni *KRC Genk* ya Ubelgiji, Valencia na Barcelona za Hispania pamoja na Ajax ya Uhlanzi.

Vilevile amepata kuwa mchezaji bora wa mwaka 2021 na amepata fursa ya kucheza timu ya wanafunzi na kusoma nchini Uhlanzi mwaka 2022. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ni mgeni wetu huyo, lakini mgeni wetu huyu ameambatana na familia yake pamoja na kocha wake ambaye ni Ndugu Martin Hamel. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Karibuni sana wazazi wa kijana huyu na ndugu zake wote, wote msimame kwa pamoja, karibuni sana. Karibuni sana tunawashukuru kwa malezi na tunawatakia kila la heri. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, alikuwa anakusudia kuwapungia, hakuwa anakusudia kwamba, mwache kupiga makofi, alikuwa anawapungia mkono. Ahsante sana. Mnaweza sasa kuketi. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambaao ni Umoja wa Mashina ya Wakereketwa wa CCM kutoka Uyole, Jijini Mbeya, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Bakari Mkwizu, wote msimame kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu.

Pia tunao walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi Nsongwi kutoka Mbeya Vijijiini, karibuni sana wanafunzi na walimu wetu kutoka Mbeya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia Wanachama wa Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA) wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wao, Ndugu Kenneth Chimoti, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Bunge ambaao ni mtandao wa watafsiri (*Translation Network International*) unaojihuisha na kutafsiri Injili katika lugha mbalimbali za Tanzania wakiongozwa na Mary Emmanuel Nnko. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambaao nao wamealikwa na wako hapa Bungeni. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wote msimame kwa pamoja. Karibuni sana wageni wetu, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Tunao wageni walotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 41 na walimu watano wa Shule ya Awali na Msingi, *Bensa/kutoka Mkoani Morogoro* wakiongozwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwalimu Jofrey Bulkati, karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi. Pia tunao wanafunzi 30 na walimu nane kutoka Shule ya Awali na Msingi, *Destiny* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 60 na walimu 10 wa Shule ya Msingi *NICOSTA* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili hapa. Tangazo la kwanza linahusu matokeo ya mechili zilizofanyika kwenye Bonanza siku ya Jumamosi, tarehe 25 Juni, 2022.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena; nikiwa nimesimama, hamruhusiwi kuzungumza! Waheshimiwa Wabunge, nikiwa nimesimama, hamruhusiwi kuzungumza, illi mnisikilize.

Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya mechili zilizofanyika kwenye Bonanza siku ya Jumamosi, tarehe 25 Juni, 2022 kati ya *Bunge Sports Club* na Benki ya *CRDB* ni kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu mchezo uliamuliwa kwa *penalty* ambapo Bunge ilishinda kwa *penalty* 6 kwa 5 dhidi ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, matokeo haya pia yanapokelewa na wageni wetu kutoka Baraza la Wawakilishi kwamba, Bunge liliongoza.

Kwa hiyo, hongereni sana *Bunge Sports Club* kwa upande wa mpira wa miguu. Pia mpira wa kikapu wanaume Bunge walishinda kwa 35 kwa 33 dhidi ya *CRDB*. Hongereni sana mpira wa kikapu. (*Makofi*)

Pia, mchezo wa kuvuta kamba wanaume na wanawake, Bunge walishinda mivuto yote dhidi ya *CRDB*. Vilevile riadha mita 100, mshindi alikuwa Spika kwa hiyo, ahsanteni sana. Kwa hiyo, nilipewa zawadi pia kwa niaba yenu. (*Kicheko/Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, kuna mpira wa pete, Bunge tulishinda magoli 25 kwa 10 dhidi ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, kwa ujumla michezo yote iliochezwa siku ya Jumamosi, *Bunge Sports Club* iliibuka mshindi kama Yanga. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia kwamba mnaalikwa kutembelea banda la Taasisi ya *Tanzania Network International* katika Viwanja vya Bunge ambao wapo kwa ajili ya kufanya maonesho ya vitabu vya dini kwa lugha mbalimbali za asili nchini Tanzania. Maonesho haya yatafanyika kwa siku mbili, yaani kuanzia leo tarehe 27 na tarehe 28 Juni, 2022 na vitabu hivyo vitatolewa bure kwa wale watakaotembelea mabanda hayo. Mnakaribishwa sana kutembelea mabanda hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022
(The Finance Bill, 2022)

(Kusomwa Mara ya Pili)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu unasomwa kwa mara ya pili. Kwa hiyo, sasa nitoe fursa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba, aje atoe maelezo kuhusu Muswada huu.

WAZIRI FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwaka 2022 (*The Finance Act, 2022*) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri mbalimbali ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali hususan Kamati ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wakati wakichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliyopitishwa Bungeni tarehe 24 Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waandishi wa Sheria, wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Vilevile, naomba kutoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wataalam wake kwa mashauriano tuliyofanya ili kuhakikisha kwamba Sheria tunazozitekeleza baina ya pande mbili za Muungano ziko katika utekelezaji uliozingatia maoni yote.

Mheshimiwa Spika, lengo la Muswada huu ni kutekeleza kisheria, hatua za mapato zinazohusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 14 Juni mwaka huu. Muswada huu unafanyia marekebisho ya sheria thelathini na Tano zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada pamoja na tozo. Lengo la kurekebisha Sheria hizi ni kuweka mfumo wa kodi ambao ni tulivu na unaotabirika na kuboresha taratibu za ulipaji na ukusanyaji kodi pamoja na kuweka na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uwekezaji yanayo kuchocha kasi ya ukuaji wa uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kufuatia marekebisho yaliyofanyika kupitia Jedwali la Marekebisho, Sheria zinazofanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

- i) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156,
- ii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197,
- iii) Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213,
- iv) Sheria ya Korosho, Sura ya 203,
- v) Sheria ya Usajili wa Makampuni, Sura ya 212,
- vi) Sheria ya Hakimiliki, Sura ya 218,
- vii) Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262,
- viii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147,
- ix) Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306,
- x) Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414,
- xi) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196,
- xii) Sheria ya Mbolea, Sura ya 378,
- xiii) Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura ya 84,
- xiv) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41,
- xv) Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada, Sura ya 134,
- xvi) Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi, Sura ya 120,
- xvii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332,
- xviii) Sheria ya Bima, Sura ya 394,
- xix) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113,
- xx) Sheria ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Nchi Kavu, Sura ya 413,
- xxi) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290,
- xxii) Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 287,
- xxiii) Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 288,
- xxiv) Sheria ya Madini, Sura ya 123,
- xxv) Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura ya 437,
- xxvi) Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297,
- xxvii) Sheria ya Bandari, Sura ya 166,
- xxviii) Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38,
- xxix) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- xxx) Sheria ya Wakala wa Meli, Sura ya 415,
- xxxi) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438,
- xxxii) Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408,
- xxxiii) Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318,
- xxxiv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, na
- xxxv) Sheria ya Mafunzo na Ufundu Stadi, Sura ya 82,

Mheshimiwa Spika, kufuatia majadiliano na wadau mbalimbali hususan michango ya Wabunge katika kujadili bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 na maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti, Serikali imefanya marekebisho mbalimbali ya hatua za mapato zilizowasilishwa kuitia hotuba ya bajeti ikiwemo yafuatayo:-

(i) Kupunguza kiwango cha kodi ya zawadi ya ushindi *Gaming Tax on Winnings* kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10 kwenye michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (*Sports betting*). Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali kutokana na watu wengi zaidi kuhamasika kushiriki kwenye michezo ya kubahatisha ya kubashiri matokeo ya michezo. Uchambuzi uliofanyika umebainisha kwamba endapo Serikali itaendelea na kupunguza kiwango husika hadi kufikia asilimia 10, ambapo mapato ya Serikali yataongezeka kutoka shilingi bilioni 4.2 hadi kiasi cha shilingi bilioni 5.2 kutokana na watu wengi zaidi kushiriki katika michezo hiyo.

(ii) Kutofanya marekebisho ya kubadili mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuhudumia miundombinu ya masoko ya machinga. Serikali itatumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali katika bajeti ya mwaka 2022/2023 yaani bilioni 1 kwa kila Mkoa kwa Halmashauri za Majiji na Manispaa zitumike kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya masoko ya machinga.

(iii) Kuondoa pendekemo la kutoza Kodi ya Zuo kwa kiwango cha asilimia mbili (2) kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (Small Scale Miners). Utozaji wa kodi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

husika utasababisha utoroshaji wa madini na kupunguza kasi ya wachimbaji kuuza madini husika katika masoko ya madini au vituo vya uchenjuaji.

(iv) Kuondoa hatua ya kutoza kodi ya awali ya mapato ya shilingi 20 kwa lita kwa wafanyabiashara wa rejareja wa mafuta ya petroli nchini ambayo ingekusanywa na waingizaji wa mafuta hayo kwa ujumla kwa kulipwa Serikalini. Hatua hii inatokana na kutotabirika kwa bei za mafuta ambazo zilionekana kuanza kushuka mwezi Mei, 2022 lakini bei hizo sasa zinaonekana kupanda.

(v) Kufanya maboresho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini sambamba na kusamehe kodi hiyo kwenye malighafi ya *soda-ash or calcium carbonate* na vifungashio vinavyotumika katika uzalishaji. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyopanda kutockana na m dororo wa uchumi na kulinda misingi ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inayoelekeza bidhaa zinazouzwa ndani ya nchi zisamehewe kodi hiyo yaani *exempted* badala ya kutozwu kodi ya asilimia sifuri.

(vi) Serikali imefanya uamuji wa kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania yaani *TASAC* ili taasisi hiyo isijihushe na jukumu la uwakala wa forodha badala yake ibaki na jukumu la kusimamia udhibiti wa watoa huduma za usafiri majini. Hata hivyo, taasisi hii itaendelea na shughuli za uwakala wa forodha kwenye bidhaa za makinikia, silaha pamoja na vilipuzi, nyara za Serikali na wanyama hai wanaotambulika kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori. Hatua hii itaondoa mgongano wa kimaslahi unaotokana na *TASAC* kuwa mtoa huduma za uwakala wa forodha na mdhibiti wa watoa huduma za usafiri majini kwa wakati mmoja.

(vii) Lingine ni kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili kuweka utaratibu kwa Waziri mwenye

dhamana ya masuala ya Fedha baada ya kufanya mashauriano na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Ardhi mamlaka ya kusamehe riba ya malimbikizo ya pango la ardhi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kuongeza mapato ya serikali kwa kukusanya malimbikizo ya kodi husika.

(viii) Lengo linguine ni kuongeza wigo wa kusamehe tozo ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wahitimu wa elimu ya juu na vyuo vya kati badala ya vyuo vikuu pekee kama nilivyopendekeza wakati wa awali kwenye Hotuba ya Bajeti. Lengo la hatua hii ni kuongeza idadi ya wanufaika wa mafunzo ya vitendo ya kuwapatia ujuzi na uzoefu wa kazi kabla ya ajira kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania.

(ix) Jambo lingine ni kuusogeza muda wa kufutwa kwa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za kukodi ndege yaani *air charter service* kwa kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 ili kutoa fursa ya utekelezaji wa miadi iliyowekwa kwa kuzingatia uwepo wa msamaha huo.

Mheshimiwa Spika, Aidha, ili kuboresha taratibu za usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya mapato, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kufuatia mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tumefanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato na Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kuwezesha yafuatayo: -

(i) Kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweka viwango mfuto vya kodi kwa walipa kodi binafsi wadogo wadogo yaani (*presumptive rates*) vitakavyotumika Tanzania Zanzibar.

(ii) Kutoa nafuu ya kodi ya mapato kwa kuwezesha kampuni zinazofanya biashara pande mbili za Muungano kupata nafuu ya kodi inayolingana na kodi iliyolipwa upande wowote wa Muungano ili kuepusha utozaji kodi mara mbili, Katika kutekeleza hatua hii, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 inatambua namba ya utambulisho ya mlipakodi aliyesajiliwa Tanzania Zanzibar ili kurahisisha taratibu za ukusanyaji kodi kwa kampuni zenyenye ofisi pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, pamoja na marekebisho hayo ya Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato ya Tanzania Zanzibar zitasaini Hati ya Makubaliano ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu Thelathini na Sita kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2022.

Sehemu ya Pili, Nane, Kumi na Moja, Kumi na Tatu, Ishirini na moja, pamoja na Thelathini na Mbili kama zillivvorekebishiwa, zinapendekaze kurekebisha Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156, Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262, Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, Sheria ya Mbolea, Sura ya 378, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu, Sura ya 413.

Vilevile Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415, ili kuondoa mwingiliano wa sheria mbalimbali za taasisi za udhibiti, hususan kwa kurejesha suala la usimamizi wa viwango kusimamiwa na Shirika la Viwango Tanzania badala ya utaratibu wa sasa ambapo kila Taasisi ya udhibiti ina mamlaka ya kusimamia masuala ya viwango kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Spika, Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha shughuli za udhibiti wa viwango zinafanywa na Taasisi moja ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Hata hivyo, kupitia Jedwali la marekebisho ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Sura ya 172, yameondolewa kwenye Muswada huu kutokana na unyeti wa shughuli za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 kwenye vifungu vya 35(2) na 36(1) ili kuongeza kiwango cha ukomo wa Serikali kukopa kutoka Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuiongoza Serikali kutekeleza Bajeti zake kwa ufanisi hususan kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213, ili kuongeza tafsiri ya neno *beneficial owner* ili kuwianisha tafsiri hiyo na ile iliyotolewa katika Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423. Kuweka sharti la kuwasilisha taarifa za wamiliki wanufaika wakati wa usajili wa biashara zinazoendeshwa kwa ubia, kubainisha watu au taasisi ambazo zinaweza kupata taarifa za mmiliki mnufaika na kuweka faini kwa kushindwa kutoa taarifa zinazohusiana na wamiliki au wanufaika wa ubia. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na upatikanaji wa taarifa za wamiliki wanufaika zinazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 17A cha Sheria ya Korosho, Sura ya 18 ili kuainisha mgawanyo wa mapato yatokanayo na korosho, ambapo asilimia 50 itaenda Mfuko Mkuu wa Hazina na asilimia 50 itagawanywa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo na ruzuku za pembejeo za kilimo. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ruzuku, pembejeo pamoja na maendeleo ya kilimo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 kama ifuatavyo:-

(i) Kama ilivyofanyika kwenye marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213, kuongeza tafsiri ya neno *beneficial owner* ili kuwianisha tafsiri hiyo na ile iliyotolewa katika Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423.

(ii) Kuweka adhabu kwa kampuni ambazo yatashindwa kutunza rejestya ya wanachama na wamiliki wanufaika au kutoa taarifa ya mabadiliko kwenye rejestya, kushindwa kuweka tafsiri ya fahirisi ya majina ya wanachama na wamiliki wanufaika wa kampuni na kushindwa kuwasilisha *return* ya kila mwaka ya kampuni.

(iii) Kuweka adhabu kwa kampuni ambazo yatashindwa kutunza rejestya ya wanachama na wamiliki wanufaika au kutoa taarifa ya mabadiliko kwenye rejestya, na kushindwa kuweka fahirisi ya majina ya wanachama na wamiliki wanufaika wa kampuni.

(iv) Kuweka wajibu kwa wafilisi wa makampuni kutunza kumbukumbu za hesabu na nyaraka zinazohusiana na ufilisi wa Makampuni.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya saba kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218 ili: -

(i) Kuongeza tafsiri ya maneno *collective management* na *collective management organization* ili kuwezesha ufanisi kwenye utekelezaji wa Sheria.

(ii) Sehemu ya pili ni kuondoa mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza majukumu ya Chama cha Hakimiliki Tanzania na Ofisi ya Hakimiliki.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iii) Kutenganisha majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki na majukumu ya taasisi za usimamizi jumuishi na kuainisha majukumu ya Ofisi hiyo.

(iv) Kuanzisha tozo ya asilimia 1.5 kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kurudufu na kutunza kazi za sanaa ambavyo ni *radio/tv set enabling recording, analogue audio recorders, analogue video recorders, CD/DVD copier, digital jukebox and mp3 player*; vinavyotumika kuwezesha kuzalisha, kusambaza, kurudufu na kutunza kazi za sanaa, uandishi na ubunifu mwengine.

(v) Jambo lingine ni kubainisha majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki na kuweka mfumo wa usimamizi jumuishi wa hakimiliki na kuweka wajibu kwa taasisi za usimamizi jumuishi kuwasilisha Ofisi ya Hakimiliki taarifa zao za utendaji na hesabu zillizokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji na kuimarisha usimamizi wa masuala yanayohusu hakimiliki na haki shirikishi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kuwianisha mfumo wa adhabu katika sheria za kodi ili kuhakikisha kuwa adhabu zitakazotumika dhidi ya makosa ya kikodi ni zile zilizoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438.

(ii) Kujumuisha katika Sheria ya Watoa Huduma wa Televisheni za Keslipia wanaotumia miundombinu mingine tofauti na ile ya ardhini.

(iii) Kurekebisha Jedwali la Nne ili kubainisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za sukari na betri za maji kwa lengo la kupanua wigo wa kodi na kulinda afya za walaji na mazingira. Aidha, kupitia marekebisho yaliyofanyika kwenye kupitia Jedwali la Marekebisco, bidhaa za sukari

zinazoingizwa kutoka nje ya nchi zitatozwa ushuru wa bidhaa kwa kiasi cha shilingi 1,000 na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa nchini hazitatozwa. Aidha, betri kutoka nje ya nchi zitatozwa ushuru wa asilimia 10 na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa nchini zitatozwa asilimia 5. Vilevile, Jedwali linarekebishwa ili kusamehe ushuru wa bidhaa kwenye vifungashio nya maua, matunda na mbogamboga kwa lengo la kuwapunguzia gharama wauzaji wa bidhaa hizo nje ya nchi na kuongeza ushindani wa bidhaa hizo katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika Sehemu ya Kumi kama ilivyorebishwa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 kwa kuongeza kifungu kipyaa cha 164B ili kutoza ada ya matumizi ya kisimbuzi kuanzia shilingi 500 hadi 2,000 kulingana na kiwango cha matumizi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali. Mchanganuo wa utozaji wa ada hii kulingana na matumizi utabainishwa kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura namba 196 ambapo Jedwali linarekebishwa ili kuweka tozo ya usafrishaji wa shaba chakavu na vyuma chakavu nje ya nchi. Lengo la marekebiso haya ni kulinda viwanda nya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda nya ndani nya bidhaa za shaba na chuma.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nne inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura namba 84 kwa kupunguza ada ya magari ya kigeni yanayozidi *escale* tatu yanayopita nchini kwa lengo la kuwianisha viwango vinavyotozwa hapa nchini na zile zinazotozwa katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Masharika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, pamoja na soko la pamoja la Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (*COMESA*).

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Michezo ya Kubahatisha, Sura namba 41 kama nilivyotoka kuisoma hapo awali nilipokuwa ninaanza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura namba 134 ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa deni la taifa kwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kuboresha utaratibu wa ukokotoaji wa uhimilivu wa deni kwa kutumia uchambuzi wa madeni unaotumia kipimo zaidi ya kimoja.

(ii) Kumwezesha Kamishna wa Usimamizi wa Madeni kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wataalam na kuboresha uwakilishi wa wajumbe katika Kamati ya Wataalamu.

(iii) Kuipa jukumu Idara ya Usimamizi wa Madeni na kufanya kazi ya uchambuzi na uandaaji wa nyaraka zinazowasilishwa kwenye Kamati za Madeni.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi, Sura ya 120 ili kuondoa ngozi au bidhaa za ngozi za wanyamapori katika wigo wa Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano wa sheria na mwingiliano wa majukumu kati ya vyombo vinavyosimamia ngozi na bidhaa za ngozi za wanyama wa majumbani na vile vinavyosimamia ngozi na bidhaa za ngozi za wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane kama ilivyorekebisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 kama ifuatavyo: -

(i) Kuongeza tafsiri ya maneno *digital market place, electronic services* ili kuwezesha utozaji kodi kwenye huduma za kidigitali.

(ii) Kuongeza tafsiri ya maneno *alternative financing arrangement* na kurekebisha kifungu cha 32 ili kuwianisha

maana ya riba inayotolewa kwa mikopo ya kawaida ya kibenki kuwa sawa na faida kwa mikopo ya mbadala.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane kama ilivyorekebisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 kama ifuatavyo:-

(iii) Kuongeza tafsiri ya maneno "*digital market place*," "*electronic services*" ili kuwezesha utozaji kodi kwenye huduma za kidigitali;

(iv) Kuongeza tafsiri ya maneno "*alternative financing arrangement*" na kurekebisha Kifungu cha 32 ili kuwianisha maana ya riba inayotolewa kwa mikopo ya kawaida ya kibenki kuwa sawa na faida kwa mikopo ya mbadala;

(v) Kuweka utaratibu maalum wa kulipa kodi kwa wamiliki wa mabasi na malori kwa viwango maalum kulingana na ukubwa wa gari;

(vi) Kuondoa kwenye wigo wa kutozwa kodi, faida ambayo haijagawanywa na taasisi za fedha za ndani ya nchi zilizo na matawi nje ya nchi kwa misingi wa taratibu zilizowekwa na Benki Kuu ya Tanzania;

(vii) Kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri maalum baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya Sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji kuhusu utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi;

(viii) Kujumuisha uendeshaji na usimamizi wa biashara unaofanyaika kwa njia za kielektroniki;

(ix) Kuongeza malipo ya utumiaji wa rasilimali pamoja na huduma za kidigitali zinazotolewa na watoa huduma wasio wakaazi hapa nchini kwa lengo la kupanua wigo wa kodi;

(x) Kuwezesha wapangaji binafsi kuzuia kodi ya mapato kwenye malipo ya pango ya nyumba za biashara na makazi. Pia Sheria itarekebishwa ili kuondoa sharti la kukata kodi ya zuio kwenye malipo ya riba ya hati fungani za makampuni na Manispaa zinazosajiliwa kwenye Soko la Hisa na Mitaji la Dar es salaam. Lengo la marekebisho haya ni kuleta ufanisi wa ukusanyaji wa kodi ya pango na kuongeza vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo;

(xi) Kutoza kodi ya mapato ya asilimia Mbili kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wasio wakaazi kwa lengo la kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya Serikali;

(xii) Kuwaondolea wajibu wa kuwasilisha *return* za kodi ya mapato walipakodi wa kidijitali wasio wakaazi;

(xiii) Kumwezesha Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweka viwango mfuto vya kodi kwa walipa kodi binafsi wadogo vitakavyotumika Tanzania Zanzibar;

(xiv) Kutoa nafuu ya kodi ya mapato kwa kuwezesha kampuni zinazofanya biashara pande mbili za Muungano, kupata nafuu ya kodi inayolingana na kodi iliyolipwa upande wowote wa Muungano ili kuepusha utozaji kodi mara mbili. Katika kutekeleza hatua hii, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 itatambua namba ya utambulisho ya mlipakodi aliyesajiliwa Tanzania Zanzibar ili kurahisisha taratibu za ukusanyaji kodi kwa kampuni zenye ofisi pande mbili za Muungano;

(xv) Kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kurekebisha kiwango cha kodi kwenye daraja la juu la mauzo kwa walipakodi binafsi wadogo ili kuongeza uwazi wa kurahisisha ukadiriaji na ulipaji wa kodi. Aidha, Jedwali la Kwanza linarekebishwa kwa kupunguza kiwango cha kodi ya zuio kwa

malipo ya bidhaa ya filamu kwa watoa huduma wa nje na ndani ya nchi kwa lengo la kuongeza ajira, kukuza tasnia ya filamu na kuchochea uhaulishaji wa uuzaaji; na

(xvi) Kurekebisha Jedwali la Pili ili kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwenye uhamishaji wa haki na taarifa za uchimbaji madini kwenda kampuni za ubia, uhamishaji wa hisa kwenda Serikalini na kwenye hisa ambazo Serikali imepata kupitia Msajili wa Hazina. Lengo la marekebiso haya ni kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuhakikisha kuwa uhamishaji wa haki na taarifa za madini unafanyika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama nilivyoeleza awali, kupitia Jedwali la Marekebiso, Serikali imeondoa pendekezo la kutoza kodi ya zio kwa wachimbaji wadogo wa madini na kuondoa sharti kwa waagizaji wa nishati ya mafuta kwa jumla kuwa mawakala wa ukusanyaji kodi wa Serikali kutoka kwa wauzaji wa reja reja wa nishati ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, ninasisitiza hapo hapo kwamba, lengo letu tuliloweka kwenye hotuba la kuweka sharti la *TIN number* kuwianishwa na Kitambulisho cha Taifa siyo kwa lengo la kila kijana mwenye miaka 18 kuwa na sharti la kulipa kodi, suala la kulipa kodi litaendelea kuwa jambo la kipato na siyo jambo la umri kama kawaida, hili ni lengo la kuwarahisishia vijana kupunguza vitambulisho pale wanapotafuta masuala yanayohusisha masuala ya vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Bima, Sura ya 394 kwa kuongeza Kifungu kipyaa cha 133A kinachoweka masharti ya bima ya lazima kwa majengo ya biashara, masoko ya umma, bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, vyombo vyaa majini na vivuko. Lengo la marekebiso haya ni kuongeza matumizi ya bima na kuimarissha ushirikishwaji wa kifedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ili kurekebisha kiwango cha riba ya pango la ardhi ambayo hajjalipwa baada ya miezi sita ya kwanza kuwa ni asilimia 0.5 na asilimia Moja baada ya miezi Sita inayofuata kuisha na deni kuwa halijalipwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, inapendekezwa kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha mamlaka ya kusamehe madeni ya riba yatokanayo na malimbikizo ya pango la ardhi baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili kama ilivyorekebushwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza ushuru wa hoteli kutoka asilimia 10 hadi Tano.

(ii) Kupunguza ushuru wa mazao kwenye misitu na kuwa asilimia Tatu badala ya Tano na kupunguza gharama kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu na kuwianisha kiwango hiki na mazao mengine ya kilimo;

(iii) Kusamehe ushuru wa mazao kwenye mbegu ili kuwapa unaifuu wakulima na kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tatu na Ishirini na Nne kama zilivyorekebushwa, zinapendekeza marekebisho ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa Sura ya 288, ili kuanzisha vituo vya Utoaji Huduma za Pamoja kwa ajili ya kuchocheara, kukuza na kuboresha biashara katika maeneo yao ya utawala na kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa mamlaka ya kutunga kanuni zitakazoweka utaratibu wa uendeshaji wa vituo hivyo. Lengo la marekebisho haya ni kuboresha mazingira ya ufanyakaji biashara na uwekezaji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tano inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123 kifungu cha 87(1) ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa makaa ya mawe yanayotumika kama malighafi ya viwandani kutoka asilimia Tatu hadi asilimia Moja na kiwango cha mrabaha kinacholipwa kwa dhahabu zinazouzwa katika viwanda vya kusafisha madini kutoka asilimia Sita hadi Nne. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuvutia uwekezaji, kukuza ajira na kuhakikisha kuwa vituo vya kusafishia madini vinapata malighafi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura ya 437 kifungu cha 46A ili kutoza tozo kwenye miamala yote ya kielektroniki isipokuwa malipo ya mishahara. Aidha, inapendekezwa kupunguza tozo ya miamala ya kiwango cha juu kuwa kiwango kisichozi Shilingi 4,000 kutoka kile cha awali kilichokuwa Shilingi 10,000 kwa kila muamala. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kwenye utozaji wa tozo na kuweka unafuu kwa kushusha kiwango kile kutoka 10,000 hadi 4,000.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Saba yenye Ibara 93 na 94 inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Afya Mahali pa Kazi, Sura Na. 297 ambapo Kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuweka sharti kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nane inarekebisha Sheria ya Bandari, Sura ya 166 Kifungu cha 67(3) ili kuwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru huo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tisa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38 ambapo Kifungu cha 20 kinarekebisha ili kuwezesha vivutio vya kodi vilivyotolewa na Kamati ya Uwekezaji kuweza kutolewa hapa nchini kwa Sheria husika ya Kodi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Moja kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399 kama tulivyoainisha vipengele ambavyo vinarekebishwa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Nne inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura Na. 408 kama ambavyo tumeionesha katika Jedwali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Tano inayopendekeza marekebisho ya Sheria ya Utalii, Sura Namba 65 kama tulivyoibainisha.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha maelezo yangu, napenda kuchukua fursa hii kutoa maelezo kuhusu malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, nakumbuka Mheshimiwa Mbunge wa Makete alilisemea kwa nguvu kubwa sana suala linalohusu *unclaimed assets* hususan fedha za Watanzania kwenye mitandao ya simu.

Mheshimiwa Spika, tunalifanyia kazi jambo hili, tunayafanyia kazi malalamiko haya, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Mipango inakamilisha mapendeleko yatakayowezesha kutungwa kwa Sheria mahsus ya Usimamizi wa Rasilimali za fedha zilizotelekezwa ili kuweka taratibu za kisheria wa usimamizi wa rasilimali kama hizo. Serikali inatarajia kukamilisha mchakato huo katika mwaka wa fedha huu 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ninapomalizia nimpongeze sana Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa vijana wake wa Tanzania *Prisons* jana kuweza kujinasua hatua moja kubwa kutoka kwenye kushuka daraja. Niwapongeze mabingwa wapya jana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wametetemesha Dar es Salaam na Dar es Salaam ilisimama.
(Makofii)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea hapo awali, mengi ya marekebisho ninayoyapendekezo ni utekelezaji wa kisheria wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MAELEZO YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2022 (The Finance Act, 2022) pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri mbalimbali ili kuuboresha.

3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya wadau mbalimbali hususan Kamati ya Bunge ya Bajeti na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wakati wakichangia katika hotuba ya bajeti ya Serikali iliopitishwa hapa Bungeni tarehe 24 Juni, 2022. Aidha, namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waandishi wa Sheria, wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebisho yake. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Saada Mkuya,

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar pamoja na wataalam wake kwa mashauriano tuliyofanya ili kuhakikisha kwamba Sheria za kodi tunazozitekeleza baina ya pande mbili za Muungano hazileti mgongango katika utekelezaji.

4. ***Mheshimiwa Spika***, lengo la Muswada huu ni kutekeleza kisheria, hatua za mapato zinazohusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 14 Juni mwaka huu. Muswada huu unafanyia marekebisho ya sheria **thelathini na Tano** zinazohusu masuala ya fedha, kodi, ushuru na tozo kwa lengo la kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo. Lengo la kurekebisha Sheria hizi ni kuweka mfumo wa kodi ambao ni tulivu na unaotabirika, kuboresha taratibu za ulipaji na ukusanyaji kodi na kuweka na kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kuchocheara kasi ya ukuaji wa uchumi na kuongeza mapato ya Serikali.

5. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia marekebisho yaliyofanyika kupitia Jedwali la Marekebisho, Sheria zinazofanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

- i) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156;
- ii) Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
- iii) Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213;
- iv) Sheria ya Korosho, Sura ya 203;
- v) Sheria ya Usajili wa Makampuni, Sura ya 212;
- vi) Sheria ya Hakimilili, Sura ya 218;
- vii) Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262;
- viii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
- ix) Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306
- x) Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414;
- xi) Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
- xii) Sheria ya Mbolea, Sura ya 378;
- xiii) Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura ya 84;
- xiv) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
- xv) Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada, Sura ya 134;

- xvi) Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi, Sura ya 120;
- xvii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- xviii) Sheria ya Bima, Sura ya 394;
- xix) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
- xx) Sheria ya Udhhibit wa Usafirishaji wa Nchi Kavu, Sura ya 413;
- xxi) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
- xxii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;
- xxiii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;
- xxiv) Sheria ya Madini, Sura ya 123;
- xxv) Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura ya 437;
- xxvi) Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297;
- xxvii) Sheria ya Bandari, Sura ya 166;
- xxviii) Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38;
- xxix) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
- xxx) Sheria ya Wakala wa Meli, Sura ya 415;
- xxxi) Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438;
- xxxii) Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408;
- xxxiii) Sheria ya Usajili wa Wadhamini, Sura ya 318;
- xxxiv) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148; na
- xxxv) Sheria ya Mafunzo na Ufundu Stadi, Sura ya 82;

6. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia majadiliano na wadau mbalimbali hususan michango ya Wabunge wakati wakijadili bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 na maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti, Serikali imefanya marekebisho mbalimbali ya hatua za mapato zilizowasilishwa kuititia hotuba ya bajeti ikiwemo yafuatayo;

(i) kupunguza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (Gaming Tax on Winnings) kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10 kwenye michezo ya kubahatisha ya ubashiri wa matokeo ya michezo (Sports betting). Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Serikali kutokana na watu wengi zaidi kuhamasika kushiriki kwenye michezo ya kubahatisha ya kubashiri matokeo ya michezo. Uchambuzi uliofanyika umebainisha

kwamba endapo Serikali itaendelea kupunguza kiwango husika hadi kufikia asilimia 10 mapato ya Serikali yataongezeka kutoka shilingi bilioni 4.2 hadi kiasi cha shilingi bilioni 5.2 kutokana na watu wengi zaidi kuhamasika kushiriki katika michezo hiyo;

(ii) kutofanya marekebisho ya kubadili mgawanyo wa asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuhudumia miundombinu ya masoko ya machinga. Serikali itatumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali katika bajeti ya mwaka 2022/23 (bilioni 1 kwa kila Mkoa) kwa Halmashauri za Majiji na Manispaa zitumike kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na masoko ya machinga;

(iii) kuondoa pendekezo la kutoza Kodi ya Zui o kwa kiwango cha asilimia 2 kwenye malipo ya wachimbaji wadogo wa madini (Small Scale Miners). Utozaji wa kodi husika utasababisha utoroshaji wa madini na kupunguza kasi ya wachimbaji kuuza madini husika katika masoko ya madini (Buying Centres/Gem Houses) au vituo vyta uchenjuaji (refinery centres);

(iv) kuondoa hatua ya kutoza kodi ya awali ya mapato (advance income tax) ya shilingi 20 kwa lita kwa wafanyabiashara wa rejareja wa mafuta ya petroli nchini ambayo ingekusanywa na waingizaji wa mafuta hayo kwa jumla na kulipwa Serikalini. Hatua hii inatokana na kutotabirika kwa bei za mafuta ambazo zilionekana kuanza kushuka mwezi Mei, 2022 lakini bei hizo sasa zinaonekana kupanda;

(v) kufanya maboresho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa nchini kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini sambamba na kusamehe kodi hiyo kwenye malighafi na vifungashio vinavyotumika katika uzalishaji. Lengo la hatua hii ni kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliopanda kutokana na m dororo wa uchumi na kulinda misingi ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani inayoelekeza bidhaa zinazouzwa ndani ya nchi zisamehewe

kodi hiyo (exempted) badala ya kutozwa kodi ya asilimia 0 (zero rated) ili kurahisisha utekelezaji wa msamaha huu;

(vi) Serikali imefanya uamuzi wa kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) ili taasisi hiyo isijihushe na jukumu la uwakala wa forodha na badala yake ibaki na jukumu la kusimamia na kudhibiti watoa huduma za usafiri majini. Hata hivyo, taasisi hii itaendelea na shughuli za uwakala wa forodha kwenye bidhaa za makinikia, silaha na vilipuzi, nyara za Serikali na wanyama hai wanaotambulika kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori. Hatua hii itaondoa mgongano wa kimaslahi unaotokana na TASAC kuwa mtoa huduma za uwakala wa forodha na mdhibiti wa watoa huduma za usafiri majini kwa wakati mmoja;

(vii) kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ardhi, Sura 113 ili kuweka utaratibu kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha baada ya kufanya mashauriano na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Ardhi mamlaka ya kusamehe riba ya malimbikizo ya pango la ardhi. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kuongeza mapato ya serikali kwa kukusanya malimbikizo ya kodi husika; na

(viii) kuongeza wigo wa kusamehe tozo ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wahitimu wa elimu ya juu na vyuo vya kati badala ya vyuo vikuu pekee kama niliyopendekeza awali kwenye Hotuba ya Bajeti. Lengo la hatua hii ni kuongeza idadi ya wanufaika wa mafunzo ya vitendo ya kuwapatia ujuzi na uzoefu wa kazi kabla ya ajira kuititia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TAESA).

(ix) Kusogea muda wa kufutwa kwa msamaha wa kodi ya Ongezeko la thamani kwenye huduma za kukodi ndege (air charter service) kwa kipindi cha miezi 6 kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 ili kutoa fursa ya utekelezaji wa miadi iliyowekwa kwa kuzingatia uwepo wa msamaha huo.

7. *Mheshimiwa Spika*, Aidha, ili kuboresha taratibu za usimamizi na ukusanyaji wa kodi ya mapato kwa Serikali ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na kufuatia mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tumefanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato na Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili kuwezesha yafuatayo;

(i) kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweka viwango mfuto vyakodi kwa walipa kodi binafsi wadogo (presumptive rates) vitakavyotumika Tanzania Zanzibar;

(ii) kutoa nafuu ya kodi ya mapato kwa kuwezesha kampuni zinazofanya biashara pande mbili za Muungano kupata nafuu ya kodi inayolingana na kodi iliyolipwa upande wowote wa Muungano ili kuepusha utozaji kodi mara mbili; Katika kutekeleza hatua hii, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 itatambua namba ya utambulisho ya mlipakodi aliyesajiliwa Tanzania Zanzibar ili kurahisisha taratibu za ukusanyaji kodi kwa kampuni zenye ofisi pande mbili za Muungano; Pamoja na marekebisho hayo ya Sheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato ya Tanzania Zanzibar zitasaini Hati ya Makubaliano ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hizi.

MAUDHUI YA MUSWADA:

8. Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu **Thelathini na Sita** kama ifuatavyo: -

9. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, inahusu masuala ya utangulizi inayojumuisha jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii ambapo Sheria itaanza kutumika tarehe 1, Julai 2022.

10. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, Nane, Kumi na Moja, Kumi na Tatu, Ishirini na moja, na Thelathini na Mbili kama zilivyorekebishwa, zinapendekeza kurekebisha Sheria ya

Magonjwa ya Wanyama, Sura ya 156; Sheria ya Tasnia ya Maziwa, Sura ya 262; Sheria ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, Sheria ya Mbbolea, Sura ya 378; Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu, Sura ya 413; na Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415, ili kuondoa mwingiliano wa sheria mbalimbali za taasisi za udhibiti hususan kwa kurejesha suala la usimamizi wa viwango kusimamiwa na Shirika la Viwango Tanzania badala ya utaratibu wa sasa ambapo kila Taasisi ya udhibiti ina mamlaka ya kusimamia masuala ya viwango kwenye eneo lake. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha shughuli za udhibiti wa viwango zinafanywa na Taasisi moja ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Hata hivyo, kupitia Jedwali la marekebisho, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Sura ya 172, yameondolewa kwenye Muswada huu kutokana na unyeti wa shughuli za mawasiliano.

11. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu kama ilivyorekebishwa*, inapendekeza kufanya marekebisho katika **Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197 kwenye vifungu vya 35(2) na 36(1) ili kuongeza kiwango cha ukomo wa Serikali kukopa kutoka Benki Kuu. Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha Serikali kutekeleza Bajeti zake kwa ufanisi hususan kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo.**

12. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne kama ilivyorekebishwa* inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 ili:**

(i) kuongeza tafsiri ya neno “beneficial owner” ili kuwianisha tafsiri hiyo na ile iliyotolewa katika Sheria ya Kudhibiti Utakashihaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423;

(ii) kuweka sharti la kuwasilisha taarifa za wamiliki wanufaika wakati wa usajili wa biashara zinazoendeshwa kwa ubia;

(iii) kubainisha watu au taasisi ambazo zinaweza kupata taarifa za mmiliki mnufaika; na

(iv) kuweka faini kwa kushindwa kutoa taarifa zinazohusiana na wamiliki wanufaika wa ubia.

Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na upatikanaji wa taarifa za wamiliki wanufaika.

13. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano* inapendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 17A cha **Sheria ya Korosho, Sura ya 18** ili kuainisha mgawanyo wa mapato yatokanayo na korosho ambapo asilimia 50 itaenda Mfuko Mkuu wa Hazina, na asilimia 50 itagawanywa kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo na ruzuku za pembejeo za kilimo. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha maendeleo ya sekta ya Kilimo kwa kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya ruzuku, pembejeo na maendeleo ya kilimo.

14. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita kama ilivyorekebishwa* inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Makampuni, Sura ya 212** kama ifuatavyo;

(i) Kama ilivyofanyika kwenye marekebisho ya **Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213**, kuongeza tafsiri ya neno "beneficial owner" ili kuwianisha tafsiri hiyo na ile iliyotolewa katika Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, Sura ya 423;

(ii) kuweka adhabu kwa makampuni ambayo yatashindwa kutunza rejestra ya wanachama na wamiliki wanufaika au kutoa taarifa ya mabadiliko kwenye rejestra, kushindwa kuweka fahirisi ya majina ya wanachama na wamiliki wanufaika wa kampuni na kushindwa kuwasilisha ritani ya kila mwaka ya kampuni;

(iii) kuweka adhabu kwa makampuni ambayo yatashindwa kutunza rejestra ya wanachama na wamiliki wanufaika au kutoa taarifa ya mabadiliko kwenye rejestra, na kushindwa kuweka fahirisi ya majina ya wanachama na wamiliki wanufaika wa kampuni; na

(iv) kuweka wajibu kwa wafilisi wa makampuni kutunza kumbukumbu za hesabu na nyaraka zinazohusiana na ufilisi wa Makampuni.

15. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba kama ilivyorekebishwa* inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sura ya 218 ili;**

(i) kuongeza tafsiri ya maneno “collective management” na “collective management organization” ili kuweshesha ufanisi kwenye utekelezaji wa Sheria;

(ii) ili kuondoa mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza majukumu ya Chama cha Hakimiliki Tanzania na Ofisi ya Hakimiliki;

(iii) kutenganisha majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki na majukumu ya taasisi za usimamizi jumuishi na kuainisha majukumu ya Ofisi hiyo;

(iv) kuanzisha tozo ya asilimia 1.5 kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kurudufu na kutunza kazi za sanaa ambavyo ni *radio/tv set enabling recording, analogue audio recorders, analogue video recorders, CD/DVD copier, digital jukebox and mp3 player*; vinavyotumika kuweshesha kuzalisha, kusambaza, kurudufu na kutunza kazi za sanaa, uandishi na ubunifu mwingine; na

(v) kubainisha majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki na kuweka mfumo wa usimamizi jumuishi wa hakimiliki na kuweka wajibu kwa taasisi za usimamizi jumuishi kuwasilisha Ofisi ya Hakimiliki taarifa zao za utendaji na hesabu zilizokaguliwa.

Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uwajibikaji na kuimarisha usimamizi wa masuala yanayohusu hakimiliki na hakishirikishi.

16. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa* kama ilivyorekebishwa, inapendekeza marekebisho katika **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo;**

- (vi) kuwianisha mfumo wa adhabu katika sheria za kodi ili kuhakikisha kuwa adhabu zitakazotumika dhidi ya makosa ya kikodi ni zile zilizoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438;
- (vii) kujumuisha katika sheria watoa huduma wa televisheni za kulipia wanaotumia miundombinu mingine tofauti na ile ya ardhini;
- (viii) kurekebisha Jedwali la Nne ili kubainisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za sukari na betri za maji kwa lengo la kupanua wigo wa kodi na kulinda afya za walaji na mazingira. Aidha, kupitia marekebisco yaliyofanyika kwenye kupitia Jedwali la Marekebisco, bidhaa za sukari zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zitatozwa ushuru wa bidhaa kwa kiasi cha shilingi 1,000 na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa nchini hazitatozwa. Aldha, betri kutoka nje ya nchi zitatozwa ushuru wa asilimia 10 na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa nchini zitatozwa asilimia 5. Vilevile, Jedwali linarekebishwa ili kusamehe ushuru wa bidhaa kwenye vifungashio vya maua, matunda na mbogamboga kwa lengo la kuwapunguzia gharama wauzaji wa bidhaa hizo nje ya nchi na kuongeza ushindani wa bidhaa hizo katika masoko ya kimataifa.

17. Mheshimiwa Spika Sehemu ya Kumi kama ilivyorebishesha inapendekeza marekebisco ya **Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 kwa kuongeza kifungu kipyaa cha 164B ili kutoza ada ya matumizi ya kisimbuzi kuanzia shilingi 500 hadi 2,000 kulingana na kiwango cha matumizi kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali. Mchanganuo wa utozaji wa ada hii kulingana na matumizi utabainishwa kwenye Kanuni.**

18. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili inapendekeza marekebisco ya **Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196 ambapo Jedwali linarekebishwa ili kuweka tozo ya usafirishaji wa shaba chakavu na vyuma chakavu nje ya nchi. Lengo la marekebisco haya ni kulinda**

viwanda nya ndani na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda nya ndani nya bidhaa za shaba na chuma.

19. Mheshimiwa Spika Sehemu ya Kumi na Nne inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura ya 84** kwa kupunguza ada ya magari ya kigeni yanayozidi ekseli 3 yanayopita nchini kwa lengo la kuwianisha viwango nya ada zinazotozwa nchini na zile zinazotozwa katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Masharika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, na Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika.

20. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tano kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41** kama ifuatavyo:

- (i) kupunguza kiwango cha kodi kinachohusiana na zawadi ya ushindi kutoka asilimia 15 hadi 10 kwenye michezo ya kubashiri matokeo;
- (ii) kuainisha masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 yatakayotumika katika kodi ya michezo ya kubahatisha; na
- (iii) kuweka utaratibu wa ukusanyaji wa kodi kwenye zawadi za ushindi katika michezo ya kubahatisha.

21. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Sita inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134** ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa deni la taifa kwa kufanya yafuatayo:

- (i) kuboresha utaratibu wa ukokotoaji wa uhimiliwu wa deni kwa kutumia uchambuzi wa madeni unaotumia kipimo zaidi ya kimoja;
- (ii) kumwezesha Kamishna wa Usimamizi wa Madeni kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wataalam na kuboresha uwakilishi wa wajumbe katika Kamati ya Wataalamu; na

(iii) kuipa jukumu Idara ya Usimamizi wa Madeni la kufanya kazi ya uchambuzi na uandaaji wa nyaraka zinazowasilishwa kwenye Kamati za Madeni.

22. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Saba* inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi, Sura ya 120** ili kuondoa ngozi au bidhaa za ngozi za wanyamaporii katika wigo wa Sheria hiyo. Lengo la marekebisho haya ni kuondoa mgongano wa sheria na mwingiliano wa majukumu kati ya vyombo vinavyosimamia ngozi na bidhaa za ngozi za wanyama wa majumbani na vile vinavyosimamia ngozi na bidhaa za ngozi za wanyamaporii.

23. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Nane kama ilivyorekebiswa* inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332** kama ifuatavyo:

(i) kuongeza tafsiri ya maneno "*digital market place*," "*electronic services*" ili kuwezesha utozaji kodi kwenye huduma za kidigitali;

(ii) kuongeza tafsiri ya maneno "*alternative financing arrangement*" na kurekebisha kifungu cha 32 ili kuwianisha maana ya riba inayotolewa kwa mikopo ya kawaida ya kibenki kuwa sawa na faida kwa mikopo mbadala;

(iii) kuweka utaratibu maalum wa kulipa kodi kwa wamiliki wa mabasi na malori kwa viwango maalumu kulingana na ukubwa wa gari;

(iv) kuondoa kwenye wigo wa kutozwa kodi faida ambayo hajagawanywa na taasisi za fedha za ndani ya nchi zilizo na matawi nje ya nchi kwa misingi au taratibu zilizowekwa na Benki Kuu ya Tanzania;

(v) kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

masharti ya Sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji kuhusu utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi;

(vi) kujumuisha uendeshaji na usimamizi wa biashara unaofanyika kwa njia za kielektroniki;

(vii) kuongeza malipo ya utumiaji rasilimali pamoja na huduma za kidigitali zinazotolewa na watoa huduma wasio wakaazi hapa nchini kwa lengo la kupanua wigo wa kodi;

(viii) kuwezesha wapangaji binafsi kuzuia kodi ya mapato kwenye malipo ya pango ya nyumba za biashara na makazi; Pia Sheria inarekebishwa ili kuondoa sharti la kukata kodi ya zuio kwenye malipo ya pango ya nyumba za biashara na makazi. Lengo la marekebisho haya ni kuleta ufanisi wa ukusanyaji wa kodi ya pango na kuongeza vyanzo mbadala vya fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo;

(ix) kutoza kodi ya mapato ya asilimia 2 kwenye malipo yanayofanywa kwa watoa huduma za kidijitali wasio wakaazi kwa lengo la kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya Serikali;

(x) ili kuwaondolea wajibu wa kuwasilisha ritani za kodi ya mapato walipakodi wa kidijitali wasio wakaazi;

(xi) kumwezesha Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya Mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuweka viwango mfuto vya kodi kwa walipa kodi binafsi wadogo vitakavyotumika Tanzania Zanzibar;

(xii) kutoa nafuu ya kodi ya mapato kwa kuwezesha kampuni zinazofanya biashara pande mbili za Muungano kupata nafuu ya kodi inayolingana na kodi iliyolipwa upande wowote wa Muungano ili kuepusha utozaji kodi mara mbili; Katika kutekeleza hatua hii, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438 itatambua namba ya utambulisho ya mlipakodi aliyesajiliwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tanzania Zanzibar ili kurahisisha taratibu za ukusanyaji kodi kwa kampuni zenyе ofisi pande mbili za Muungano;

(xiii) kurekebisha Jedwali la Kwanza ili kurekebisha kiwango cha kodi kwenye daraja la juu la mauzo kwa walipakodi binafsi wadogo ili kuongeza uwazi na kurahisisha ukadiriaji na ulipaji wa kodi. Aidha, Jedwali la Kwanza linarekebishwa kwa kupunguza kiwango cha kodi ya zuio kwa malipo ya mrabaha ya filamu kwa watoa huduma wa nje na ndani ya nchi kwa lengo la kuongeza ajira, kukuza tasnia ya filamu na kuchochea uhaulishaji wa ujuzi; na

(xiv) kurekebisha Jedwali la Pili ili kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji kwenye uhamishaji wa haki na taarifa za uchimbaji madini kwenda Kampuni za Ubia, uhamishaji wa hisa kwenda Serikalini, na kwenye hisa ambazo Serikali imepata kuitia Msajili wa Hazina. Lengo la marekebisheso haya ni kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuhakikisha kuwa uhamishaji wa haki na taarifa za madini unafanyika kwa wakati.

Aidha, kama nilivyoeleza awali, kuitia Jedwali la marekebisheso, Serikali imeondoa pendekezo la kutoza kodi ya zuio kwa wachimbaji wadogo wa madini na kuondoa sharti kwa waagizaji wa nishati ya mafuta kwa jumla kuwa mawakala wa ukusanyaji kodi wa Serikali kutoka kwa wauzaji wa reja reja wa nishati ya mafuta.

24. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Tisa inapendekeza marekebisheso ya **Sheria ya Bima, Sura ya 394** kwa kuongeza kifungu kipyä cha 133A kinachoweka masharti ya bima ya lazima kwa majengo ya biashara, masoko ya umma, bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, vyombo vyä majini na vivuko. Lengo la marekebisheso haya ni kuongeza matumizi ya bima na kuimarisha ushirikishwaji wa kifedha hapa nchini.

25. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini kama ilivyorekebisheswa inapendekeza marekebisheso ya **Sheria ya Ardhi, Sura ya 113** ili kurekebisha kiwango cha riba ya pango la ardhi ambayo haijalipwa baada ya miezi sita ya kwanza

kuwa ni asilimia 0.5 na asilimia 1 baada ya miezi sita inayofuata kuisha na deni kuwa halijalipwa. Aidha, inapendekezwa kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha mamlaka ya kusamehe madeni ya riba yatokanayo na malimbikizo ya pango la ardhi baada ya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi.

26. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Mbili kama ilivyorekebishwa* inapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama ifuatavyo:**

- (i) kupunguza ushuru wa mazao kwenye misitu na kuwa asilimia 3 badala ya 5 ili kupunguza gharama kwa wafanyabiashara wa mazao ya misitu na kuwianisha kiwango hiki na mazao mengine ya kilimo;
- (ii) kusamehe ushuru wa mazao kwenye mbegu ili kuwapa unafuu wakulima na kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali.
- (iii) Kuondoa pendeleko la kupunguza ushuru wa hoteli kutoka asilimia 10 hadi 5, ili kutoathiri utekelezaji wa bajeti za Halmashauri ambazo tayari zilizingatia mapato hanayotokana na ushuru huu.

27. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tatu na Ishirini na Nne kama zilivyorekebishwa* zinapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288** ili kuanzisha vituo vya Utoaji Huduma za Pamoja kwa ajili ya kuchocheara, kukuza na kuboresha biashara katika maeneo yao ya utawala na kumpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa mamlaka ya kutunga kanuni zitakazoweka utaratibu wa uendeshaji wa vituo hivyo. Lengo la marekebiso haya ni kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji.**

28. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tano* inapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Madini, Sura ya 123**

kifungu cha 87(1) ili kupunguza kiwango cha mrabaha kwa makaa ya mawe yanayotumika kama malighafi ya viwandani kutoka asilimia 3 hadi asilimia 1 na kiwango cha mrabaha kinacholipwa kwa dhahabu zinazouzwa katika viwanda vyta kusafisha madini kutoka asilimia 6 hadi 4. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuvutia uwekezaji, kukuza ajira na kuhakikisha kuwa vituo vyta kusafisha madini vinapata malighafi ya kutosha.

29. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Sita kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Mifumo ya Malipo, Sura ya 437** kifungu cha 46A ili kutoza tozo kwenye miamala yote ya kielektroniki isipokuwa malipo ya mishahara. Aidha, inapendekeza kupunguza tozo ya miamala ya kiwango cha juu kuwa kiwango kisichozidi shilingi 4,000 kwa kila muamala wa kielektroniki. Lengo la marekebisho haya ni kuweka usawa kwenye utozaji wa tozo hii kwenye miamala inayofanana.

30. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Saba yenyewe lbara za 93 na 94 inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297** ambapo kifungu cha 17 kinarekebishwa ili kuweka sharti kwa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kutoa leseni ndani ya siku saba toka kupokelewa kwa maombi ya leseni baada ya mwombaji kukidhi vigezo. Lengo la marekebisho haya ni kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini.

31. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Nane kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Bandari, Sura ya 166** kifungu cha 67(3) ili kuwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya ushuru wa bandari na mapato husika kuhifadhiwa katika akaunti maalum itakayofunguliwa Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, fedha hizi zitatumwa na Mamlaka ya Bandari baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali.

32. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Ishirini na Tisa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Uwekezaji Tanzania**,

Sura ya 38 ambapo kifungu cha 20 kinarekebishwa ili kuwezesha vivutio vya kikodi vilivyoidhinishwa na Kamati ya Uwekezaji ya Taifa kutolewa chini ya sheria husika za kodi baada ya kuridhiwa na Baraza la Mawaziri. Marekebisheso haya yanalenga kuwianisha masharti ya Sheria hii na masharti ya sheria za kodi kuhusu utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi.

33. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Moja kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399* kama ifuatavyo:

(i) kutambua ada kwenye huduma za kitaalamu zinazotolewa na TRA kama sehemu ya ada zinazotozwa na kukusanywa na Mamlaka hii;

(ii) kuwezesha mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kutohana na uchakataji wa nyaraka za uingizaji wa mizigo nchini kutoingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja na mapato hayo yatumike kuboresha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato.

34. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Mbili kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Wakala wa Meli, Sura ya 415 ili Shirika la Wakala wa Meli libaki na jukumu la kusimamia watoa huduma za usafiri majini na shughuli za uwakala wa forodha kwenye bidhaa za makinikia, silaha na vilipuzi, nyara za Serikali na Wanyama hai wanaotambulika chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.*

35. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Tatu kama ilivyorekebishwa inapendekeza marekebiso ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 ili pamoja na mambo mengine kufanya yafuatayo:*

(i) kuweka sharti kwa kila mtanzania mwenye kitambulisho cha Taifa kupata Namba ya Mlipa Kodi. Vilevile, kuhakikisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Namba ya Mlipakodi inayotolewa inaoanishwa na Namba ya Kitambulisho cha Taifa;

(ii) kuweka masharti yanayohusu mamlaka ya utoaji leseni, usimamizi na ufuatiliaji wa mienendo ya washauri wa kodi;

(iii) kuweka utaratibu wa usajili wa maghala ili kuwezesha ufuatiliaji wa kodi;

(iv) kuwezesha adhabu mbalimbali za kikodi kushughulikiwa chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi;

36. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Nne* inapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Rufaa za Kodi, Sura ya 408** kifungu cha 22 ili kuwezesha migogoro ya kikodi baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na walipakodi kutatuliwa bila kuhusisha msuluhishi. Lengo la marekebiso haya ni kuwezesha utatuvi wa migogoro kwa haraka na kwa gharama nafuu.

37. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Tano* inayopendekeza marekebiso ya **Sheria ya Utalii, Sura ya 65** imeondolewa kwa kuwa marekebiso yanayopendekezwa yalishafanyika kuititia Sheria ya Marekebiso ya Sheria Mbalimbali, Na. 5 ya 2021.

38. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Sita* inapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Udhamini Sura ya 318** ili pamoja na mambo mengine kumwezesha mdhamini aliye po kutoa taarifa za mabadiliko za mdhamini au mmiliki mnufaika au mdhamini mpya aliye teuliwa kwa Kabidhi Wasihi Mkuu. Vilevile, marekebiso haya yanatoa adhabu kwa mdhamini atakayeshindwa kutoa taarifa zinazohitajika. Lengo la marekebiso haya kuweza kukidhi matakwa ya kimkataba wa Kimataifa wa ubadilishanaji taarifa za kikodi wa Mataifa wanachama.

39. *Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Saba kama iliyorekebishwa* inapendekeza marekebiso ya **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148** kama ifuatavyo:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) kuongeza tafsiri ya maneno "*alternative financing product*" na kurekebisha kifungu cha 94 ili kuwianisha maana ya riba inayotolewa kwa mikopo ya kawaida ya kibenki kuwa sawa na faida kwa mikopo mbadala;
- (ii) kumpa Waziri mamlaka ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa wawekezaji mahiri maalumu baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri. Lengo la marekebisho haya ni kuwianisha masharti ya Sheria hii na masharti ya Sheria ya Uwekezaji kuhusu utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi;
- (iii) kuongeza kwenye orodha ya bidhaa za mtaji zinazopata ahirisho la kodi kwa matrela na vichwa vya magari ya mizigo viliviyotengenezwa au kuunganishwa hapa nchini vinavyobainishwa kwenye Heading 8716 na HS Code 8701.20.90 chini ya utaratibu wa kiforodha unaotambua wazalishaji kwa utaratibu wa dhamana (*manufacturing under bond*). Lengo la marekebisho haya ni kulinda viwanda vya ndani na kuchochea shughuli za biashara ya usafirishaji nchini;
- (iv) kurahisisha utaratibu wa usajili wa walipa kodi wanaotoa huduma za kidigitali bila ya kuwa na makazi hapa nchini hivyo ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye biashara zinazofanyika kwa njia ya mtandao;
- (v) kurekebisha Jedwali katika Sehemu ya kwanza ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye uuzaaji wa miti hai kwa lengo la kuwezesha kodi kutozwa pale tu bidhaa za misitu zitakapokuwa zimeongezwa thamani; kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya kupima kiwango cha maji na unyevunyevu na vifaa vya utabiri wa hali ya hewa kwa lengo la kukuza utafiti na kuendeleza sekta ya kilimo pamoja na kuimarisha shughuli za utabiri wa hali ya hewa nchini; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mtindi na maziwa yanayozalishwa kwa joto la juu na kudumu kwa muda mrefu (UHT Milk), pamoja na kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifungashio vya maziwa kwa lengo la kutoa unafuu kwa

watumiaji wa bidhaa za maziwa, kulinda viwanda vya ndani na kuongeza ajira.

Aidha, inapendekezwa kusamehe kodi kwenye hereni za mifugo na vifaa vingine vya ufugaji vinavyotambulika kwa lengo la kuleta ufanisi katika utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo nchini; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vanilla ya kijani isiyochakatwa, vyandarua vinavyotumika katika uzalishaji wa mbogamboga na maua pamoja na vifaa vya uvuvi kwa lengo la kuchocha ukuaji wa sekta ya kilimo na uvuvi nchini. Vilevile, kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye kamba za katani kwa lengo la kukuza kilimo cha zao la katani na kuongeza ajira nchini. Vilevile, Jedwali husika linapendekezwa kurekebishwa ili kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye simu janja za mkononi, vishikwambi na modemu, kwa lengo la kupanua wigo wa kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

Marekebisho mengine yanapendekezwa katika Jedwali ili kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye magari yenyen jokofu na vyumba vya ubaridi kwa lengo la kuchocha ukuaji wa sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi nchini; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vifaa vya machinjio ili kuhamasisha uchakataji bora wa nyama nchini; kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi na mashine zinazotumika kuzalisha mbolea nchini na kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye malighafi za kutengenezea mitungi ya gesi kwa lengo la kutoa unafuu kwa wazalishaji wa mbolea na mitungi ya gesi, kuchocha uwekezaji na kuongeza ajira.

40. Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Thelathini na Nane kama ilivvorekebishwa inapendekeza marekebisho ya **Sheria ya Mafunzo ya Ufundu Stadi, Sura ya 82 ambapo kifungu cha 19 kinarekebishwa kwa lengo la kutoa motisha kwa waajiri wanaowapa nafasi ya mafunzo kwa vitendo wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya kati chini ya mpango wa TAESA katika maeneo yao ya kazi. Lengo la marekebisho hayo ni kuongeza idadi ya wanufaika wa mafunzo hayo watakaopatiwa ujuzi na uzoefu wa kazi kabla ya ajira.**

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

41. **Mheshimiwa Spika**, baadhi ya hatua nyingine za mapato zilizopo katika Hotuba ya Bajeti na ambazo hazijabainishwa kwenye Muswada huu, zitatekelezwa na Mawaziri husika kupitia Kanuni na Matangazo ya Serikali (Government Notices) kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika.

42. **Mheshimiwa Spika**, kabla sijahitimisha maelezo yangu, napenda kuchukua fursa hii kutoa maelezo kuhusu malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuhusu kutokuwepo kwa utaratibu wa kisheria wa usimamizi wa rasilimali fedha zilizotelekelezwa (*unclaimed assets*) hususan fedha za watanzania kwenye mitandao ya simu.

43. **Mheshimiwa Spika**, tunafanya kazi malalamiko haya, na napenda kulifahamisha Bunge lako kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inakamilisha mapendekezo yatakayowezesha kutungwa kwa Sheria mahsusini ya Usimamizi wa Rasilimali fedha zilizotelekezwa ili kuweka utaratibu za kisheria wa usimamizi wa rasilimali hizo. Serikali inatarajia kukamilisha mchakato huu katika mwaka wa fedha 2022/23.

HITIMISHO:

44. **Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, mengi ya marekebisho ninayopendekeza ni utekelezaji wa **kisheria** wa mapendekezo ya Serikali kuhusu bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha ili kuwezesha Serikali kutekeleza bajeti yake.

45. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa hizi ni katika zile hoja ambazo utaratibu wa kuhoji unakuja baadaye tukishamaliza taratibu zetu. Waheshimiwa Wabunge sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Mheshimiwa Daniel Baran Sillo aje awakilishe mawazo yetu.

MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Juni, 2022, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali ya Muswada huu na baada ya kuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika uliiagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuuchambua Muswada huo.

Aidha, siku hiyo hiyo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande aliwasilisha Muswada huo mbele ya Kamati kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada. Kamati kwa muda wa siku Kumi ilifanya vikao kwa ajili ya kuuchambua Muswada huu. Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kujelimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, Kamati illitisha Maoni ya Umma “*Public Hearing*.” Wadau walioshiriki walitoka katika sekta zifuatazo:-

- (i) Sekta ya utalii,
- (ii) Sekta ya viwanda,
- (iii) Sekta ya usafiri na usafirishaji,
- (iv) Sekta ya kilimo,
- (v) Sekta ya habari na mawasiliano; na
- (vi) Wauzaji wa mafuta kwa Jumla na reja reja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilipata fursa ya kukutana na Watalaam wa Serikali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania - *TRA*, Ofisi ya Mwandishi wa Sheria pamoja na Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali zinazojitegemea.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yetu yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022. Muswada huu unafanya mabadiliko katika Sheria 38 zenye malengo makuu Saba kama ifuatavyo:-

- i. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara Nchini,
- ii. Kupanua wigo wa kodi kwa kuanza kutoza kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani kwa Biashara za Mtandano
- iii. Kuboresha usimamizi wa kodi kwa kuondoa mianya ya ukwepaji wa Kodi;
- iv. Kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvumi pamoja na kuvilinda viwanda vyatya ndani;
- v. Kuanzisha utaratibu wa ukusanyaji mrabaha, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya haki miliki za wasanii;
- vi. Kuanzisha utaratibu mpya utakaowezesha utoaji wa vivutio maalum kwa Wawekezaji mahiri; na
- vii. Kuanzisha vituo vya pamoja yaani *One Stop Centre* kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kushughuikia masuala ya Biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua mapendendekezo ya mabadiliko mbalimbali kuititia Sheria zilizoko kwenye Muswada ili kujiridhisha endapo yanaakisi malengo yaliyokusudiwa na hayataleta madhara kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

jamii, biashara na uwekezaji nchini. Hivyo maoni na mapendekezo ya kamati kuhusu muswada huu kwa kila Sheria ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki Kuu Sura 197. Mabadiliko yanayofanywa kwenye Sheria hii yana lengo la kuongeza wigo wa Serikali kukopa kutoka Benki Kuu kutoka wastani wa asilimia 12.5 ya makusanyo halisi ya mwaka wa fedha uliotangulia na kuwa asilimia 18 ya makusanyo yanayokadiriwa katika mwaka wa fedha unaotekelozwa. Baada ya majadiliano ya kina Kamati ilikubaliana na ongezeko la Serikali kukopa kutoka Benki Kuu hata hivyo kiwango hicho kikokotolewe kutokana na mapato halisi ya mwaka wa fedha uliopita na siyo mwaka wa Fedha unaotekelozwa. Hatua hii itaepusha kuwa na mzigo wa deni kubwa endapo mapato ya bajeti ya mwaka inayotekelozwa hayatafikiwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara Sura ya 213. Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali katika Sheria hii kwa sababu kimsingi ni mwendelezo wa Mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ambayo ililiridhiwa na Bunge mwezi Februari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Korosho, Sura ya 203. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutenga asilimia 50 ya mapato yanayotokana na ushuru wa mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi ambazo zitapelekwa kwenye mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, Ruzuku na Pembejeo. Rai ya Kamati kwa Serikali ni kuhakikisha mfuko huo unatumia fedha hizo kwa malengo yanayokusudiwa na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Makampuni Sura 212. Mabadiliko yanayofanyika katika Sheria hii yanalenga kuingiza dhana ya mnufaika yaani "*Beneficial Owner*" katika Sheria ya Makampuni. Aidha, marekebisho hayo ni muendelezo wa marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ambayo Bunge lako liliyaridhia mwezi Februari 2022.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Haki Miliki Sura ya 218. Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali kuhusu mabadiliko ya Sheria hii na kubainisha masuala yafuatayo:-

(i) Kuanzisha utaratibu mpya wa ukusanyaji, usimamizi na ugawaji wa mrabaha unaotokana na kazi za sanaa; na

(ii) Kuanzisha tozo ya asilimia 1.5 ya thamani ya kila kifaa kitakachoingizwa nchini kwa ajili ya kuhamishia, kutunzia, kudurufu na kusambaza bidhaa na huduma za sanaa ili kupunguza madhara ya upotevu wa mapato yanayotokana na uharamia wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali, hata hivyo inaendelea kushauri kwamba uanzishwe mfuko maalumu ambapo fedha hizi zitawekwa na kugawiwa. Ikibaki kama ilivyo fedha hizi zitaenda Mfuko Mkuu na itakuwa vigumu sana kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147. Serikali imekusudia kuanzisha Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zilizobainishwa katika kichwa 17.04 na 19.05 kwa lengo la kudhibiti madhara ya kiafya yanayoweza kujitokeza kutoptaka na matumizi ya Bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kutoptaka ushuru kwa bidhaa hizo zinazozalishwa nchini zilizotajwa katika kichwa 17.04 na kichwa 19.05 kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kwa bidhaa za pipi na chokuleti zinazozalishwa na viwanda vya ndani, Kamati imebaini kwamba viwanda hivi vina changamoto ya uzalishaji kutoptaka na kupanda kwa bei za malighafi zinazotumika kuzalisha bidhaa hizo;

(ii) Bidhaa hizi ndizo biashara kuu ya wafanyabiashara wadogo waliopo katika maeneo ya stendi kuu za mabasi; na

(iii) Nchi jirani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hazitozi kodi hii na kwa sababu tuko kwenye jumuiya moja bidhaa hizi kutoka nchi jirani zitakuwa na bei nafuu kuliko zinazozalishwa nchini na hivyo kuleta ushindani usio sawa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuongeza ushuru wa bidhaa hizi kutoka nje kutoka Shilingi 700 iliyopendekezwa hadi Shilingi 1,000 na kusamehe kodi za ndani mpaka hali itakavyotengemaa. Serikali ilikubali pendekezo la kuongeza bei ya bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Sura ya 306 Serikali ilileta pendekezo la kuanzisha tozo ya Shilingi 1,000 hadi Shilingi 3,000 kwa vig'amuzi itakayokuwa ikitozwa kupitia malipo ya vifurushi. Hata, hivyo baada ya majadiliano ya kina illonekana kwamba kiwango hiccho ni kikubwa. Hivyo Kamati ilipendekeza kuanza kutoza kati ya Shilingi 500 hadi Shilingi 2,000. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati kama inavyoonekana kwenya Jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Sura ya 414, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Sura 413, Sheria ya Usalama Mahala pa Kazi Sura ya 297, Sheria ya Sekta ya Maziwa Sura 262 na Sheria ya Mbolea Sura ya 378. Marekebisheso yanayofanyika katika Sheria hizi yana lengo la kuondoa muingiliano wa kupanga viwango vya ubora baina ya Shirika la Viwango nchini (*TBS*) na Mamlaka ambazo ama zinasimamia au kutekeleza jukumu sanjari na hilo. Kamati imechambua mapendekezo na kubainisha masuala yafuatayo:-

(i) Mamlaka hizo zina uzoefu wa muda mrefu katika kusimamia sekta husika hivyo mabadiliko yanayopendekezwa yataondoa majukumu yao ya msingi;

(ii) Mapendekezo hayo yanaondoa dhana na umuhimu wa uwepo wa baadhi ya Taasisi za Umma zinazosimamiwa na sheria hizo; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iii) *TBS* ilivyo hivi sasa haina uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali watu kutekeleza majukumu iliyonayo kwenye Sheria yake hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la maboresho haya ni kuondoa muingiliano wa Taasisi za Umma katika kusimamia biashara na wafanyabiashara. Kamati ilitoa ushauri ufuataao kwa Serikali:-

(i) *TBS* kwa kushirikiana na Mamlaka husika wahishe viwango ili visitofautiane; na

(ii) Baada ya viwango kuhuishwa na *TBS*kila Mamlaka itawajibika kuvifuata na jukumu la *TBS* litakuwa ni kuhakiki tu endapo viwango vinafuatwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea ushauri wa Kamati na mabadiliko yamefanyika kupitia jedwali la marekebishao la Serikali. Vilevile, Kamati inashauri kwamba pale ambapo Mamlaka husika inapotoa leseni ya kuthibitisha ubora basi *TBS* isilazimike kutoa leseni nyingine na badala yake ifanye uhakiki kupitia mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mauzo nje ya Nchi Sura ya 196. Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutoza asilimia 30 ya *FOB* au Dola za Marekani 150 kwa tani kwa chuma chakavu kinachosafirishwa nje ya nchi. Lengo la mapendekezo hayo ni kuhakikisha kwamba viwanda vyatatu vinavyotumia malighafi hiyo inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Magari ya Kigeni, Sura 84; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka kiwango linganifu cha kutoza magari ya kigeni yanapopita nchini cha Dola za Marekani 10 kwa kila kilometra 100 ili kiendane na nchi za *SADC*. Hata hivyo uchambuzi wa kamati umebaini kwamba baadhi ya nchi za *SADC* zinatoza tozo nyingine ambazo Tanzania haitozi. Mfano, kuna tozo inaitwa *Park Fee* ambapo malori ya Tanzania yatatozwa kiasi cha dola za marekani 100 kila yaingiapo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika nchi husika. Kuna tozo ya uchafuzi wa Mazingira yaani *carbon emission fee* ambayo hutozwa kwa kiasi cha dola za marekani 60 kwa mwaka na kuna tozo ya *toll gate* ya kiasi cha dola za marekani 100 ambayo hutozwa mara tu baada ya lori kufika kwenye mpaka wa nchi husika.

Mheshimiwa Spika, katika misingi ya kutenda sawa sawa na unavyotendewa na mwenzako, tunaishauri Serikali kuanzisha tozo hizo ili malori ya nchi jirani yanapokuja nchini nayo yaweze kulipa tozo hiyo. Hatua hii ikichukuliwa inawezekana nchi jirani wakaacha kutoza tozo hizo au kutoza kwa viwango sawa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali, Sura ya 134; Kamati imechambua mapendekezo ya Serikali na kubaini yana malengo makuu mawili:-

- (i) Kuwianisha viashiria vyatupimaji wa uhimilivu wa deni ili viendane na viashiria vyakimataifa; na
- (ii) Kubainisha timu ya wataalam ya usimamizi wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba upimaji wa deni kwa uwiano wa mapato ya ndani si kigezo cha kimataifa kamati inaishauri Serikali kuendelea kuangalia uwezekano wa kutumia kigezo hicho ambacho ni muhimu katika ulipaji wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ngozi, Sura 120; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ambayo yana lengo la kudhibiti mauzo ya ngozi zinazohusu nyara za Serikali kama ngozi za wanyama na ambao si nyara za Serikali kama vile ngozi za wanyama wafugwao.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332; mapendekezo ya mabadiliko katika Sheria hii yana malengo makuu yafuatayo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(i)Kupanua wigo wa kodi ya mapato kwa kuanza kutoza kodi ya mpato kwenye biashara za mtandao;

(ii)Kuweka utaratibu wa vivutio vya kikodi kwenye miradi ya kimkakati;

(iii)Kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya awali ya shilingi 20 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli pindi ambapo wauzaji wa jumla wanapowauzia wafanyabiashara ya reje reja;

(iv)Kuanza kutoza kodi ya zuio kwa wamiliki kwa nyumba za kupangisha;

(v)Kuanza kutoza kiwango mfuto cha Shilingi Milioni 3.5 kwa malori yenye *excel* kuanzia tatu na kuendelea pamoja na magari ya abiria kama vile mabasi makubwa na madogo;na

(vi)Kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji (*capital gain tax*) kwa mali pamoja na hisa ambazo Serikali itazipokea ama kuzitoa kwa wabia wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina baina ya Serikali na Kamati yafuatayo yalikubalika:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kusitisha utozaji wa Shilingi 20 kama kodi ya awali kwenye mafuta pindi ambapo wauzaji wa jumla wanapowauzia wafanyabiashara ya rejareja, kwa sababu suala hili lilionekana kuleta mtafaruku katika sekta ya uuzaji wa mafuta nchini pamoja na kuongeza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, pili, kusitisha utozaji wa viwango mfuto kwa malori na badala yake kila lori au basi litozwe kulingana na uwezo wake wa kubeba mizigo na abiria. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho hayo yanaonekana kwenye jedwali la marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bima, Sura ya 394; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka sharti la lazima la kukatia bima masoko makubwa na majengo makubwa ya biashara ili kulinda mali za wafanyabiashara pindi inapotokea majanga ya moto na majanga mengine. Mabadiliko haya yanafuatia matukio ya hivi karibuni ambapo masoko mengi yameungua nchini na kuacha wafanyabiashara kwenye hali mbaya kwa sababu tu hayakuwa na bima. Aidha, Kamati inasisitiza kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa bima ikiwa ni pamoja na Serikali kuanza kukatia bima mali zake kama vile magari.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi, Sura 113; Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sheria hii ambayo yanaweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa kodi ya ardhi pamoja na utozaji wa adhabu kwa kuchelewa kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kwa mapendekezo ya Serikali ya Mabadiliko katika Sheria hii na kubaini kwamba mabadiliko hayo yanalenga masuala yafuatayo:-

(i) Kupunguza ushuru wa hoteli kwa Halmashauri za Wilaya na Miji kutoka asilimia 10 ya sasa hadi asilimia 5;

(ii) Kuweka utaratibu wa kisheria kutoza ushuru wa mazao na huduma kwa makampuni ambayo yanamiliki mashamba kwa ajili ya uzalishaji wa mazao na yanaongeza thamani ya mazao hayo katika Wilaya husika na makampuni ambayo yanachukua mazao katika Wilaya au Halmashauri moja na kuyaongezea thamani katika Halmashauri nyingine; na

(iii) Kuanzisha utaratibu mpya wa mgawanyo wa asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri ambazo zilikuwa zikigawanywa kwa wanawake asilimia nne, Vijana asilimia nne na Watu wenye Ulemavu asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina kamati ilikubaliana na Serikali kuondoa mapendekezo ya utaratibu mpya wa utozaji wa ushuru wa mazao na huduma na kuondoa mapendekezo ya mgawanyo mpya wa asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri. Mabadiliko hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la Mabadiliko la Serikali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba fedha za kujenga miundombinu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo ziwe zinatengwa kuititia mradi wa kuzisaidia halmashauri ili ziweze kujitegemea kimapato ambao uko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Miji), Sura ya 288; Mabadiliko yaliyofanywa na Serikali katika Sheria hizi yana lengo la kuanzisha Kituo cha Pamoja cha Huduma kwa Wawekezaji na Wafanyabiashara yaani *One stop Centre* kwa ajili ya kutoa huduma kwa wawekezaji katika Halmashauri za Wilaya na Miji.

Lengo lake ni kuondoa usumbufu uliokuwa unawakabili wafanyabiashara na wawekezaji katika Halmashauri za Wilaya na Miji kwa kuzunguka katika ofisi mbalimbali. Kamati ilishauri Serikali na ikakubali kuweka mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutunga kanuni ambazo zitaelekeza namna ya uendeshaji wa vituo hivyo na mabadiliko ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, Sura ya 123; Kamati imekubaliana na mependekezo ya Serikali ya kupunguza kiwango cha mrabaha kwenye makaa ya mawe yanayouzwa kwenye viwanda kwa ajili ya kutumika kama nishati pamoja na kupunguza kiwango cha mrabaha kwa madini ya dhahabu yanayouzwa kwenye viwanda vya uchenjuaji. Mapendekezo haya yatapunguza gharama kwa viwanda vya ndani vinavyotumia makaa ya mawe kwa uzalishaji pamoja na kuhimiza wachimbaji wadogo na wakubwa walipo nchini kutumia viwanda vya ndani kwa ajili ya uchenjuaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Malipo ya Taifa, Sura ya 437; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kupunguza kiwango cha ukomo wa tozo kilichokua kwenye sheria cha Sh.10,000 na kuwa Sh.4,000 sawa na punguzo la asilimia 60. Aidha, Kamati ilikubaliana na Serikali kupanua mawanda ya utozaji wa tozo hii kwa miamala yote ya kieletroniki. Hivi sasa kuna baadhi ya miamala ilikuwa haitozwi na hivyo kukwepa tozo hiyo. Hata hivyo, hatua hii haitahusisha uhamishaji wa mishahara kutoka benki moja kwenda benki nyiningine.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Bandari, Sura ya 166; Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka utaratibu kisheria wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya *Warfage* ambayo ni chanzo cha Mapato ya Mamlaka ya Bandari. Mapendekezo haya yamechelewa kwa sababu utaratibu huu ndivyo ulivyo hivi sasa pamoja na kwamba haukuwa kisheria.

Aidha, Kamati ilipendekeza na Serikali ilikubali kubainisha wazi kwamba fedha hizo ziwekwe kwenye akaunti maalum ilioko Benki kuu kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura ya 38; Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye sheria hii ambayo kimsingi yanatoa fursa kwa Serikali kutoa vivutio vya ziada kwa wawekezaji mahiri kwenye Miradi ya Kimkakati ili kuvutia wawekezaji zaidi kwenye miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano, Tanzania Sura 172; Kamati imefanya upembuzi wa mapendekezo ya Serikali kwenye sheria hii na kubaini kwamba:-

(i) *TCRA* ni mjumbe wa kimataifa wa Taasisi za kimataifa yaani *International Telecommunication Union* na *Universal Postal Union*, hivyo kuondoa jukumu hili ni kwenda kinyume na makubaliano ambayo nchi imeridhia; na

(ii) Vifaa vya TEHAMA vinaweza kuwa na ubora ila visiweze kutumika katika mazingira ya nchi yetu kulingana na miundombinu ya TEHAMA iliyopo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Serikali yanamaanisha kwenda kuondoa majukumu ya msingi ya Mamlaka hiyo. Baada ya mashauriano baina ya Kamati na Serikali, ilikubalika kuondoa sehemu yote ya thelathini ya muswada iliyokuwa inafanya mabadiliko kwenye sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399; Kamati imefanya uchambuzi wa mabadiliko yaliyopendekezwa katika sheria hii na kubaini kwamba inalenga masuala yafuatayo:-

(i) Kufanya marekebisho ya kiuandishi ili kuleta mantiki iliyokusudiwa;

(ii) Kutoa fursa kwa Mjumbe wa Bodi kumteua mtu amwakilishe katika vikao vya Bodi; na

(iii) Kuiruhusu Mamlaka ya Mapato kukusanya ada kwa huduma za kitaalam zinazotolewa na Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kwamba ni vyema sifa za mtu anayemwakilisha mjumbe wa Bodi zibainishwe katika sheria. Jambo hili Serikali ilikubali kama linavyoonekana katika jedwali la marekebisho la Serikali. Aidha, Kamati imekubaliana na pendekezo kwamba ada zinazokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na ushauri wa kitaalam kwenye masuala ya forodha zibaki kwa mamlaka kwa kipindi cha mwaka mmoja ili zitumike kuboresha mifumo ya mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, Sura 415; Kabla sijaeleza mapendekezo ya Serikali katika sheria hii kwanza nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara alioufanya wa kupunguza haki maalum yaani *exclusive mandate* ya uondoshaji wa mizigo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

bandarini kwa bidhaa ambazo Serikali ina maslahi nazo. Mabadiiliko haya yamebakisha haki maalum ya kuondosha mizigo ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, silaha, makinikia na nyara za Serikali tu. Jambo hili limekuwa kilio cha miaka mingi kwa umoja wa Wakala wa Forodha Tanzania. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenganisha jukumu la Usimamizi wa Sekta ya Forodha na Uondoshaji wa mizigo kwa sababu si sahihi kwa *TASAC* kuwa na majukumu yote ya usimamizi na wakati huo huo anafanya shughuli za uwakala wa forodha.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438; Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali katika sheria hii na kubaini kwamba yanagusa masuala yafuatayo:-

(i) Kuanzisha utaratibu wa kusajili watu wote wenye miaka 18 na kuendelea ili kuwapa Namba na Mlipa Kodi;

(ii) Kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwasajili washauri wa masuala ya kodi ili kuondoa vishoka katika tasnia ya kodi;

(iii) Kuyatambua na kuyaandikisha maghala ambayo yanayojiendesha kwa misingi ya uwekezaji na biashara;

(iv) Kuweka masharti ya lazima kwamba popote ambapo mtu atakuwa ama anafanya manunuzi au anauza bidhaa au huduma ni lazima awasilishe namba ya mlipa kodi;

(v) Kuhamisha mamlaka ya kusamehe riba na adhabu kutoka kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato na kuyapeleka kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha; na

(vi) Kuhamisha makosa na adhabu zilizokuwa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147 na kuyaweka kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili Sheria hiyo nayo isimamiwe na Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati ilishauri Serikali kufanya masuala yafuatayo:-

(i) Kuondoa sharti la lazima kwamba popote ambapo mtu atakuwa anafanya manunuzi au kuuza bidhaa ni lazima awasilishe namba ya mlipa kodi kwa sababu jambo hili haliwezekani kwa mazingira yetu;

(ii) Kuacha mamlaka ya Kusamahe riba na adhabu kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyo hivi sasa; na

(iii) Kuyatambua maghala ambayo yameanzishwa kwa misingi ya biashara tu na isihusu maghala pamoja na vihenge ambavyo vinatumika na wakulima kuhifadhi mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho yamefanyika kuitia jedwali la marekebisho ya Serikali. Aidha, nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu habari potofu za kwamba eti Serikali imekusudia kutoza kodi kwa kila mtu aliyefikisha umri wa miaka 18 si za kweli. Lengo la Serikali ni kuwatambua wananchi wote katika mfumo wa kodi ili pindi wapatapo ajira au kuanzisha biashara wasipate tabu ya kutafuta Namba ya Mlipa kodi na badala yake iwe ni kuzuhisha tu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utalii, Sura ya 65; Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapendekezo yaliyokuwa yameletwa kwenye Muswada yalikwisha kufanyika kuitia Sheria Na.5 ya mwaka 2021. Hivyo, Kamati ilikubaliana na Serikali kuyaondoa marekebisho hayo. Hivyo sehemu yote ya 35 ya Muswada imeondolewa kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa hatua zinazopendekezwa na Serikali kuitia Mabadiliko ya Sheria hii na kubaini malengo ya mabadiliko ni:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (i) Kuchochaea uzalishaji wa ndani hasa kwa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi;
- (ii) Kulinda viwanda vya ndani kwa kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa malighafi muhimu;
- (iv) Kupunguza gharama ya bidhaa muhimu kama mafuta ya kula; na
- (iv) Kuzitambua bidhaa na huduma za kidijiti ili zianze kutozwa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauriana na Serikali na Serikali ilikubali kufanya marekebisho kwa baadhi ya maeneo ili yaendane na malengo ya Serikali na wakati huo huo yasiathiri mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hata hivyo, Kamati bado inaishauri Serikali kutokuondoa msamaha wa kodi kwenye ndege za kukodi kwa sababu hatua hii itaongeza gharama kwa watalii wanaotumia ndege hizo na kulifanya Taifa la Tanzania kuonekana la ghali katika utalii kuliko nchi jirani ambazo zina msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani katika ndege za kukodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hii itaathiri sana sekta ya utalii wa anga ambapo katika kipindi cha miaka miwili ndege za kukodi zimepungua kutoka ndege zaidi ya 200 hadi ndege 105 tu. Pamoja na kwamba Serikali imeweeka muda wa mpito wa miezi sita ya utekelezaji wa hatua hii hadi Disemba, 2022, Kamati bado inasisitiza kutoondoa msamaha huo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mafunzo ya Ufundi ya Stadi Sura 82; Serikali ilipendekeza kutoa msamaha wa kutotoza kodi ya Maendeleo ya Ufundi yaani *SDL* kwa waajiri ambao wanatumia wanafunzi kwa muda (*intern students*) ambao wako chini ya Tanzania *Employment Services Agency*. Kamati ilishauri na Serikali ilikubali kupanua wigo wa ahueni ya kutolipa kodi ya *SDL* kwa wanafunzi wa muda watakaokuwa wanatoka katika vyuo vya kati na vyuo vikuu tofauti na pendekexo la Serikali kutoa ahueni hiyo kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanafunzi wa vyuo vikuu pekee. Maboresho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004; Kamati imekuwa ikilieleza Bunge lako mara kwa mara kwamba sheria hii mabadiliko yake hufanywa na Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji na Biashara wa Afrika Mashariki na baadaye kuridhiwa na Bunge la Afrika Mashariki. Hivyo inapoletwa Bungeni na Bunge likakataa kuridhia mabadiliko hayo, kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Mkataba wa Forodha wa Afrika Mashariki (*The East Africa Custom Union Protocol*), Waziri wa Fedha atalazimika kumjulisha Katibu wa Jumuiya ili Tanzania isitekeleze makubaliano ambayo yanaweza kuwa na athari kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalla maeneo yote ambayo yamelalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge na kuitaarifu jumuiya hatua ambazo Tanzania itachukua kulinda viwanda vya ndani. Aidha, ni wakati muafaka wa kuweka suala hili ama kikanuni au kwa Kisheria ambapo itamlazimu Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na baadaye Bunge zima kabla hayajaridhiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa na maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022. Aidha, nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; Mheshimiwa Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ndugu Emmanuel Tutuba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango; Manaibu Makatibu wa Wakuu; Ndugu Onerius

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali pamoja na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndugu Alphayo Kidata pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Kamishna wa Sera Ndugu Elijah Mwandumbywa kwa umahiri wao katika kuielimisha Kamati wakati wote wa uchambuzi wa Muswada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua, Makamu mwenyekiti wa kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa umakini, umahiri wao na uvumilivu wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Naomba majina yao yote yaingie katika kumbukumbu Rasmi za Bunge za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi Nenelwa Mwihambi, *ndc*, pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndugu Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Emmanuel Rhobi, Ndugu Wilfred Akasi pamoja na Bi. Maombi Kakozi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Serikali pamoja na Watendaji wa Serikali, marekebisho tuliyoyafanya hapa yana nia ya kuleta mapato kwa Serikali pamoja na kuboresha usimamizi wa kodi na si fimbo ya kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA
MWAKA 2022 (THE FINANCE BILL, 2022)
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022. Tarehe 17 Juni, 2022, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali ya Muswada huu, na baada ya kuwasilisha Muswada huo, Mheshimiwa Spika ulilagiza Kamati ya Bunge ya Bajeti kuuchambua muswada huo. Aidha, siku hiyo hiyo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe Hamad Hassan Chande (Mb) aliwasilisha Muswada huo mbele ya Kamati kwa niaba ya Serikali.

1.1. Uchambuzi wa Muswada

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa muda wa siku kumi ilifanya vikao kwa ajili ya kuuchambua Muswada huu. Kamati imepitia Muswada huu kifungu kwa kifungu kwa madhumuni ya kuijelimisha maudhui ya kila kifungu na kupendekeza marekebisho katika maeneo ambayo yanahitaji maboresho. Baada ya kujiridhisha na maudhui ya Muswada, Kamati iliitisha Maoni ya Umma *"Public Hearing."* Wadau walioshiriki walitoka katika sekta zifuatazo:- Sekta ya utalii, Sekta ya viwanda, Sekta ya usafiri na usafirishaji, Sekta ya kilimo, Sekta ya habari na mawasiliano na Wauzaji wa mafuta kwa Jumla na reja reja. Aidha, kamati ilipata fursa ya kukutana na Watalaam wa Serikali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Muandishi wa Sheria pamoja na Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali zinazojitegemea.

2.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2022

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unafanya mabadiliko katika sheria 38 zenyet malengo makuu saba kama ifuatavyo:-

- i. Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Business Environment);
- ii. Kupanua wigo wa kodi kwa kuanza kutoza kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani kwa Biashara za Mtandano (Digital Economy);
- iii. Kuboresha usimamizi wa kodi kwa kuondoa mianya ya ukwepajji wa Kodi;
- iv. Kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na kuvilinda viwanda vya ndani;
- v. Kuanzisha utaratibu wa ukusanyaji mrabaha, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya haki miliki za wasanii;
- vi. Kuanzisha utaratibu mpya utakaowezesha utoaji wa vivutio maalum kwa Wawekezaji mahiri; na
- vii. Kuanzisha vituo vya pamoja (One stop Centre) kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kushughuikia masuala ya Biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kamati ilichambua mapendendekezo ya mabadiliko mbalimbali kupitia Sheria zilizoko kwenye muswada ili kujiridhisha endapo yanaakisi malengo yaliyokusudiwa na hayataleta madhara kwenye jamii, biashara na uwekezaji nchini. Hivyo maoni na mapendendekezo ya kamati kuhusu muswada huu kwa kila sheria ni kama ifuatavyo:-

2.1. Sheria ya Benki Kuu Sura 197

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko yanayofanywa kwenye Sheria hii yana lengo la kuungeza wigo wa Serikali kukopa kutoka Benki Kuu kutoka wastani wa asilimia 12.5 ya makusanyo halisi ya mwaka wa fedha uliotangulia na kuwa asilimia 18 ya makusanyo yanayokadiriwa katika mwaka wa fedha unaotekelozwa. Baada ya majadiliano ya kina Kamati ilikubaliana na ongezeko la Serikali kukopa kutoka Benki Kuu hata hivyo kiwango hicho kikokotolewe kutokana na mapato halisi ya mwaka wa fedha uliopita na sio mwaka wa Fedha unaotekelozwa. Hatua hii itaepusha kuwa na mzigo wa deni kubwa endapo mapato ya bajeti ya mwaka inayotekelozwa hayatafikiwa kwa asilimia 100.

2.2. Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara Sura ya 213

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya Serikali katika Sheria hii kwa sababu kimsingi ni mwendelezo wa Mabadiliko yaliyofanyika katika Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ambayo illiridhiwa na Bunge mwezi Februari mwaka huu.

2.3. Sheria ya Korosho, Sura ya 203

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kutenga asilimia 50 ya mapato yanayotokana na ushuru wa mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi ambazo zitapelekwa kwenye mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, Ruzuku na Pembejeo. Rai ya kamati kwa Serikali ni kuhakikisha mfuko huo unatumia fedha hizo kwa malengo yanayokusudiwa na si vinginevyo.

2.4. Sheria ya Makampuni Sura 212

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko yanayofanyika katika Sheria hii yanalenga kuingiza dhana ya mnufaika yaani "*Beneficial owner*" katika sheria ya Makampuni. Aidha, marekebisho hayo ni muendelezo wa marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423 ambayo Bunge lako liliyaridhia mwezi Februari 2022.

2.5. Sheria ya Haki Miliki Sura ya 218

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali kuhusu mabadiliko ya Sheria hii na kubainisha masuala yafuatayo:-

- i. Kuanzisha utaratibu mpya wa ukusanyaji, usimamizi na ugawaji wa mrabaha unaotokana na kazi za sanaa;
- ii. Kuanzisha tozo ya **asilimia 1.5** ya thamani ya kila kifaa kitakachoingizwa nchini kwa ajili ya kuhamishia, kutunzia, kudurufu na kusambaza bidhaa na huduma za sanaa ili kupunguza madhara ya upotevu wa mapato yanayotokana na uharamia wa kazi za wasanii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali, hata hivyo inaendelea kushauri kwamba uanzishwe mfuko maalumu ambapo fedha hizi zitawekwa na kugawiwa. Ikibaki kama ilivyo fedha hizi zitaenda mfuko mkuu na itakuwa vigumu sana kuwafikia walengwa.

2.6. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147

Mheshimiwa Spika, Serikali imekusudia kuanzisha Ushuru wa Bidhaa kwa bidhaa zilizobainishwa katika kichwa 17.04 na 19.05 kwa lengo la kudhibiti madhara ya kiafya yanayoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya Bidhaa hizo. Kamati inapendekeza kutokutoza ushuru kwa bidhaa hizo zinazosalishwa ndani nchi zilizotajwa katika **Heading 17.04** na **Heading 19.05** kwa sababu zifuatazo:-

- i. Kwa bidhaa za pipi na chokuleti zinazosalishwa na viwanda vya ndani, Kamati imebaini kwamba viwanda hivi vina hali mbaya ya uzalishaji kutokana na kupanda kwa bei za malighafi zinazotumika kuzalisha bidhaa hizi;
- ii. Bidhaa hizi ndizo biashara kuu ya wafanyabiashara wadogo waliopo katika maeneo ya stendi kuu za mabasi; na
- iii. Nchijirani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hazitozi kodi hii na kwa sababu tuko kwenye jumuiya moja bidhaa hizi

kutoka nchi jirani zitakuwa na bei nafuu kuliko zinazozalishwa nchini na hivyo kuleta ushindani usio sawa .

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwa Serikali kuongeza ushuru wa bidaa hizi kutoka nje kutoka shilingi 700 iliyopendekezwa hadi 1000 na kusamehe za ndani mpaka hali itakavyotengemaa.Serikali ilikubali pendekezo la kuongeza bei ya bidhaa hizo kutoka nje hata hivyo haikuondoa ushuru wa bidhaa za ndani.

2.7. Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Sura ya 306

Mheshimiwa Spika, Serikali ilileta pendekezo la kuanzisha tozo ya **Shilingi 1000** hadi **Shilingi 3000** kwa vig' amuzi itakayokuwa ikitozwa kupitia malipo ya vifurushi. Hata, hivyo baada ya majadiliano ya kina ilionekana kwamba kiwango hicho ni kikubwa. Hivyo kamati ilipendekeza kuanza kutoza kati ya **shilingi 500** hadi **Shilingi 2000**. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati kama inavyoonekana kwenya Jedwali la marekebisho.

2.8. Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Sura ya 414, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Sura 413, Sheria ya Usalama Mahala pa Kazi Sura ya 297, Sheria ya Sekta ya Maziwa Sura 262 na Sheria ya Mbolea Sura ya 378

Mheshimiwa Spika, Marekebisho yanayofanyika kwenye Sheria hizi yana lengo la kuondoa muingiliano wa kupanga viwango vya ubora baina ya Shirika la Viwango nchini (TBS) na Mamlaka ambazo ama zinasimamia au kutekeleza jukumu sanjari na hilo. Kamati imechambua mapendekezo na kubainisha masuala yafuatayo:-

- i. Mamlaka hizo zina uzoefu wa muda mrefu katika kusimamia sekta husika hivyo mabadiliko yanayopendekezwa yataondoa majukumu yao ya msingi;
- ii. Mapendekezo hayo yanaondoa dhana na umuhimu wa uwepo wa baadhi ya Taasisi za Umma zinazosimamiwa na sheria hizo; na

iii. TBS ilivyo hivi sasa haina uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali watu kutekeleza majukumu iliyonayo kwenye sheria yake hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Kwakuwa lengo la maboresho haya ni kuondoa muingiliano wa Taasisi za Umma katika kusimamia biashara na wafanyabiashara. Kamati ilitoa ushauri ufuatao kwa Serikali:

i. TBS kwa kushirikiana na Mamlaka Husika wahishe Viwango (Harmonize standards) ili zisitofautiane; na

ii. Baada ya Viwango kuhuishwa na TBS kila Mamlaka itawajibika kuvifuata na jukumu la TBS litakuwa ni kuhakiki tu endapo viwango vimefuatwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea ushauri wa kamati na mabadiliko yamefanyika kupitia jedwali la marekebishao la Serikali. Vilevile, Kamati inashauri kwamba pale ambapo Mamlaka husika inapotoa leseni ya kuthibitisha ubora basi TBS isilazimike kutoa leseni nyingine na badala yake ifanye uhakiki kupitia mamlaka husika.

2.9. Sheria ya Mauzo nje ya Nchi Sura ya 196

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuanza kutoza asilimia 30 ya FOB “Free on Board” au Dola za marekani 150 kwa tani kwa chuma chakavu kinachosafirishwa nje ya nchi. Lengo la mapendekezo hayo ni kuhakikisha kwamba viwanda vyta ndani vinavyotumia malighafi hiyo inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu nchini.

2.10. Sheria ya Magari ya Kigeni Sura 84

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka kiwango linganifu cha kutoza magari ya kigeni yanapopita nchini cha Dola za marekani 10 kwa kila kilometer 100 ili kiendane na nchi za SADC. Hata hivyo uchambuzi wa kamati umebaini kwamba baadhi ya nchi za SADC zinatoza tozo nyingine ambazo Tanzania haitozi. Mfano

kuna tozo inaitwa *Park Fee* ambapo malori ya Tanzania yatatozwa kiasi cha dola za marekani 100 kila yaingiapo nchi husika, Kuna tozo ya uchafuzi wa Mazingira "Carbon emmission fee" ambayo hutozwa kwa kiasi cha dola za marekani 60 kwa mwaka na kuna tozo ya *Toll gate* ya kiasi cha dola za marekani 100 ambayo hutozwa mara tu baada ya lori kufika kwenye mpaka wa nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Katika misingi ya "reprocity" yaani kutenda sawa sawa na unavyotendewa na mwenzako . Tunaishauri Serikali kuanzisha tozo hizo ili malori ya nchi jirani yanapokuja nchini nayo yaweze kulipa tozo hiyo. Hatua hii ikichukuliwa inawezekana nchi jirani wakaache kutoza tozo hizo au kutoza kwa viwango sawa.

2.11. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali Sura ya 134

Mheshimiwa Spika,Kamati imechambua mapendekezo ya Serikali na kubaini yana malengo makuu mawili:-

- i. Kuwianisha viashiria vya upimaji wa uhimilivu deni "Debt Sustainability" ili viendane na viashiria vya kimataifa; na
- ii. Kubainisha timu ya wataalamu ya usimamizi wa deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba upimaji wa deni kwa uwiano wa mapato ya ndani si kigezo cha kimataifa kamati inaishauri Serikali kuendelea kuangalia uwezekano wa kutumia kigezo hicho ambacho ni muhimu katika ulipaji wa deni la Serikali.

2.12. Sheria ya Ngozi Sura ya 120

Mheshimiwa Spika, kamati inakubaliana na mependekezo ya Serikali ambayo yana lengo la kudhibiti mauzo ya ngozi zinazohusu nyara za Serikali kama ngozi za wanyama na ambaio sio nyara za Serikali kama vile Ngozi za wanyama wafugwao

2.13. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332;

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya mabadiliko katika Sheria hii yana malengo makuu yafuatayo:-

- i. Kupanua wigo wa kodi ya mapato kwa Kuanza kutoza kodi ya Mapato kwenye biashara za mtandao;
- ii. Kuweka utaratibu wa vivutio vyta kikodi kwenye miradi ya kimkakati;
- iii. Kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya awali ya shilingi 20 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli pindi ambapo wauzaji wa jumla wanapowauzia wafanyabiashara ya reje reja;
- iv. Kuanza kutoza kodi ya zui o kwa wamiliki kwa nyumba za kupangisha;
- v. Kuanza kutoka kiwango mfuto cha **Shilingi milioni 3.5** kwa malori yenye *exe/* kuanzia tatu na kuendelea pamoja na magari ya abiria kama vile mabasi makubwa na madogo;na
- vi. Kusamehe kodi ya ongezeko la mtaji "*Capital gain tax*" kwa mali pamoja na hisa ambazo Serikali itazipokea ama kuzitoa kwa wabia wake.

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano ya kina baina ya Serikali na Kamati yafuatayo yalikubalika. Kwanza ni kusitisha utozaji wa shilingi 20 kama kodi ya awali kwenye mafuta pindi ambapo wauzaji wa jumla wanapowauzia wafanyabiashara ya rejareja kwa sababu suala hilli lilionekana kuleta mtafaruku katika sekta ya uu zaji wa mafuta nchini pamoja na kuongeza gharama za uendeshaji. Pili kusitisha utozaji wa viwango mfuto kwa malori na badala yake kila lori au basi litozwe kulingana na uwezo wake wa kubeba mizigo na abiria. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na marekebisho hayo yanaonekana kwenye jedwali la marekebishi la Serikali.

2.14. Sheria ya Bima Sura ya 394

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka sharti la lazima la kukatia Bima masoko makubwa na majengo makubwa ya biashara ili kulinda mali za wafanyabiashara pindi inapotokea majanga ya moto na majanga mengine. Mabadiliko haya yanafuatia matukio ya hivi karibuni ambapo masoko mengi yameungua nchini na kuacha wafanyabiashara kwenye hali mbaya kwa sababu tu ya kutokuwa na bima. Aidha, kamati inasisisitiza kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa bima ikiwa ni pamoja na Serikali kuanza kukatia Bima mali zake kama vile magari.

2.15. Sheria ya Ardhi Sura ta 113

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali katika sheria hii ambayo yanaweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa kodi ya ardhi pamoja na utozaji wa adhabu kwa kuchelewa kulipa kodi hiyo.

2.16. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kwa mapendekezo ya Serikali ya Mabadiliko katika Sheria hii na kubaini kwamba mabadiliko hayo yanalenga masuala yafuatayo:-

- i. Kupunguza ushuru wa hotel “*Hotel Levy*” Kwa Halmashauri za Wilaya na Miji kutoka **asilimia 10** ya sasa hadi **asilimia 5**;
- ii. Kuweka utaratibu wa kisheria kutoza ushuru wa mazao na huduma kwa makampuni ambayo yanamiliki mashamba kwa ajili ya uzalishaji wa mazao na yanaongeza thamani ya mazao hayo katika Wilaya husika na makampuni ambayo yanachukua mazao katika Wilaya au Halmashauri moja na kuyaongeza thamani katika Halmashauri nyingine; na
- iii. Kuanzisha utaratibu mpya wa mgawanyo wa **asilimia 10** za Mapato ya ndani ya Halmashauri ambazo zilikuwa

zikigawanywa kwa wanawake asilimia 4, Vijana Asilimia 4 na Watu wenyewe Ulemavu asilimia 2.

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano ya Kina kamati ilikubaliana na Serikali kuondoa mapendekezo ya utaratibu mpya wa utozaji wa ushuru wa mazao na huduma na kuondoa mapendekezo ya mgawanyo mpya wa asilimia 10 za mapato ya ndani ya Halmashauri. Mabadiliko hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la Mabadiliko la Serikali. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba fedha za kujenga miundombinu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo ziwe zinatengwa kuititia mradi wa kuzisaidia Halmashauri ili ziweze kujitegemea kimapato ambao uko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango.

2.17. Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Wilaya) Sura ya 287 na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Miji) Sura ya 288

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko yaliyofanywa na Serikali katika Sheria hizi yana lengo la kuanzisha kituo cha Pamoja cha Huduma kwa wawekezaji na wafanyabiashara "One stop Centre" kwa ajili ya kutoa huduma kwawawekezaji katika Halmashauri za Wilaya na Miji. Lengo lake ni kuondoa usumbufu uliokuwa unawakabili wafanyabiashara na wawekezaji katika Halmashauri za Wilaya na Miji kwa kuzunguka katika Ofisi mbalimbali. Kamati illishauri Serikali na ikakubali kuweka mamlaka kwa Waziri mwenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutunga kanuni ambazo zitaelekeza namna ya uendeshaji wa vituo hivyo na mabadiliko ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la mabadiliko.

2.18. Sheria ya Madini Sura ya 123

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mependekezo ya Serikali ya kupunguza kiwango cha mrabaha kwenye makaa ya mawe yanayouzwa kwenye viwanda kwa ajili ya kutumika kama nishati pamoja na kupunguza kiwango cha mrabaha kwa madini ya dhahabu yanayouzwa kwenye

viwanda vya uchenjuaji "Refinery". Mapendekezo haya yanapunguza gharama kwa viwanda vya ndani vinavyotumia makaa ya mawe kwa uzalishaji pamoja na kuhimiza wachimbaji wadogo na wakubwa waliopo nchini kutumia viwanda vya ndani kwa ajili ya uchenjuaji wa dhahabu.

2.19. Sheria ya Malipo ya Taifa Sura ya 437

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kupunguza kiwango cha ukomo wa tozo kilichokuwa kwenye sheria cha **shilingi 10,000** na kuwa **shilingi 4,000** sawa na punguzo la **asilimia 60**.

Aidha, kamati ilikubaliana na Serikali kupanua mawanda ya utozaji wa tozo hii kwa miamala yote ya kieletroniki. Hivi sasa kuna baadhi ya miamala ilikuwa haitozwi na hivyo kukwepa tozo hii. Hata hivyo, hatua hii haitahusisha uhamishaji wa mishahara kutoka benki moja kwenda benki nyingine.

2.20. Sheria ya Mamlaka ya Bandari Sura ya 166

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuweka utaratibu kisheria wa Mamlaka ya Mapato kukusanya "Warfage" ambayo ni chanzo cha Mapato ya Mamlaka ya Bandari. Mapendekezo haya yamechelewa kwa sababu utaratibu huu ndivyo ulivyo hivi sasa pamoja na kwamba haukuwa kisheria. Aidha, kamati ilipendekeza na Serikali ilikubali kubainisha wazi kwamba fedha hizo zitawekwa kwenye akaunti maalumu iliyoko Benki kuu kama ilivyo hivi sasa.

2.21. Sheria ya Uwekezaji Tanzania Sura ya 38

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kwenye Sheria hii ambayo kimsingi yanatoa fursa kwa Serikali kutoa vivutio vya ziada kwa wawekezaji mahiri kwenye miradi ya Kimkakati ili kuvutia wawekezaji Zaidi kwenye miradi mikubwa.

2.22. Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Sura ya 172

Mheshimiwa Spika, kamati imefanya upembuzi wa mapendekezo ya Serikali kwenye sheria hii na kubaini kwamba:-

- i. TCRA ni mjambe wa kimataifa wa Taasisi za kimataifa za *International Telecommunication Union (ITU)* na *Universal Postal Union (UPU)* hivyo kuondoa jukumu hili ni kwenda kinyume na makubaliano ambayo nchi imeridhia; na
- ii. Vifaa vya Tehama vinaweza kuwa na ubora ila visiweze kutumika katika mazingira ya nchi yetu kulingana na miundombinu ya tehama iliyopo.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya ya Serikali yanamaanisha kwenda kuondoa majukumu ya msingi ya Mamlaka hiyo. Baada ya mashauriano baina ya Kamati na Serikali, ilikubalika kuondoa sehemu yote ya thelathini ya muswada iliyokuwa inafanya mabadiliko kwenye sheria hiyo.

2.23. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura ya 399

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mabadiliko yaliyopendekezwa katika Sheria hii na kubaini kwamba inalenga masuala yafuatayo:-

- i. kufanya marekebisho ya kiuandishi ili kuleta mantiki iliyokusudiwa;
- ii. Kutoa fursa kwa mjambe wa Bodi kumteua mtu amuwakilishe katika vikao vya Bodi; na
- iii. Kuiruhusu Mamlaka ya Mapato kukusanya ada kwa huduma za kitaalamu zinazotolewa na Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, kamati iliishauri Serikali kwamba ni vyema sifa za mtu anayemuwakilisha mjambe wa Bodi zibainishwe katika Sheria. Jambo hili Serikali ilikubali kama linavyoonekana

katika jedwali la marekebisho la Serikali. Aidha, kamati imekubaliana na pendekezo kwamba ada zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato kutokana na ushauri wa kitaalamu kwenye masuala ya forodha zibaki kwa mamlaka kwa kipindi cha mwaka mmoja ili zitumike kuboresha mifumo ya mamlaka hiyo.

2.24. Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania Sura ya 415

Mheshimiwa Spika, Kabla sijaeleza mapendekezo ya Serikali katika Sheria hii kwanza Nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa busara alioufanya wa kupunguza Haki maalumu “*exclusive mandate*” ya uondoshaji wa mizigo bandarini kwa bidhaa ambazo Serikali ina maslahi nazo. Mabadiliko haya yamebakisha haki maalumu ya kuondosha mizigo ifuatayo silaha, maknikia na nyara za Serikali tu. Jambo hilli imekuwa kilio cha miaka mingi kwa umoja wa Wakala wa Forodha Tanzania. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenganisha jukumu la Usimamizi wa Sekta ya Forodha na Uondoshaji wa mizigo kwa sababu si sahihi kwa TASAC kuwa na majukumu yote ya usimamzi na wakati huo huo anafanya shughuli za uwakala wa forodha.

2.25. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438;

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali katika sheria hii na kubaini kwamba yanagusa masuala yafuatayo:-

- i. Kuanzisha utaratibu wa kusajili watu wote wenyewe miaka 18 na kuendelea ili kuwapa Namba na Mlipa Kodi “*TIN-Tax Identification Number*”;
- ii. Kuweka utaratibu wa kuwatambua na kuwasajili washauri wa masuala ya kodi ili kuondoa vishoka katika tasnia ya kodi;
- iii. Kuyatambua na kuyaandikisha maghala ambayo yanajidesha kwa misingi ya uwekezaji na biashara;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- iv. Kuweka masharti ya lazima kwamba popote ambapo mtu atakuwa ama anafanya manunuzi au anauza bidhaa au huduma ni lazima awasilishe namba ya mlipa kodi;
- v. Kuhamisha mamlaka ya kusamehe riba na adhabu kutoka kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato na kuyapeleka kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha; na
- vi. Kuhamisha makosa na adhabu zilizokuwa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147 na kuyaweka kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi ili Sheria hiyo nayo isimamiwe na Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya majadiliano ya kina kamati ilishauri Serikali kufanya masuala yafuatayo:-

- i. Kuondoa sharti la lazima kwamba popote ambapo mtu atakuwa anafanya manunuzi au kuuza bidhaa ni lazima awasilishe namba ya mlipa kodi kwa sababu jambo hili haliwezekani kwa mazingira yetu;
- ii. Kuacha mamlaka ya Kusamahe riba na adhabu kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyo hivi sasa; na
- iii. Kuyatambua maghala ambayo yameanzishwa kwa misingi ya biashara tu na isihusu maghala pamoja na vihenge ambavyo vinatumika na wakulima kuhifadhi mazao yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubali mapendekezo ya kamati na marekebisho yamefanyika kuititia jedwali la marekebisho ya Serikali. Aidha, nipende kulihakikishia Bunge lako Tulkufu habari potofu za kwamba eti Serikali imekusudia kutoza kodi kwa kila mtu aliyefikisha umri wa miaka 18 si za kweli. Lengo la Serikali ni kuwatambua wananchi wote katika mfumo wa kodi ili pindi wapatapo ajira ama kuanzisha biashara wasipate tabu ya kutafuta Namba ya Mlipa kodi na badala yake iwe ni kuziuuhisha tu.

2.26. Sheria ya Utalii Sura ya 65

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapendekezo yaliyokuwa yameletwa kwenye muswada yalikwisha kufanyika kuititia Sheria na 5 ya mwaka 2021. Hivyo, kamati ilikubaliana na Serikali kuyaondoa marekebisho hayo. Hivyo sehemu yote ya 35 ya Muswada imeondolewa kama inavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho la Serikali

2.27. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa hatua zinazopendekezwa na Serikali kuititia Mabadiliko ya Sheria hii na kubaini malengo ya mabadiliko ni:-

- i. Kuchochea uzalishaji wa ndani hasa kwa sekta ya Kilimo, mifugo na uvuvi,
- ii. Kulinda viwanda vya ndani kwa kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa malighafi muhimu;
- iii. Kupunguza gharama ya bidhaa muhimu kama mafuta ya kula; na
- iv. Kuzitambua bidhaa na huduma za kidijiti ili zianze kutozwa kodi hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauriana na Serikali na Serikali ilikubali kufanya marekebisho kwa baadhi ya maeneo ili yaendane na malengo ya Serikali na wakati huo huo yasiathiri mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hata hivyo, Kamati bado inaishauri Serikali kutokuondoa msamaha wa Kodi kwenye Ndege za kukodi kwa sababu hatua hii itaongeza gharama kwa watalii wanaotumia ndege hizo na kulifanya Taifa la Tanzania kuonekana la ghali katika utalii kuliko nchi jirani ambazo zina msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika ndege za kukodi. Aidha, hatua hii itaathiri sana sekta ya Utalii wa anga ambapo katika kipindi cha miaka miwili ndege za kukodi zimepungua kutoka ndege zaidi ya 200 hadi

ndege 105 tu. Pamoja na kwamba Serikali imeweka muda wa mpito wa mizezi 6 wa utakelezaji wa hatua hii hadi Disemba 2022 kamati bado inasisitiza kutoondo msamaha huo.

2.28. Sheria ya Mafunzo ya Ufundu ya Stadi Sura 82

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipendekeza kutoa msamaha wa kutotoza kodi ya Maendeleo ya Ufundu “*SDL-Skills Development Levy*” kwa waajiri ambalo wanatumia wanafunzi kwa muda “*Intern students*” ambao wako chini ya Tanzania Employment Services Agency (TaESA). Kamati iliishauri na Serikali ilikubali kupanua wigo wa ahueni ya kutolipa kodi ya SDL kwa wanafunzi wa muda watakaokuwa wanatoka katika vyuo vya kati na vyuo vikuu tofauti na pendekezo la Serikali kutoa ahueni hiyo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu pekee. Maboresho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la Marekebisho ya Serikali.

2.29. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikilieleza Bunge lako mara kwa mara kwamba Sheria hii mabadiliko yake hufanywa na Mawaziri wa Fedha, Uwekezaji na Biashara wa Afrika Mashariki na baadaye huridhiwa na Bunge la Afrika Mashariki. Hivyo inapoletwa Bungeni na Bunge likakataa kuridhia mabadiliko hayo kwa mujibu wa Ibara ya 36 ya Mkataba wa Forodha wa Afrika Mashariki “The East Africa Custom Union Protocol”, Waziri wa Fedha atalazimika kumjulisha Katibu wa Jumuiya ili Tanzania isitekeleze makubaliano ambayo yanaweza kuwa na athari kwa uchumi wetu. Kamati inaishauri Serikali kuangalia maeneo yote ambayo yamelalamikiwa na waheshimiwa wabunge na kuitaarifu jumuiya hatua ambazo Tanzania itachukua kulinda viwanda vya ndani. Aidha, ni wakati muafaka wa kuweka suala hili ama kikanuni au kwa Kisheria ambapo itamlazimu Waziri wa Fedha na Mipango kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti na baadae

Bunge zima kabla hayajaridhiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

3.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson, (Mb) kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022. Aidha napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchomba (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Jaji. Eliezer Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ndg Emmanuel Tutuba Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Manaibu Makatibu wa Wakuu, Ndugu Onerius Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali pamoja na Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndg. Alphayo Kidata pamoja na wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Kamishna wa Sera Ndg. Elijah Mwandumbywa kwa umahiri wao katika kuielimisha kamati wakati wote wa uchambuzi wa muswada.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mhe. Omari Kigua Makamu mwenyekiti wa kamati pamoja na Wajumbe wa kamati ya Bunge ya Bajeti kwa umakini, umahiri na uvumilivu wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada huu, hasa ukizingatia kwamba muda haukuwa rafiki sana. Wajumbe hao ni:

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalo, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Dkt Charles Kimei, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Mjumbe
23. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge Bi Nenelwa Mwihambi *ndc* pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Emmanuel F.B.Rhobi, Ndg. Wilfred Akasi pamoja na Bi. Maombi Kakozi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati. Nitoe rai kwa Serikali pamoja na Watendaji wa Serikali marekebisho tuliyoyafanya hapa yana nia ya kuleta mapato kwa Serikali pamoja na kuboresha usimamizi wa kodi na sio fimbo ya kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Daniel Baran Sillo (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

27 Juni, 2022

SPIKA: Mwenyekiti tunakushukuru sana. Ahsante sana kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge tumeshasikia upande wa Serikali, tumeshasikia upande wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na sasa tutaendelea na uchangiaji; ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba fursa ya kuchangia, lakini kabla yao nilete tangazo kwenu kutoka *TWPG*, hili tangazo ngoja nisimame.

Waheshimiwa Wabunge tangazo kutoka kwa Katibu wa *TWPG*, Mheshimiwa Agnes Hokororo, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mara baada ya kuahirisha Bunge saa saba mchana mnaalikwa kwenye hafla ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji mzuri wa bajeti ya mwaka 2021/2022 na mengine yatajitekeza huko ya bajeti 2022/2023. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kwenye hafla hii na hafla hii itafanyika katika Ukumbi wa PSSSF zamani *LAPF* Makole Dodoma. Wabunge wote mnakaribishwa na jambo hili ni hafla ya kumpongeza Mheshimiwa Rais yaani Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo mnakaribishwa Wabunge wote wanawake na wanaume. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye Muswada huu wa Sheria ya Fedha. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu, ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa. Nianze kwa kusema kwamba mimi pia ni mijumbe wa Kamati ya Bajeti, kwa hiyo sitakuwa na mengi sana isipokuwa nitakazia mawili au matatu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa namna ambavyo umeendesha Bunge hili kwa kipindi hiki cha bajeti na kwa namna ambavyo umetuelekeza vizuri na kutulea hasa sisi ambao ni wapya kwenye Bunge hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa sababu naamini wote tumesikia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti namna ambavyo Waziri wetu Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, kwa namna ambavyo alikuwa *flexible* na kukubali na kuwa tayari kurekebisha kama vile alivyoshauriwa na watalaan wake lakini pamoja na kamati yetu.

Tunamshukuru sana kwamba kweli ameonyesha uelewa na naamini kwamba uelewa huu na utayari huo umetokana pia na Rais mwenyewe kukubali marekebisho haya yafanyike kwa sababu tunaelewa kwamba bajeti hii Rais ameweka mkono wake kwa nguvu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba pia nilipokuwa nachangia kwenye hotuba ya bajeti nilianza kusema kwamba Wizara ya Fedha imekuja na nadharia ambayo kweli ni bunifu kuelewa kwamba kuongeza kodi siyo njia pekee ya kuongeza mapato ya Serikali. Nadharia nzima ya *Tax Calendar, calendar* ya kodi inaendana na ukweli huo kwamba ukishaweka tozo kwenye kiwango fulani kikakaa kwa muda fulani kwa sababu kile kianzio kinakuwa kwa matumizi ya kile kianzio kuongezeka mwaka hadi mwaka namna ambavyo pato la Taifa linatarajiwa lionezeke *in nominal term* kwa bei za sokoni, basi utakuta kwamba na wewe hivyo hivyo utakuwa unaongeza mapato yako bila kugusa kile chanzo.

Mheshimiwa Spika, kile chanzo kinakua kwa sababu ya *confidence* ya watu kuamini kwamba wanaweza wakaweka hesabu zao sawa sawa kwa sababu hakutakuwa na mabadiliko makubwa na pia wawekezaji kuongezeka kwenye eneo husika. Kwa mantiki hiyo, naamini kwamba tataanza kuona sasa kwa sababu bajeti hii haikuwa ya kuongeza kodi zaidi, ni bajeti ya kuboresha na kuweka mazingira ya wawekezaji kuona kwamba uchumi wetu unatabirika kisera, hasa Sera ya Bajeti ndiyo muhimu sana kwa upande huu, basi naamini kwamba uzalishaji utaongezeka na hivyo tutaweza kupata kodi kwa wingi zaidi, mapato ya Serikali yataongezeka kwa wingi zaidi sokoni na

hivyo tutaweza kufikia malengo ya matumizi ambayo Serikali imojiwekea.

Mheshimiwa Spika, cha msingi kingine ambacho kimejitokeza hapa ni rekebisho lilitopendekezwa kwenye Sheria ya Benki Kuu. Pendekazo hili limeongeza uwezo wa Serikali kukopa hapa ndani. Unafahamu kwamba mikopo ya Serikali inapoongezeka hapa ndani, kwanza uhimilivu wa deni la ndani siyo changamoto kama uhimilivu wa deni la nje. Uhimilivu wa deni la nje una changamoto ya kubadilika badilika kwa thamani ya fedha yetu. Unakuta kwamba nchi zote ambazo zinakopa ndani; na hata tunapokokotoa, kama tungekuwa tumekopa ndani kwa asilimia 100 hatungekuwa na tatizo lolote la uhimilivu kwa sababu tunajua kwamba hilo linalipika. Unaweza ukaamua hata kuchapisha hela ukalipa. Ndiyo maana nasema hilo la nje ndiyo changamoto.

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu nasema kwamba kusema kweli hii nadharia na pendekazo lilitotoka kwenye Wizara yetu kwamba tubadilishe, tuongeze uwezo ule. Wakati ambapo pia utulivu wa uchumi mkubwa kwa upande wa mfumuko wa bei kwa muda mrefu umekuwa vizuri; *inflation* iko chini sana. Naamini kwamba hii itaenda kuchochaea ongezeko la ukwasi kwenye uchumi na pia uwekezaji na pia inaweza ikapunguza kwa kiwango kikubwa ule ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama tunavyojua mtiririko wa mapato ya Serikali na matumizi ni tofauti. Sasa unapoipa Serikali mwanya kidogo wa kukopa fedha hata zile za muda mfupi illi itumie huku ikitusanya na kurejesha, basi hiyo inasaidia pia miradi ile ambayo tunapelekewa kwenye maeneo yetu iweze kutekelezwa ndani ya wakati badala ya kusubiri kwamba mwishoni mwa mwaka ndiyo tunaanza kuona fedha nydingi inapelekwa kule. Kwa hiyo, naamini na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha kwa kuliletta hilo.

Mheshimiwa Spika, ili uone kwa namna gani Serikali imejipanga kwa wale wengine ambao sisi tulichambua sana

tumekutana na wadau wengi sana na tumechambua sana kwenye Kamati, na ninaweza nikawahakikishia Watanzania wenzangu kwamba bejeti ya wakati huu ni tofauti na itakuja kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kero zote au maoni yote yaliyowasilishwa na wadau yamezingatiwa na niseme kwamba, naamini sasa hivi kuna watu wengi wanafurahia na wanachekelea hususan suala zima la *TASAC* limepata ufumbuzi. Pale kwenye bandari yetu kwa mfano, Bandari ya Dar es Salaam siku zote imebaki ikilalamikiwa kwa kukosa ufanisi kwa sababu ya uwepo wa siyo tu tozo za *TASAC*, lakini pia ukiritimba ambao uliingizwa kwenye uondoaji wa mizigo kwenye bandari yetu kutokana na uwepo wa shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, ni shirika zuri, lakini kwa vile ye ye ni msimamizi, na tunaamini wazi kwamba ni vizuri ile biashara nyingine ambayo siyo nyeti, maana ile nyeti wamebakiziwa, lakini ile biashara ya mizigo ya kawaida iwe *handled* na *Clearing and Forwarding Agency* wengine.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nipongeze kwamba katika suala zima la *Charter Flights*, tunamshukuru Waziri alikaanalo sana, lakini baadaye alikubali kwamba lisitishwe kidogo, lisogezwe *applicability*yake iwe ni miezi sita ijayo.

Mheshimiwa Spika, pia bado naamini kwamba kusema kweli kwa namna ambavyo tunakimbizana na *Royal Tour* na utalii kuwa ni sekta muhimu sana, naamini kwamba ili tuweze kushindana na wenzetu majirani ambao wao wamekwenda mbali na walikuwa wameshika nafasi kubwa katika soko hili la utalii, inaweza pengine baadaye Waziri akaja akaridhia kwamba tuendeleze hata kwa mwaka mzima tusiweke VAT kwenye *Charter Flights Services* ili wale watalii wanaokuja na kukaa kwa muda mrefu zaidi nchini kufanya *hunting* (kuwindia) nasikia wanakaa mpaka siku 21, wale wengine wanaokuja, wale wadogo wadogo wenzangu, wanakaa siku nne sana sana *on average*.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa wanaokuja wanakaa muda mrefu wakachukua *Charter Flights* zetu kwa bei ambayo haina VAT, tutaona kwamba matunda ya *Royal Tour* tunayozungumza yataonekana kwa uharaka na kwa ukubwa zaidi.

Kwa hiyo, naendelea kusihu Serikali iangalie hili kwa sababu sekta imeanza kufunguka na sisi tumeanza kuona matunda ya *Royal Tour* na tumeweza kuona kila mtu anafaidi kwenye mnyororo mzima wa sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba Waziri aendelee kuliangalia. Namshukuru sana kwamba amekubali lisogezwe lakini naamini kwamba baadaye atakavyozidi kuona mapato yanaongezeka kutoka vyanzo vingine vyaa sekta hii, basi atalisitisha kabisa mpaka pengine baada ya mwaka mmoja au miwilli. Aliwekee kalenda ndefu zaidi, kalenda ya miezi sita haitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge...

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kimei, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kwagilwa.

TAARIFA

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nimpe taarifa mzungumzaji kwamba baada ya ile shughuli ya Mheshimiwa Rais ya *Royal Tour* takwimu zimebadilika sana. Mwaka 2021 mwezi kama huu tulikuwa na watalii 43,966. Hivi tunavyozungumza tuna watalii 79,405. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni kwamba watalii hawa 79,000 wakiwemo wawindaji, wengi wao wanatumia ndege zetu hizi. Tukichaji VAT tutawa-*discourage* kuja. Tujitahidi sana tui-wave outhii VATkwenye ndege ili waweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuja kwa wingi. Kwa sababu tusipofanya hivyo watatumia ndege nyingine kwa mataifa mengine kwenda sehemu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili taarifa ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, ni taarifa nzuri na hizo takwimu ni sahihi na ninaamini kwamba zitazidi kuongezeka kwa sababu kasi ni kubwa sana. Kwa sisi ambao tumepita kwenye hoteli tukafanya *survey* kidogo, tunaambiwa kwamba hoteli zimekuwa *booked* kwa miezi mitatu yote ijayo zimejaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini Mheshimiwa Waziri atapata fedha nyingi zaidi na pia atapunguza uwekezano au umuhimu wa kutoa ruzuku yoyote kwa taasisi hizi ambazo zinashughulika na sekta hiyo kama tulivyotoa miaka iliyopita. Fedha hiyo itaingia kwenye bajeti kwa sababu zile sekta, hoteli na Ngorongoro *Observation Unit* na TANAPA na wenyewe sasa watakuwa wanajitegemea na pia kutoa gawio lao la kutosha kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kushukuru tena, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa fedha ambao Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ametuwasilishia mbele ya Bunge lako Tukufu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wa fedha, madhumuni yake ni kuweka taratibu za kisheria katika hatua zote za kikodi zilizokuwa zimetajwa ndani ya bajeti na kwamba sasa baada ya mjadala, zile hatua za kikodi zinakuja kupewa nguvu ya kisheria na ndiyo maana Muswada huu unakuja mbele yetu ili kubariki sasa zile hatua ambazo zimetajwa ndani ya bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti hii tulijadili kuanzia iliposomwa tarehe 14 hadi tarehe 25, tumefanya mjadala mrefu sana, hatimaye tukaipitisha ile bajeti kwa kishindo kwa asilimia 94. Maana yake ni kwamba hata hizi hatua ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema sasa hivi, tunaziridhia. Kwa sababu hiyo, napenda niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hatua ambazo Mheshimiwa Waziri amezungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waweze kuunga mkono Muswada huu kwa sababu hii ni kazi ambayo naweza nikasema ni kazi iliyotukuka kutengeneza bajeti ambayo haiendi kumwongezea mzigo mwananchi. Naweza nikasema ni mara ya kwanza katika historia ya karibu, bali ni bajeti ambayo inakwenda kupunguza mizigo mingi sana iliyokuwa ikibebwa na wananchi kutohana na tabia tulizokuwa nazo miaka ya nyuma, kwamba bejeti ikija, kodi ya bia itaongezeka, au soda na kadhalika na kadhalika. Hivyo, nampongeza Mheshimiwa Rais sana kwa kazi kubwa ya ubunifu ambayo ameweza kuifanya na ndiyo maana sifa zimekuwa ni nydingi kwamba hii ni bajeti ya kiuchumi na inakwenda kutukomboa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kinafurahisha ni kwamba Muswada huu wa sheria hizi ambao unafanya marekebisho ya sheria hizi 38, ukiusoma vizuri sana utakuta Serikali imekubali maoni ya Wabunge, maoni ya wadau, maoni ya Kamati ya Bajeti kwa zaidi ya asilimia 40. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naweza nikasema ni Serikali sikivu kuwa tayari kurekebisha Muswada wa Fedha kwa kiasi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kikubwa kama hicho. Ukiangalia hata vile vifungu kimoja kimoja, zaidi ya vifungu 50 vimefanyiwa marekebisho ili ku-accommodate ili kuweza kuchukua maoni ya Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, naweza nikasema kwamba hii ni bajeti yetu na sisi Wabunge lazima tuipokee. Samahani, nitatumia neno la Kiingereza, neno la Kiswahili la haraka haraka silioni; *we have to own...*

MBUNGE FULANI: Kumiliki.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: ...tuimiliki iwe yetu sote. Kwa hali hiyo, napenda tu nitoe mifano kama mitatu kuonesha ni kwa jinsi gani bajeti hii inamgusa mwananchi wa kawaida? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuangalie kwenye ile Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290 ambapo Serikali kwanza ilikuja na mawazo, ingependa katika zile asilimia 10, ule mgawanyo wa nne, nne, mbili ubadilike ili asilimia tano ziende kwenye miundombinu ya Wamachinga. Wabunge hapa tukasema hapana, Serikali msilifanye hivyo, msitie mkono katika mgawanyo ule kwa sababu unawagusa wananchi wetu. Serikali ikasema naam, tuwesasikia Wabunge. Sasa hiyo ni heshima kubwa sana ambayo Serikali imetupa sisi Wabunge tunapowatetea wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Mwigulu tulipokuwa kwenye Kamati, yawezekana vilevile Serikali ikafikiria kuboresha zaidi eneo hili na kufanya wananchi wetu waweze kupata mikopo kiurahisi zaidi na kufaidika. Hii ni kazi iliyyotukuka ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mungu ampe busara zaidi ya kuweza kututetea wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiangalia eneo lingine, Serikali ilikuwa imepanga kuweka kodi ya awali ya Shilingi 20/= kwa kila lita ya mafuta. Kazi hii ingepata tafsiri tofauti huko chini huko. Watu wangefikiri kwamba Serikali imeweka tozo mpya

ya Shilingi 20/= kwa kila lita na ingeleta majadiliano ambayo siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya ile Shilingi 20/= ni kuichukua mapema ili Serikali iweze ikapata kama vile Sheria ile ya Kodi ya Mapato mwishoni mwa biashara, kwa kuwa imeleta mikingano, Kamati ilishauri kwamba kodi hii iondolewe. Hii kuondolewa maana yake inaleta unaifuu mwingine kwa wananchi wa Tanzania. Natoa pongezi kubwa sana kwa Serikali kwa kuliangalia eneo hili ili lisileté mtafaruku katika bei za mafuta ya *Petrol* na kutuchanganya kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine mengi ambayo tumeyazungumza yanayohusiana na tozo zile za simu wakati wa kutuma fedha. Mnakumbuka tozo hizi zililetá majadiliano marefu sana lakini Serikali imetusikiliza, imepunguza hata kima, kutoka kima cha juu cha shilingi 10,000 na kuja mpaka kima cha juu sasa kitakuwa shilingi 4,000. Maana yake ni kwamba unaleta unaifuu mkubwa kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, bajeti hii kila ukiiangalia maeneo yale ambayo yanamgusa mwananchi wa kawaida katika maisha yake ya kawaida amepata unaifuu sana. Hii nayo ni kazi ambayo Mwenyezi Mungu amemjalia Mheshimiwa Samia kuweza kumwangalia mwananchi wake wa Tanzania ni kwa namna gani anamwondolea mizigo mizito. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sema tu kuna hizi taratibu za Kibunge kwamba huu Muswada lazima tuujadili na umepewa siku mbili. Laiti kama ningekuwa naruhusiwa kutoa ushauri, ningesema hiki kitu kingeweza kujadiliwa kwa siku moja tu, inatosha. Kwa sababu sisi wenyewe tulikubali ile bajeti na tukakubali hata zile taratibu ambazo Mheshimiwa Mwigulu amezzungumza. Maana yake sasa hivi tunakwenda kutafsiri kisheria na kuzipa nguvu za kisheria. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mifano hii michache niliyoizungumza, hamwoni kwamba ni lazima sasa hivi hii bajeti itakapokuja kuhitimisha, tuihitimishe kwa kishindo kama wakati tunahitimisha bajeti ambayo ilisomwa ya Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napungukiwa na maneno, sina maneno mengi. Naona umeshakipeleka kisemeo. Nataka nikushauri kwamba Wabunge hata ukitupa siku moja hii ingetosha kabisa kuimaliza bajeti hii. Naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyowasilishwa leo juu ya Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi na kukupongeza. Najua tunakaribia kuhitimisha Bunge hili la Bajeti na Muswada huu unakwenda kuhitimisha safari ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2022/2023 kwa namna ambavyo umetuongoza na kwa namna ambavyo umetoa maelekezo mara kwa mara na pia Katibu wa Bunge kwa namna ambavyo pia ametusaidia na Sekretarieti mahiri ya Kamati yetu na Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti na Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wetu wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu hiso kwako na viongozi mbalimbali wa Bunge naomba kipekee nimpongeze sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake, Watendaji Wakuu wa taasisi chini ya Wizara hii na wadau wote ambao walishiriki mjadala huu na kipekee pia Kamishna wa Sera ndani ya Wizara ya Fedha

kwa umahiri wake pamoja na Kamishna wa *TRA* wakati wanatupitisha kwenye vifungu mbalimbali vyta Muswada huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake kwenye Wizara ya Fedha na hata pale aliposema: "*Tumewasikia Wabunge, nimemshauri Waziri atakapoleta marekebisho mbalimbali iendane na ushauri wa Wabunge ndani ya Bunge.*" Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naamini pia maoni yangu ni machache kwa sababu tumeshiriki kwa muda mrefu kwenye Kamati, lakini nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo Sura ya 437, Punguzo la ukomo wa juu wa kiwango cha kutuma na kupokea miamala kutoka shilingi 10,000 mpaka shilingi 4,000. Kwa kweli ni ukombozi wa hali ya juu na imelenga kupunguza ukali wa maisha kwa mwananchi wa kawaida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, palikuwa na maneno mengi, lakini Serikali hatua kwa hatua ilipunguza kwenye hatua za awali kwa mwaka 2021, lakini safari hii imekuja na punguzo zaidi ya asilimia 60. Maana yake Serikali imesikiliza, Serikali hii ni sikivu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kipekee nashukuru kwa makusanyo ya tozo kwa ujenzi wa vituo 288 na umaliziaji wa madarasa 560 kwa Mkoa wa Pwani. Nashukuru kwa vituo vya afya tisa, tumepokea shilingi 4,500,000,000. Kipekee nivitaje vituo ambavyo nimevitembelea; Kituo cha Afya Fukayosi, Bagamoyo; Kituo cha Afya Msata, Chalinze; Kituo cha Afya Kongowe, Kibaha; Kituo cha Afya Pangani, Kibaha Mjini; Kituo cha Afya Mjawa, Kibiti; na Kituo cha Afya Ngorongo, Rufiji. Hivi nimevishuhudia katika hatua mbalimbali za ujenzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru Watanzania kwa kodi hii ya uzalendo kwamba imefanikisha kupatikana

kwa vituo vya afya lakini na hatua hii ya kupunguza sasa, Serikali imeleta vyanzo vingine mbadala, naipongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili naomba nishukuru Serikali kwa kukubali maoni yetu kuacha mgawanyo wa fedha hizi za asilimia 10 kwenye sheria 290 ya fedha ya Serikali za Mitaa kwa kweli Serikali nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa ushauri kwenye hili kwamba, kwa yale Majiji na Manispaa Serikali iweke utaratibu ili iweze walau kuendana au kupata soko la aina yake kama lilitu kwa na hapa Dodoma, kwa sababu gharama yake ni kama bilioni 9, kwa hiyo uwezekano wa kupata masoko ya namna hiyo ni mkubwa. Kwa hiyo naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili naomba pia nikubaliane na mapendekezo ya Serikali ya kuongeza kiwango cha mkopo kutoka Benki Kuu, Sura ya 197. ninaipongeza kwa sababu tumeona hata kwenye taarifa za CAG zipo hoja ambazo za tozo za ucheleweshaji wa malipo kwenye ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa mfano kwa ripoti inayoishia mwaka wa fedha Juni 2020 kuliwa na hoja bilioni 14 iliyotokana na ucheleweshaji wa malipo kwa miradi hiyo ambayo inatokana pengine na uchache wa fedha. Kwa hiyo, kifungu hiki maana yake Serikali inaweza sasa ikakopa hizi pesa ndani ya Benki Kuu, ambayo tunajua ni benki ambayo ni *last resort*; kwa upande wa Serikali kwa hiyo itawezesha kupunguza gharama kama hizi.

Mheshimiwa Spika, pia niishukuru Serikali kwa kufanya marekebisho Sheria ya Korosho ya Sura 203 na kurejea ule mgawanyo wa asilimia 50 iende kwenye Mfuko wa Pembejeo ambayo itaenda kwenye Wizara ya Kilimo na asilimia 50 itaenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa niaba ya wakulima wa korosho wa Mikoa Mtwara, Lindi Pwani tunaomba tuishukuru sana Serikali. Tushukuru pia kwa sababu hata kabla ya hatua hii tulipataruzuku ya bilioni 61 na imeongeza uzalishaji wa zao hili la korosho.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nimpongeze kwa kweli kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais Samia Hassan kwa kuridhia kuipunguzia haki mahususi *TASAC*. Kwa kweli amejipambanua ni mtu anayeaminisecta binafsi secta ya wafanyabiashara. Kwa hiyo niwaombe Wakala wa Ushuru wa Forodha Tanzania, yale yaliokuwa yanasemekana makando makando; jambo hili wamelisubiri miaka mingi Mama sasa ameliridhia na hatimaye limekuja hapa. Hatutarajii kusikia makando makando wala kusikia masuala mbalimbali ya *forgery* kwa Wakala wakati wa uondoaji wa mizigo bandarini na mambo mbalimbali. Kwa hiyo naamini watachangia pato la Taifa na masuala ya kulipa kodi,

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba hizi sheria mbalimbali zilizofanyiwa marekebisho pamoja na tozo zilizopunguzwa zitasaidia kuhakikisha kwamba tunapata mapato ya troni 28 kati ya troni 41.48 ambazo tumezipitisha kwa kishindo kwa asilimia 94 ndani Bunge lako Tukufu. Ninaamini kupitia hatua ya Mheshimiwa Rais kutoa kibali ya ajira kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, takribani vijana 1400 watawezesha Mamlaka hii kukusanya kiwango kilichokasimiwa kwao troni 23 kati ya troni 24 kwa mapato ya ndani. Kwa hiyo niwaombe Watanzania tuendelee kutoa ushirikiano wa kulipa kodi kwa wakati, matumizi sahihi ya *EFD* na pia kulipa kodi kwa kadri wanavyokadiliwa.

Mheshimiwa Spika, na mwisho mimi niendelee kushukuru sana, bajeti hii imelenga kupunguza makali ya maisha ya Watanzania. Ni bajeti ya wananchi na ndio maana hata hizi hatua zinazopendekezwa leo ni hatua ambazo ni za kuwezesha secta ya viwanda na secta ya uzalishaji kilimo. Tozo mbalimbali humu zimepunguzwa, ili kuwawezesha Watanzania walipa kodi lakini pia kupanua wigo wa kodi. Tumeona vyanzo ambavyo vimeongezeka, nishukuru sana, hongereni Wizara ya Fedha nawatakia kila la kheri katika kuhakikisha troni 41.48 zinapatikana Mwaka wa Fedha unaoanza tarehe moja mwezi wa saba. Watanzania wenzangu na Mamlaka za Serikali za Mitaa tuendelee kutoa ushirikiano kuhakikisha kodi inapatikana na inatumika kwa kadri ilivyokusudiwa. Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira ajiandae.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe mionganoni mwa Wabunge ambao wanachangia muswada ambao umeletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa; lakini pili naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu wangu wakupitia miswada ya fedha kama hii mswada huu umekuwa wa tofauti kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mswada wa Serikali wa fedha unapokuja badiliko lolote ambalo linafanyika lazima mamlaka itoe idhini. Na kipindi hiki Waziri wa Fedha pamoja na kumpongeza na wasaidizi wake wamekuwa na kazi nyepesi kwa sababu yale ambao walikuwa wana-*propose* walikuwa wanapata *go ahead*; hongereni sana. Inayobaki sasa ni suala la utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nilishauri kwenye Kamati ya Bajeti na leo naomba nishauri maeneo machache kwa kuwa mengi yameboreshwa. Na kama alivyosema Mheshimiwa Tarimba, laiti ingekuwa inawezekana hakika leo ilikuwa tunahitimisha; lakini kwa sababu iko kwenye ratiba naomba tuendelee kuboresha maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, liko suala la utekelezaji na ni suala la *administration*. Naomba Wizara ya Fedha kwa kupitia *TRA*, kuna maeneo machache ambayo ni vizuri mkaenda kuyarekebisha ili wananchi wasione adha kutoka nchi za Jirani. Kwa sisi ambao wilaya zetu zinapakana na nchi jirani ukiongelea maeneo kama Songwe, Kalambo naamini hata ukienda Songea kule kuna bidhaa ambazo zinakuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zinaingia kutoka nchi jirani ambazo hazitokani na ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukiwa kule Tunduma kuna sukari ambayo inaingia kutoka nchi Jirani ya Zambia na nyine inaingia kutoka Malawi. Sasa, mwananchi wa kawaida akikutwa na ile sukari inaonekana kama vile anavunja sheria. Niiombe *TRA*, bidhaa kama za sabuni na bidhaa nyine uwekwe utaratibu wa kuhakikisha tunawaelewsa wafanyabiashara, kwamba bidhaa ikiingia nchi kutoka jirani ni wajibu wa kuhakikisha kwamba inalipiwa kodi na isije ikaonekana kama vile ni bidhaa haramu.

Mheshimiwa Spika, mwananchi akipata sukari kwa bei nafuu hakuna kosa. Wakati mwingine ailingii akilini pale ambapo labda bidhaa imesafiri kilometri nyangi kutoka Nairobi mpaka ije ifike Kalambo kule kwa vyovoyote vile ukiweka gharama za usafirishaji bidhaa hiyo itauzwa kwa bei kubwa. Hayo mengine mwende mkatekeleze wakati unatekeleza sheria hii ya fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo wa jumla naomba niendelee kutoa mchango kidogo katika maeneo ambayo tulijadili kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna rekebisho la Sheria ya Bima jambo, jema sana na naipongeza Serikali. Hata hivyo ni vizuri pale ambapo unatoa ushauri kwa mwezako kwamba akatekeleze anza kutekeleza na wewe. Ni wakati mwafaka Serikali ianze kufirikiria kwamba gari zake zote ikatie bima. Haina afya hata kidogo gari jipya la Serikali linapata ajali halafu Serikali inapata sifuri si jambo lenye afya. Kama ambavyo tunasisitiza wananchi wetu wakatie bima na Serikali vyombo vyake kwa kuanzia na magari; na Mheshimiwa Waziri amesema anaenda kuanza kubana matumizi; sasa kubana matumizi ni pamoja na kuhakikisha kwamba upati hasara jumla. Anzeni kukatia bima magari ya Serikali na tutumie taasisi ya umma, kwa maana ya bima ambayo iko chini ya *N/C*. Hii ndiyo namna pekee na nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba *N/C*inasimama na baadaye inashindana na taasisi

nyingine za bima kwa hiyo anzeni kufikiria kuhakikisha kwamba gari za Serikali zinakatiwa bima.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nipongeze sana, Serikani inakwenda kidijitali hii habari ya kwamba unatarajia maduka ni yale ambayo unayakuta *physically* duniani huko tunahama. Sasa hivi biashara inafanyika kwenye mtandao; na ndiyo maana marekebisho ambayo yameletwa sasa yatawezesha kuhakikisha kwamba kuna kuwa na *water tight* katika maeneo kama hayo. Kwa sbabu leo hii naweza nikatizama kwenye mtandao nikaona bidhaa nikaipenda nikaagiza nikaletewa hapo nilipo. Sasa, Serikali ni wapi ambapo inakutana kuhakikisha kwamba inakusanya tozo ambazo ni stahiki?

Mheshimiwa Spika, kwa sheria hii ambayo inaenda kupita hakika, ninaamini *TCRA* nao watajiongeza ili tuweze kuwa-*track* hawa wote ambao wanafanya biashara bila kulipa kodi stahili kwa Serikali. Niwaombe Serikali mnafanya kazi nzuri ya kuwezesha vijana kujenga mifumo. Tuhakikishe kwamba tunaleta nguvu kubwa sana katika *IT*, hakuna namna ambavyo tunaweza kuendelea kuishi *traditionally*. *It is high time*, mnafanya kazi vizuri, vijana wanakuja na mifumo, muwapeleke wakasome ili wawe *current* na mataifa mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nipongeze; kuna hii sheria ya hati miliki itakayosaidia vijana wetu ambao ni watunga miziki, waigizaji na watu wa filamu kwa ujumla wake. Wamekuwa wakilalamika kwa kipindi kirefu kwamba kumekuwa kuibiwa kwa kazi zao ambazo wamejifanya vizuri. Sasa, kwa muswada huu ambao utapita na kuwa sheria, hakika kwa kuanzisha hii asilimia 1.5 pale ambapo zile bidhaa ambazo zinaingia *quality cd* na vingine vyote hivyo wataweza kupata hiyo na mchanganuo wake ni namna gani inaenda kugawanyika imewekwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwaomba sasa Serikali mhakikishe hichi ambacho kimekuwa kikilalamikiwa kwa muda mrefu sasa hivi tunaenda kutibu hilo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana naunga mkono hoja, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Halima James Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Na mimi kama ambavyo wajumbe wengine wa Kamati ya Bajeti walivyosema nichukuwe nafasi hii kwa kweli kutambua *fixability* ya Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri kwa kuzingatia ushauri wa Wabunge pamoja na kuzingatia mapendekezo ya Kamati, kwa hiyo nitambue huo utayari wenu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, mchango wangu utakuwe kwenye maeneo machache; la kwanza ni ile asilimia kumi ya mapato ya halmashauri, ambayo Serikali walileta mapendekezo ya tano, kwa mantiki ya ujenzi, na 2, 2, 1. Tunashukuru kwamba mmerudihsa katika utaratibu wa awali. Kwamba asilimia 10 ibaki 4, 4, 2, kwa mantiki ya vijana akina mama na wenzetu watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, sasa, pamoja na kupendekeza irejewe na imekubaliwa nadhani Serikali ina wajibu wa kufanya usimamizi ulio thabitii, kwenye fedha hizi ili zikatumike na wakapewe watu wanaostahili ili waweze kufanya marejesho stahiki na ili watu wengine waweze kupata.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tumekuwa *vocal* sana kutetea, na kama ambavyo na mimi ninatetea iendelee kuwepo lakini lazima wananchi wetu tunaowawakilisha wajue fedha hizi zinazotolewa bila riba si zawadi, si sadaka ni kwaajili ya kusaidia kunyanya maisha yao.

Sasa nimesema haya kwa sababu mwaka wa kwanza ambao huu mfuko maendeleo wa vijana na akina mama kuwa *introduces* ilikuwa mwaka 1993, *for the first time*. Mwaka

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2019 ndipo tukafanya marekebisho tena ya hii sheria ili kuweza kufanya huo mgawanyo ambao tume-*propose*.

Mheshimiwa Spika, kwa maana yake ni nini; huu mfuko kwa ujumla wake una umri wa miaka 29. Kwa hiyo, kama sasa tuna mfuko ambao una umri wa mtu mzima lazima tujilize umekuwa na *impact* gani katika kuondoa umaskini na kutengeneza ajira za mtu mmojammoja? Kwa hiyo ni jukumu la Serikali Mheshimiwa pamoja na kwamba tumekubaliana ama amekubaliana na mapendekezo ya Bunge kwenda kufanya tathmini ya kina ili kujuua tumekosea wapi, tumepatia wapi na tutaboresha wapi.

Mheshimiwa Spika, nilibahatika kupitia ripoti ya CAG, kwa sababu ndiyo tunajenga, na tuko na Serikali hapa; kuhusiana na eneo kama hili ripoti ya mwaka huu; inatuambia kwamba katika mwaka huu mmoja wa hesabu 2020/2021 ambayo ametolea taarifa yake Machi mwaka huu; anasema kwamba wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za Serikali za Mitaa hawakurejesha bilioni 47.01. Sasa, tuna Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kati ya hizo 155 kwa dhamira njema ya Bunge na Serikali, hela zinatolewa lakini Mamlaka 155 kuna shida ya marejesho, then kuna tatizo, lazima tukatatue tatizo.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inajumlisha Serikali ya Mtaa kwa mantiki ya kwamba Waziri wa TAMISEMI ana dhamana pamoja na Wakurugenzi wake...

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa inatoka upande gani, simuoni aliyesimama.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, hapa kwa Mheshimiwa Ulenge.

SPIKA: Inabidi uwe umesimama, ukiwa umekaa nakuwa sikuoni, Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge.

TAARIFA

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Halima Mdee kwamba anayoyasema ni sahihi, na suala la kutokurejeshwa mikopo ile ya asilimia 10 ni kwa sababu mwongozo uliotolewa Machi una mapungufu mengi na unapaswa ukarekebishwe. Moja ya pungufu ni kwamba, mwongozo unazungumza marejesho ni makubaliano lakini Wakurugenzi wa Halmashauri kwa sababu ni *annual collection* wanalazimisha mtu amechukuwa Shilingi milioni 10 arudishe ndani ya mwaka mmoja, kitu ambacho hakiwezekani; naomba kumpa taarifa mzungumzaji.

SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee kabla sijakuuliza kama unapokea hiyo taarifa ama upokei; Waheshimiwa Wabunge nillshapata kueleza hapa, niwakumbushe tu yule anayekuwa amechangia usahihi au kutokuwa sahihi kwa mchango wake ye ye huko sahihi kama hauko sahihi basi kuna kanuni zetu kwa hiyo Mheshimiwa ukiacha hiyo sehemu ya usahihi wa mchango wako unaipokea taarifa hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, yah! Ninaikubali kwa sababu ameendelea kuonyesha mapungufu yaliyopo katika huu utaratibu mzima.

Mheshimiwa Spika, na ili Serikali ikafanyie kazi, nimejaribu tu kufanya tathmini ya miaka mitano ili mijue ukubwa wa tatizo. Kwa mfano, tunaambiwa mwaka 2016 na 2017 halmashuri 84 zilishindwa kurudisha bilioni 5.8. Mwaka 2017/2018 halmashauri 90 bilioni 10 zinaongezeka tu. Mwaka 2018/2019 halmashauri 111 bilioni 13.7. Mwaka 2019/2020 halmashuri 130 bilioni 27. Mwaka 2020/2021 halmashuri 155 bilioni 47. Kwa hiyo kwa miaka mitano tumepoteza kodi za Watanzania bilioni 104.

Mheshimiwa Spika, sasa tunasema hivi; lazima kila mmoja atekelze wajibu wake. TAMISEMI asimamie, lakini pia ni muhimu sana ili zoezi lihushe wataalam wa mikopo jamanii! Yaani huko chini tunatoa *billions of money* halafu

wanaoachiwa wasimamie mama maendeleo ya jamii. Tunapenda sana Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa akina baba na akina mama, tunawapenda; lakini kwa sababu dhamira ni kutambua vikundi kwenye maeneo yetu waweke ni pia wataalam wa mikopo ili basi hili jambo liweze kwenda vyema na kila mmoja aweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa miaka mitano tumepoteza kodi za Watanzania Bilioni 104. Sasa tunasema hivi, lazima kila mmoja atekeleze wajibu wake, TAMISEMI isimamie lakini ni muhimu sana sana hili zoezi lihusishe Wataalam wa Mikopo jamani. Huku chini tunatoa *billions of moneys* halafu wanaoachiwa wasimamie ni Maafisa Maendeleo ya Jamii hawa wakinababa na wakinamama tunawapenda, lakini basi kwa sababu dhamira ni kutambua vikundi kwenye maeneo yetu, wawekeeni pia Wataalam wa Mikopo ili basi hili jambo liweze kwenda vema na kila mmoja aweze kunufaika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza jambo la pili ni kuhusu suala la utalii. Nami niende kwenye hii hoja ya kufuta msamaha wa VAT kwenye hizi ndege ndogo ndogo zinazobeba watalii. Mheshimiwa Waziri umefanya jambo ndiyo sawa, nzuri la kuahirisha miezi sita, lakini mimi kitu ninachojuiliza hivi kwanini Rais anaenda kulia na ninyi mnaenda kushoto? Rais ameamua kutibu tatizo lilitokuwepo, kwamba tulikuwa hatuna mikakati ya *BOOST*, utalii na kuutangaza duniani, amefanya na *Royal Tour One*, mimi naamini hiyo ni *one*, naamini kutakuja na *part two* kwa sababu naona haja-cover mambo utajiri watu naamini itakuja *part two*, Rais kafanya kazi yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi leo Rais anasema watu waje, wanakuja, tunaenda kutoa msamaha VAT kwenye ndege ambazo tunajua kwenye utalii wa kuwinda ndizo zinazotumika! *it doesn't make sense* yaani haingi akilini.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa Kamati imesema hapa vizuri kabisa, ndege za kukodi zimepungua katika kipindi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

cha miaka miwili kutoka 200 mpaka 105 yaani zimepindua
by 48% almost hivi kweli unaenda una-introduce VAT...

Mheshimiwa Spika, lazima ifike kipindi Mheshimiwa Waziri Mwigulu, kumiliki ndege siyo anasa! Shida ni kwamba *sometimes* sisi Watanzania tunafikiria kimaskini maskini sana, yaani tufikirie kwamba Ester Bulaya ama Mwigulu Nchemba kuwa na kile ka-*charter* cha abiria 14 ni kitu cha kawaida ili tushindanishe watu waruke huko hewani, watalii waje wabebewe hii lazima iwe *mentality* yetu. Tusifikirie kimaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mmeona watalii, amesema hapa rafiki yangu Mheshimiwa Reuben kwamba eti wametoka 45 mwaka jana sawa, wamefika 75 wameshaanza kuona *deal* lile haya, suala hili sasa hatutakiwi kufika huko! Hii sekta ya utalii mpaka Ianze kukua tunahitaji kuipa likizo ya milaka minne hivi mpaka ikue.

Mheshimiwa Spika, hawa watu wa ndege wanatuambia ukiilinganisha Tanzania, Zambia, Namibia, Botswana, wakati wenzetu, kwanza VAT zao ndogo lakini sisi tunavyozungumza sasa hivi ukiacha hii ya *charter VAT* kwenye masuala haya ya *hunting* ipo bado, kwenye bidhaa zingine ipo ukiacha ndege.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee kuna taarifa kutoka kwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

TAARIFA

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, nilipenda tu kumpa Taarifa msemaji anayesema ili ajenge hoja yake vizuri Zaidi, kwamba kimsingi katika kipindi tunachopitia ambapo sekta ya utalii ilipigwa na UVIKO-19 maana yake idadi ya watalii wakapungua, mikakati ambayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ingepaswa kutekelezwa kwa sasa ni pamoja na mikakati ya kupunguza kodi na siyo kuongeza kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia ni pamoja na mikakati ya kupunguza gharama za ndege kutua katika nchi yetu ili kushusha gharama ya Tanzania, kwa sababu Tanzani *has been labelled* kwenye sekta ya utalii kwamba ni *destination* ambayo inagharama kubwa sana kufanya utalii kitu ambacho kwa sasa kinegeswa kuwa *observed*. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, naipokea na ukizingatia alikuwa Waziri wa Maliasili na Utalii ninaachaje kupokea kwa mfano taarifa yeke. Kwa hiyo mimi ninaipokea na ninaamini Mheshimiwa Mwigulu anasikiliza. (*Makofii/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa mfano hapa, kwa mfano kwa *package* wakati wenzetu wanatoza VAT kwa chakula na malazi *food and accommodation* hizi nchi zote Zambia, Namibia, Botswana, kutohana na kutoza hivyo unakuta mtu analipa kwa siku labda kwa *trip* moja ama kwa abiria mmoja kwa ndege yake Dola 22, Dola 52, Dola 60, Dola 32 na hii ilikuwa ni Tanzania toka 2016 hatuja-*introduce VAT*.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania kwa *package* moja ambayo inaweza ika-*range* kwa Dola 1,500 hadi Dola 2,000 kila siku nazungumza kabla *introduction* hii VAT kwenye *charter*, analipa Dola 228 mpaka Dola 350 kila siku ya Mungu. Sasa uki-*introduce* na haka ka-*charter* tena si *double taxation* kwa mtu huyo huyo, kwa hiyo lazima unaambiwa *Tax kidogo, Tax less ili upate zaidi*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana ametoa miezi sita *well and good*, tunaamini miezi sita hii ni njia ya kuja kuifuta *completely*. Lakini la mwisho siyo kwa umuhimu masuala ya ushuru kwenye vi-*biscuit*, vipipi, vi-*chocolate* halafu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mnatudanganya ni afya! Mimi kila mtu hapa tokea tupo watoto wadogo, tuko shulenii vile vitu vinatupa *boost* wakati tunasubiri chakula! Hata hapa Bungeni tunavipiga sana vipipi hapa, sasa kama ndiyo hivyo, naongea kama mzaha lakini hili jambo lina madhara makubwa sana kwa viwanda vyetu nya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais anaenda nje anasema njooni muwekeze, hivi u-Swiss si ndiyo wanasisika duniani kwa *chocolate*, yaani ukisikia *chocolate* Swiss wanakosema halafu eti sisi tuko dhaifu *binhal!* Wazalishaji wetu wameanza kuzalisha *chocolate* za Kitanzania, mnatoa masharti makubwa ambayo mwakani viwanda vitazidi kufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, muda umeisha ningezungumza kwa kina ila ninaomba mno mliangalie hili, tufikirie kwa upana tuisue watoto wetu wa ndani, mazingira yetu ya kiblashara kiushindani ni tofauti na Kenya ni tofauti na India, huu ushuru mliowawekea nje *I can assure you*, kutokana na mazingira yao bado pipi zao zitakuwa *cheap*, bado *chocolate* zao zitakuwa *cheap*, bado *biscuit* zao zitakuwa *cheap*. Tutumie akili tusaidie Taifa, tuwasaidie Wawekezaji wetu wa ndani.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangila atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kipekee kabisa naomba nianze kwa kumpungeza Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kuhakikisha ya kwamba tunamtua Mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Spika, hii imeendelea kujidhihirisha kupitia mradi mkubwa wa Miji 28 ambaa una thamani zaidi ya Shilingi Triliioni Moja. Sambamba na hili tunafahamu kupitia llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi Serikali imejipanga kuhakikisha tunafikisha huduma ya upatikanaji

wa maji vijijini kwa asilimia 95 na kuimarisha upatikanaji wa maji vijijini utakuwa unafikia asilimia 85 na mijini utafikia asilimia 95. Hii inaendelea kuonyesha namna gani ambavyo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuhakikisha ya kwamba tunamtua Mama ndogo kichwani.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika mwaka huu mwezi Mei, 2022 huduma ya upatikanaji maji vijijini imefikia asilimia 74.5 na huduma ya upatikanaji maji mijini imefikia asilimia 86, hii inaendelea kuonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais anaenda kufanya changamoto yam aji hapa Tanzania kuwa historia.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu kabisa naomba niombe Serikali katika mwaka wa fedha ujao 2023/2024 waone namna gani ya kuweka msamaha wa kodi zinazotumia nishati ya jua yaani *solar water pumps* ili kuweza kurahisisha kufikisha maji kwa wakazi lakini vivyo hivyo kuweza kurahisisha kilimo cha umwagiliaji ambao ndiyo dira ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo la langu la pili naipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa *blue print* katika eneo la urahisishaji wa biashara ya *easy of doing business* kwa kuhamisha baadhi ya shughuli za utoaji viwango, kutoka kwenye taasisi za kisekta na kwenda *TBS* Shirika la Viwango Tanzania. Kwa mfano, katika Sehemu ya Tatu, Sehemu ya Saba, Sehemu ya 11, Sehemu ya 21, Sehemu ya 23, Sehemu ya 30 na Sehemu ya 32 ya Muswada huu wa Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, napata hofu kuhusu uwezo wa *TBS* kumudu na kubeba majukumu yote haya, ukizingatia ya kwamba majukumu haya yanahitaji uelewa, yanahitaji taaluma mambo ambayo yapo kwenye taasisi za kisekta na siyo *TBS*. Kwa mfano, suala la usalama wa chakula.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naelewa dhamira ya dhati kabisa ya Serikali kufanya hivi nikuongoa mgongano na muingiliano baina ya hizi taasisi za umma katika kusimamia biashara na wafanyabiashara. Kwa unyenyekevu mkubwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ninaiomba sana Serikali ipitie upya uamuzi huu ili kuhakikisha ya kwamba vinaendelea kusimamiwa na taasisi za kisekta.

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwa Serikali kwamba katika vifungu vyote hivi tajwa iongeze takwa kuwa kuwa viwango vitakavyowekwa na Taasisi za Kisekta viwe vimehuishwa, yaani kufanya *harmonize standards* na *TBS* iwe na jukumu la kuhakikisha kwamba viwango hivi vimeduwa *harmonized* na vimefuatwa, kwa kufanya hivyo tutaweza kuhakikisha ya kwamba taasisi za kisekta zinasimamia viwango na *TBS* inakuwa na jukumu lake la kuhakikisha kwamba viwango hivyo vimehuishwa na vimefuatwa, kulikoni hivi sasa kuweka mzigo mkubwa kwa *TBS* na hata hapa ilipo *TBS* inaelemewa na kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu naipongeza sana Serikali kuititia hii Ibara ya 135 ya Muswada wa Sheria huu wa Fedha ya kuamua kuondoa mzigo wa kulipa *SDL* kwa waajiri ambao wanatumia wanafunzi kwa muda (*Intern Students*) kwa Vyuo Vikuu. Uamuzi huu utatoa fursa kwa vijana wengi zaidi kuweza kupata ujuzi na uzoefu (*practical training*) lakini kwa unyenyekevu kabisa si tu vijana wanaosoma Vyuo Vikuu ambao wanahitaji kupata fursa hii, fursa hii iende kwa vijana wote, hivyo napenda kupendekeza kwa Serikali ifanye maboresho kidogo kuhakikisha ya kwamba msamaha huu wa ulipaji wa *SDL* inatolewa kwa Waajiri wote watakaotumia wanafunzi yaani *intern students* kutoka vyuo vyote ikiwemo vyuo nya katii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha naomba nirejee tena ili kutekeleza dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua Mama ndoo Kichwani, Serikali ihakikishe ya kwamba itatoa msamaha wa kodi katika *solar water pumps* hata kama haitakuwa katika mwaka huu wa fedha basi ihakikishe itafanya hivyo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwamba Serikali ione namna gani ya kubakisha jukumu la viwango kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

taasisi za kisekta na badala yake *TBS* isimamie kuhakikisha kama uhuishwaji umefanyika na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu Serikali ihakikishe ya kwamba huu msamaha wa waajiri ambaa watatumia wanafunzi wa ulipaji wa *SDL* uende kwa vyuo vyote na siyo tu Vyuo Vikuu ikiwemo Vyuo vya Kati ili iwe ni chachu ya kuhakikisha ya kwamba vijana wetu wote wanaweza wakapata ujuzi wa kazi kwa maana ya *practical training*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya, kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa usikivu mkubwa wa namna ambavyo anachukua maoni ya Wabunge na kuyafanya kazi na hii inaendelea kutupa sisi moyo Wabunge kuendelea kuishauri Serikali kwa tija, pia kwa *speed*kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni dhahiri kabisa malengo mengi ambayo tumejiwekea yataweza kutekelezeka kabla hata ya kufikia 2025 hivyo kuhakikisha kwamba njia yetu ya huko mbele itakuwa ni kuteremka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo kwa niaba ya akina Mama na Vijana wetu hapa Tanzania natoa shukrani za kipekee kabisa kwa Mheshimiwa Rais kwa kutoa ada, kwa kuhakikisha kwamba kutakuwa na elimu bila malipo ya watoto kuanzia chekechea mpaka kidato cha sita. Kwa maana hiyo imeuondolea mzigo sana familia na haswa akina mama ambaa huwa wanabeba jukumu sana la kulea na kutafuta fedha za hapa na pale za kuendesha mambo kadha wa kadha kwenye familia zetu. Hii inaonesha ya kwamba kwa sisi akina Mama tusiwe na woga wa kuendelea kuongeza familia, maana kuongeza watoto ni baraka na kupitia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan basi watoto wetu wasoma na sisi tuendelee kuongeza Watanzania ili tuwe wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na shukuru sana kwa fursa hii. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Shukrani sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukushukuru sana kupata fursa ya kuweza kuchangia *Finance Bill*. Mimi nitajielekeza kwenye maeneo mawili na kama muda utabaki nitaweza kuongelea pia kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kuhusiana na wawekezaji mahiri au wawekezaji maalum. Tunafahamu kwamba nchi yetu imekuwa na changamoto za muda mrefu sana kwenye upande wa uwekezaji. Nafurahi kuona kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan inachukua hatua madhubuti ili kuhakikisha kwamba inaweka mazingira mazuri sana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Rais kwenye hotuba zake nyingi amekuwa anasisitiza umuhimu wa Serikali kufanyakazi kama Serikali moja na tumeona kwenye hatua ambazo Wizara ya Fedha wamekuja nazo zinakwenda kutekeleza maelekeo haya ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba wapo wawekezaji ambao wamepata mikataba kwa muda mrefu kutoka *TIC* pamoja Wizara ya Uwekezaji. Hawa wawekezaji walifuata hatua zote zinazotakiwa, walitakiwa watume maombi *TIC* wakatuma maombi, wakatakiwa wasaini *performance contract* wakasaini *performance contract*, wakatakiwa baadaye wasuburi kikao cha kisheria kikae Kamati ya Kitifa ya Uongozi ambaye Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Waziri Mkuu wakaa wakakidhi vigezo. Sasa ikawa ni kazi ya Serikali sasa kuwapa kibali ili waendelee kufanya hizo shughuli.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi kufika mwaka 2014 Serikali yenye kaja ikabadilisha Sheria ya Kodi na Sheria yenye ni ya mwaka 2014 Sheria ya *Value Added Tax* waliibadilisha kama kipande wakaisahau Sheria ya Uwekezaji

huku Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, kupitia *TIC* umeingia mkataba anaruhusiwa kuendelea na shughuli zake, wakija *TRA* wanasema hapana sisi huo mkataba hatuufahamu, sisi tunachotaka mtulipe kodi zetu wakati Serikali ni moja na nchi ni moja.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kuona mwaka huu Serikali imekuja na mapendekezo ya kufanya maboresho kwenye *The Income Tax Act* lakini pia *The Value Added Tax Act*. Pamoja na kufanya maboresho bado wakasema kwamba pamoja na maombi yao kukubalika, pamoja na kusaini *performance contract*, pamoja na kupitishwa na kikao cha *NISC*, kabla ya Wizara ya Fedha kusaini lazima pia mambo haya yapitiwe na *Cabinet*. Mimi naona hili jambo ni jambo zuri ni jambo ambalo linataka wawekezaji wote wanaopitishwa lazima wapitie vigezo vyote, kwa sababu uklzungumza *Cabinet* Mwenyekiti wa *Cabinet* ni Rais, Mawaziri wote wako pale na mchakato kabla ya kwenda kule tunaamini vyombo vyetu na watu wote watakuwa wamejiridhisha, kwa hiyo huu mchakato ulioletwa ni mchakato sahihi na mimi binafsi ninauunga mkono na siyo mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata kwenye Sheria yetu ya *The Income Tax Act* ya mwaka 2021 na yenye pia Kifungu cha 10 (b) Kifungu Kidogo cha (2) *on public interest* wamesema kabisa *as may be approved by the Cabinet*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili siyo jambo la kwanza kwamba kutaka masuala yaende kwenye *Cabinet*. Mimi naunga mkono na kwa sababu Rais wetu ni kinara wa uwekezaji, amezunguka dunia nzima kushawishi wawekezaji, tunaamini kwamba jambo likienda mezani na yeye ndiyo Mwenyekiti hakuna mwekezaji ambaye atakwamishwa.

Mheshimiwa Spika, katika hilo ninayo mapendekezo:

Mheshimiwa Spika, pendeleko la kwanza tunaomba Wizara zote na Serikali wanapoleta mabadiliko ya sheria lazima wahakikishe wanafanya *harmonization* ya sheria siyo

wanakuja na sheria kipande kipande halafu mwisho wa siku wanaleta changamoto kwenye utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili ni kuhusiana na *TRA*. *TRA* ni kama Serikali inayojitegemea. Taratibu zikipitishwa, maelekezo yakipitishwa ukienda kwenye utekelezaji kwa sababu wao wanawekewa *target* wanakwenda nje ya maelekezo na tunayo mifano.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukiangalia sheria zetu *TRA* wanaruhusiwa kurudi nyuma kwenye kukusanya kodi si zaidi ya miaka mitano lakini tunayo mifano wamerudi zaidi ya miaka mitano kwenye maeneo mengi sana, hasa kwa miaka mitano iliyopita kumekuwa na vilio vingi vya wafanyabiashara, wafanyabiashara wengi walikata tamaa kwa sababu ya mchakato wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kuona Mheshimiwa Rais wakati alipokuwa Kagera, naweza nikamnukuu tarehe 10 Juni, 2022 alisema: “*Kwa hiyo wafanyabiashara walipe kuanzia mwaka jana, lakini kama ni miaka mitatu, minne au mitano nyuma, ulikuwa wapi yaani wanaulizwa TRA. Achaneni na hiyo biashara wapeni raha wafanyabiashara wafanye biashara zao. Sasa msisitize ukusanyaji wa mapato kuanzia tulipo, kwenda mbele, asitokee mfanyabiashara hakulipa kodi*”.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ndio kwenye hoja yangu, nilipata heshima ya kuwa Mkuu wa Mkoa katika nchi hii. Miaka yote Rais akitoa maelekezo Viongozi wote wa Serikali kazi yao ya kwanza ni kuji-align kuhakikisha kwamba maelekezo ya Rais yanatekelezwa, lakini sasa hivi tumeona yanaweza yakatoka maelekezo ya Rais, lakini bado wakakaa watu wakaanza kujadiliana na kuanzia kujipanga, kitu ambacho nadhani siyo sawa. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baada ya maelekezo haya ya Mheshimiwa Rais ambayo ameyatoa hadharani. Kwanza yeye anatakiwa atoe Waraka kwa *TRA*, wasikusanye kodi zaidi ya miaka miwili kama ambavyo Rais ameelekeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kazi ya pili pia ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tunamwomba alete Sheria hapa Bungeni, nimeangalia hii *Financial Bill* yote, sijaona mapendekozo ya mabadiliko ya Sheria hapa ya kuhusiana na maelekezo aliyotoa Mheshimiwa Rais. Mwisho wa siku sasa utekelezaji kule, utaenda kuwa ni mgumu. Kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tuletewe Muswada wa dharura au ikiwezekana tufanye marekebisho hapa ili haya maelekezo aliyotoa Mheshimiwa Rais ya kwamba kodi isikusanywe zaidi ya miaka miwili yawe ni maelekezo ya kisheria na wala yasiwe matakwa ya mtu au watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nisisitize hilo, lakini naunga mkono kabisa hii *Finance Bill*, lakini pia naunga mkono zaidi kwa sababu tunafahamu changamoto ya ajira ni kubwa sana. Tunaamini mazingira mazuri ya uwekezaji yakiwekwa basi tutaweza kuajiri watu wengi zaidi na mazingira ya Uongozi yatakuwa rahisi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa uwasilishaji wake mzuri na amekwenda mbali zaidi mpaka akatoa utani fulani hivi wa kimichezo. Nataka nimwambie tangu mapema kabisa kwamba furaha ambayo tumeishuhudia jana ni sawasawa na furaha ya nchi ambayo ilikuwa inatawaliwa kwa muda mrefu, sasa imepata uhuru. Wananchi wake huwa na furaha ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Naibu Waziri, Wataalam, Wadau mbalimbali na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti na Wabunge kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wamejadiliana kwa kina Muswada huu mpaka leo umewasilishwa na Kamati ya Bajeti imewasilisha taarifa yake

ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Kwa kweli tumepiga hatua kubwa sana, nikiangalia ile miaka ya nyuma jinsi ambavyo kulikuwa na misuguano wakati wa kujadili vipengele mbalimbali vya Sheria ya Fedha na ukilinganisha na mwaka huu ambao tumekuwa na mjadala mzuri wa maelewano mazuri katika hatua nyingi. Ni jambo la kumpongeza sana Mheshimiwa Rais ametoa wigo mpana kwa Mawaziri na Wataalam kuweza kujadiliana na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Ijumaa iliyopita tumepitisha Bajeti ya nchi hapa karibu trillioni 41.48, ni jambo ambalo tunatakiwa tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, hii ni bajeti yake ya kwanza kuiongoza tangu hatua za awali mpaka mwisho. Naunga mkono kama nilivyounga mkono bajeti ile, naendelea kuunga mkono kwamba sasa tuipe nyenzo ya utekelezaji bajeti ile ili iweze kutekelezeka. Bajeti ile ni nzuri na ndiyo maana hata wakati wa kuipitisha, wakati wa kujadili, kuanzia Wizara mpaka Bajeti Kuu hakuna shilingi iliyondolewa moja kwa moja. Kuna watu wa hapa na pale wakasema anaongezewa shilingi, wakarudisha. Kwa hiyo hakuna shilingi iliondolewa, maana yake ni kwamba bajeti ile ilipitishwa kwa asilimia mia moja na Bunge tangu mwanzo mpaka mwisho. Ni jambo ambalo leo naomba tuhitimishe kwa kuunga mkono Sheria hii ili iweze kwenda kutekeleza bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, pongezi yangu ya pili lazima nipongeze Bunge, kuanzia kwako mwenyewe Spika wetu, Naibu Spika, Wenyevitii wetu wa Bunge na Wabunge kwa ujumla kwa jinsi ambavyo walipokea na kujadili kwa kina mawasilisho yote ya Serikali na kuyapitisha, nawapongeza sana, sana.

Mheshimiwa Spika, kati ya zile fedha za Bajatei trioni 41.48 tulizopitisha, *TRA*, Wizara mbalimbali na Msajili wa Hazina na Halmashauri, wanatakiwa kukusanya trillioni 28.02, hizi ni fedha nyingi sana. Hata hivyo, kuna fedha nyingine ambavyo ni trillioni 13.46 hizi tutazitegemea kutoka kwenye misaada, mikopo nafuu na mikopo mingine ya ndani na nje. Sasa kwa kupitia marekebisho madogo ya Sheria ya

Dhamana za Serikali mikopo na Misaada, Sheria Na.30 ya mwaka 1974, ambayo tumeyafanya, naamini kwa umahiri wa Serikali yetu na hasa kwenye maeneo matano:-

(1) Eneo la kuimarisha demokrasia, hasa kupitia mazungumzo ya hivi karibuni kati ya CCM na vyama vingine vya Siasa yanayoendelea;

(2) Kuimarisha maelewano na maridhiano ya Kitaifa ikiwemo kufuta kesi za mwelekeo wa kisiasa;

(3) Mchango wa filamu ya *royal tour* katika utalii;

(4) Wiki iliyopita Chama cha Mapinduzi kukubali umuhimu wa mchakato wa Katiba mpya; na

(5) Rais kuifungua nchi kwa kuitangaza nje na kukaribisha uhusiano mzuri zaidi kati yetu na nchi nyingine duniani ikiwemo Mashirika ya Kiuchumi na Fedha ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, haya yote matano, yananifanya ni amini kwamba hakuna shaka yoyote kwamba hizi trillioni 13.46 ambazo tunazitegemea kwenye misaada na mikopo ya ndani na nje na mambo mengine, tutazipata zote na inawezekana zikaongezeka zaidi kama ilivyokuwa mwaka jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, niseme wazi kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. Tupitishe mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ambayo ndiyo tunaitegemea itumiwe na vyombo vyetu ikiwemo *TRA* kuhakikisha kwamba fedha ile trillioni 28.02 inapatikana. Maana yake kama tutaanza utaratibu wa kukwamisha baadhi ya vipengele vikasababisha tusipate hiyo trillioni 28.02, maana yake ni kwamba tunaweza tukajikuta tunakwamisha utekelezaji wa baadhi miradi ambayo ni muhimu sana ambayo tumeipitisha. Miradi hiyo ni kama vile miradi ya miundombinu; huduma za jamii kama elimu, afya, maji; uchumi katika Sekta ya Kilimo ambayo tumeongezewa bajeti.

Kwa hiyo kama tutakwamisha inawezekana tukakwamisha upatikanaji wa hizo trilioni 28.02.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imeyapitia mapendekezo ya marekebisho ya Sheria Na.38. Tumekubaliana katika maeneo mengi kimsingi, karibu asilimia 40, lakini Mamlaka ya kuitisha marekebisho haya ni Mamlaka ya Bunge chini ya Uwenyekiti wako.

Kwa hiyo kwa sababu haya marekebisho yote yalilenga kuhakikisha fedha zinazohitajika zinapatikana, kwa kweli, naomba sana tuwe pamoja katika kuiunga mkono marekebisho ambayo yamependekezwa na Waziri wa Fedha ili tuweze kuipa nguvu zaidi Serikali kuweza kukusanya hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, kuna marekebisho mengi ambayo ni mazuri, kwa mfano tumefanya marekebisho ya kuipa nguvu Sekta Binafsi kama injini ya uchumi ili ifanye kazi kwa ufanisi zaidi. Na hilo jambo ni jambo nzuri sana kwa uchumi wetu. Vilevile kupunguza mlolongo wa mamlaka za udhibiti kwenye eneo hasa la viwango ili kupunguza taasisi ambazo mfanyakishara anatakiwa kwenda kupata idhini, hilo ni jambo lingine ambalo ni zuri sana. *TBS* itakuwa na jukumu kubwa zaidi kwa hiyo Serikali itahitajika kujengea uwezo *TBS*, uwezo wa utaalam pamoja na vifaa. Kwa hiyo lazima kibajeti waangalie kuipa nguvu zaidi *TBS* ili isimamie vizuri suala la viwango.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni *TASAC* kuipunguzia baadhi ya kazi ambazo zilikuwa inaifanya, ambazo zinaweza kufanywa vizuri zaidi na Sekta Binafsi. Hili jambo ni zuri sana kwenye marekebisho haya. Tumekuwa tunapata malalamiko ya wadau wengi sana, wanalalamika kwamba sasa *TASAC* inafanya kazi zilezile ambazo zinafanywa na Kampuni Binafsi. Sasa kazi yake ni ku-regulate, kazi yake kudhibiti, badala yake amekuwa sasa ndiyo mchezaji katika uwanja. Kwa hiyo, hilo jambo la kupunguzia kazi badala yake abakiziwe zile kazi za kimkakati na zile

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambazo zinalenga usalama wa nchi, hilo ni jambo ambalo ni zuri sana kwenye marekebisho hayo ya sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna maboresho mengine mengi sana ambayo yanalenga kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara na wananchi kwa lengo la kuongeza utayari wa kulipa kodi na kuboresha mawasiliano kati ya walipa kodi na *TRA*. Hayo ni mambo ambayo ni mazuri sana. Kinachotakiwa kwa sasa tupunguze urasimu, kuna urasimu katika maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Spika, nilisafiri hapa kwenda Kenya mwezi Aprili, niliposafiri kwenda Kenya niliambiwa nipime *Rapid test*, ile *Rapid test* nilipofika uwanja wa ndege wa Tanzania kila mtu ananiuliza iko wapi, iko wapi, lakini nimefika uwanja wa ndege wa Kenya hakuna hata Afisa aliyeniuiliza *Rapid test*, nikailingia mpaka Hotelini hakuna urasimu. Nilivyorudi hapa Tanzania nchini kwangu, pale uwanja wa ndege wa Kenya hakuna aliyeuliza jambo lolote, kufika hapa naambiwa fungua fungua kupitia simu yako, fungua, yaani nusu saa nzima unaipoteza pale *airport*. Sasa hapo tunakuwa tunazuia hata utalii. Kwa hiyo pamoja na Kanuni ambazo tumejiwekea lakini lazima turekebishe hizi Kanuni zetu ziwe *supportive* yaani zilenge kutoa urahisi wa watu kuingia nchini na *ku-enjoy* kupata furaha katika nchi ya Tanzania badala ya lawama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno yangu hayo, naomba Wabunge wenzangu tupitishe sheria hii. Naunga mkono hoja ya Waziri na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa marekebisho mbalimbali ambayo ameyafanya na kuwa

msikivu na kutengeneza mazingira wezeshi katika kuiendesha nchi yetu na katika kufanya biashara na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kuja na Muswada kwa kweli ni Muswada ambaao ni mzuri sana, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kiponengeza Kamati ya Bajeti kwa namna walivyoichambua, wamechambua huu Muswada vizuri sana na wameweza kurekebisha mambo mengi. Mambo mengi wameyaweka vizuri na Serikali kwa sababu ni sikiu imeweza kuyachukua yote, kwa kweli tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa ushauri tu wa mambo kama mawili. Jambo la kwanza, duniani kote sasa hivi nchi nydingi zimeanza kufikiria kuondokana na kodi za moja kwa moja yaani *direct taxes*, zimeenda sasa kwenye kodi zisizionekana ambazo siyo moja kwa moja kwenye bidhaa na huduma yaani *indirect taxes*. Sababu ya msingi ya kuondoka huko inatokana kwamba hizi *direct taxes* zinaleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi. Kwa hiyo ukiziweka kwenye bidhaa bila kuonekana wananchi wengi wanalipa bila kujua kama wanalipa kodi. Ndiyo maana hata sasa hivi Watanzania karibu wote, wawe watoto, wawe wakubwa tunalipa kodi, lakini watu wengi wanasema Watanzania hawalipi kodi. Kodi tunazolipa kubwa kwa kiwango kikubwa ni zile ambazo siyo za moja kwa moja yaani *indirect taxes*, kila mtu analipa, kila Mtanzania analipa. Hizi za *direct taxes* ndiyo zenye shida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapendekezo mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri amekuja nayo na Muswada ulivyo, jambo moja ambalo nataka tuliangalie vizuri, kwamba tunataka kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma katika nchi. Tunapotaka kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma, vipo vitu vinavyosaidia uzalishaji uongezekere na gharama zisipande sana. Sasa kuna mapendekezo kwenye Muswada huu unaohusu masuala ya usafirishaji ambapo magari ya

mizigo kuanzia *excel* tatu na magari ya abiria yanaenda kutozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati ya Bajeti ilikuwa ni 3,500,000 imepungua lakini hajaisha, imepungua. Sasa hii maana yake nini? Kama hii itakwenda kama ilivyo inaenda kuweka maisha ya wananchi wa kawaida kuwa magumu. Uzalishaji gharama zinaenda kuongezeka, haya magari ya mizigo, ukichukua fuso, kenta, *pickup* na magari mengine ndiyo yanayoenda kuchukua bidhaa za wakulima huko vijijini na kuzileta kwenye soko, ndiyo yanayosafirisha bidhaa mbalimbali. Ukiweka kodi pale maana yake umeongeza gharama za uzalishaji, hasa gharama za uzalishaji zikipanda, maisha yatapanda gharama. Kwa hiyo, nafikiri hili suala tungeliangalia. Vivyo hivyo kwenye mabasi, kwenye mabasi wanaenda kuongeza hii kodi, sasa kwenye mabasi maana yake nauli za kawalda zitapanda.

Mheshimiwa Spika, hii nafikiri tungeliangalia vizuri tuone namna tunavyoweza kuiboresha, tunajua tunahitaji kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, kwa ajili ya kuendesha Serikali. Lakini tuangalie ni mbinu gani tunazitumia katika kutoza hizo kodi ili isiwe mzigo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka miaka ya nyuma ilikuwa ni usumbufu mkubwa sana, nakumbuka baba yangu alikuwa na *pickup* wakati ule, yeze kazi yake siyo kwamba *pickup* alikuwa anaifanya biashara, yeze kazi yake anataka awe anaiona tu. Wananchi wenzake, wanakijiji wanasema ana gari liko pale, mzee ana gari, anaiweka pale. Ile gari inaweza ikafanya mara moja kwa mwaka kwenda kupeleka mbolea shambani na kuchukua mavuno, basi. Sasa tukianza kusema kwamba hii tutoze kwa mwaka walipie kodi, nafikiri tungeliangalia namna ya kuiweka.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma kodi hizi tuliamua zikae kwenye mafuta, kwenye matumizi, kwa sababu ukiweka kwenye mafuta anapotaka kuitumia ile gari akinunua mafuta anaenda, tayari anakuwa amelipa hizo kodi. Kwa hiyo tuliondokana na *road license* zile ambazo walikuwa

wanalipa, tuliondoka na vitu vingine tukaviweka hapa. Sasa tunapokuja na hii kodi kuna uwezekano kukawa na *double taxation*. Sasa nafikiri waliangalie vizuri kama wataalam, waone namna itakavyoweza kusaidia katika kupunguza hizi gharama za uzalishaji ili nchi yetu iendelee kuwa na ushindani mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema, kama hili tusipoliangalia vizuri pamoja na magari yale ya wafanyabiashara wa nje ambao watakuwa wanalipa sasa hizi, zitaongeza gharama na zinaweza zikasababisha hata Bandari yetu ya Dar es Salaam isiwe na ushindani mkubwa. Hii ni kwa sababu wafanyabiashara wengine wa nje wanaangalia je, nikipitishia Mombasa, nikipitishia wapi, je, gharama zitakuwaje. Wakikokotoa wakikuta kwamba kwetu gharama zitakuwa ni kubwa tutapunguza mzigo ambao unaweza kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nashauri waliangalie vizuri sana hili ili tuweze kuboresha ili kusudi tuweze kuhakikisha kwamba gharama za uzalishaji zinapungua na maisha ya wananchi wa kawaida wa Tanzania waweze kusafirisha mazao yao, kusafirisha huduma zao na kuweza kupata huduma hizi kwa urahisi zaidi hiyo itasaidia sana na naamini tutakwenda vizuri. Kwa hiyo, nampongeza Waziri, nawapongeza Serikali, mambo mengi ya msingi wameshayapitisha, mambo mengi wameshayakubali, lakini haya machache hebu wayaangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ambalo nataka kupendekeza, tuangalie uwezekano, sasa hivi mkazo ni kuimarisha uwekezaji kwenye nchi. Sasa ni vizuri wakapitia Sheria zote, Kanuni zetu zote, zinazoweza kuwa ni kikwazo kwenye uwekezaji zaidi. Wakizipitia zile tuzirekebishe, tukizerekebisha zitatusaidia kuongeza uwekezaji, uzalishaji, pato la Taifa, tutakabiliana na upungufu wa ajira kwenye nchi, lakini pia maisha ya watanzania yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru kwa kunipa hii nafasi. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa maana ya wale waliyokuwa wameomba kuchagiaji kwa asubuhi kwa sehemu ya kwanza ya Mkutano wetu kwa siku ya leo.

Sasa mchango wa Mheshimiwa Hasunga, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hamjaletewa bado marekebisho haya ambayo yamefanywa na Serikali kwa yale mapendekozero ambayo yalikuwa yameletwa na makubaliano yao na Kamati ya Bajeti, kwa maana ya marekebisho yanayotakiwa kufanywa, ndiyo maana nimemuacha amalizie mchango wake bila kumjulisha hapo katikati.

Ninayo hapa marekebisho, nadhani tutakapopewa tufuatilie hii hoja ya Mheshimiwa Hasunga, kwa sababu amealeleza kwa namna ambayo na nafafanua ili waandishi wetu wapate picha, wasije wakaanza bajeti juu imeanza na mambo kama hayo. Kwa hiyo tutaanza tena hapa kusema wamepotosha, lakini marekebisho yanayoletwa na Serikali yana sehemu ambayo yanaonyesha; mwanzoni kabisa ilikuwa fedha ambayo ingekuwa inadaiwa kwenye hayo magari ilikuwa iwe 3,500,000. Hapa kwangu inasomeka kwa mwaka, sijajua kama ndiyo huo utaratibu kwenye ile ambayo mlikuwa mmeileta mwanzo imeandikwa kwa mwaka na sasa hayo marekebisho yanasema hivi; magari yale ya kubeba mizigo yameweka sasa utaratibu wa kuanzia tani sifuri mpaka tani moja, halafu mpaka tani 25 kodi zinatofautiana. Kwa hiyo kuna sifuri mpaka moja, halafu moja mpaka tano, halafu sita mpaka 10, kuanzia 11 mpaka 15, kuanzia 16 mpaka 20, halafu 21 mpaka 25, halafu 25 na kuzidi. Hizi zinatoka kuanzia sasa kiasi cha chini kabisa ni 180,000 mpaka 2,790,000 kwa magari ya mizigo. Kwa hiyo yanategemea ule uzito wa mzigoto uliyobebwa na aina pia ya gari.

Kwa hiyo nadhani ile picha ambayo Mheshimiwa Hasunga alikuwa hana, pengine mchango wake ungekuwa tofauti kama angekuwa nayo hii. Kwa hiyo yale maneno ya kwamba, mzigoto utawaendea wananchi kwa sababu ya uzito wa kodi hii yanakuwa yamepunguzwa sana, kwa sababu

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sasa pia gari haiwezi kufanya kazi bila kulipa kodi kabisa. Hii kodi imewekwa kwa muktadha huo. Pia vivyo hivyo kwa mabasi kwa sababu ameeleza kwamba kodi hii ikiachwa maana yake watu wataanza kulipa nauli kubwa zaidi.

Sasa nafafanua hivi kwa sababu haya marekebisho Waheshimiwa Wabunge bado hamjapewa, lakini Ofisi imeshayapokea marekebisho ya Serikali kwa ushauri ambao wamepewa na Kamati yetu ya Bajeti. (*Makofi*)

Kwa upande wa magari yanayobeba abiria vivyo hivyo, hawa wamewekewa sasa siyo kwa tani ila kwa idadi ya abiria. Kwa hiyo na wenyewe mabasi yanatofautiana kiwango cha kodi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge hilo ni muhimu kulifahamu, nimefanua hivi ili lisije likaleta picha kwamba kuna eneo ambalo huko kote kodi mambo yameenda vizuri isipokuwa hapa kwenye magari ya abiria lakini pia magari ya mizigo. Kwa hiyo Kamati yetu ya Bajeti wameishauri vizuri Serikali na Serikali imeafikiana na ushauri wao wameweka hapa viwango vinavyotofautiana kutokana na ukubwa wa gari au idadi ya abiria kwa yale magari ya abiria. Kwa hiyo marekebisho haya yatakapokuja, wakati sasa tunapotunga sasa hii sheria, tutakuwa tukiyapitia haya marekebisho ya Serikali na kuona wapi ambapo tunaona bado pana changamoto.

Kwa uzito ule wa mchango wa Mheshimiwa Hasunga nimeona nitoe ufanuzi huo ili isije ikaenda picha huko nje kwamba Muswada huu wa Sheria ya Fedha una hilo eneo ambalo limeleta mzigo kwa wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi. (*Makofi*)

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilihahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 28 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*